# MASUALA YA KISIASA KATIKA USHAIRI WA KANDORO: MIFANO KUTOKA KATIKA MASHAIRI YAKE

**MOHAMED KHALFAN YUNUS**

**TASINIFU YA PHD KATIKA KISWAHILI**
**CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**
**2013**

# MASUALA YA KISIASA KATIKA USHAIRI WA KANDORO: MIFANO KUTOKA KATIKA MASHAIRI YAKE

**MOHAMED KHALFAN YUNUS**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA MASHARTI YA DIGIRII YA PHD. KATIKA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHATANZANIA**
**2013**

## UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma Tasinifu hii iitwayo: ***Masuala ya Kisiasa Katika Ushairi wa Kandoro: Mifano Kutoka Katika Mashairi Yake,*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digirii ya Uzamivu katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

----------------------------------------

Prof. Dkt. Sheikh, T.S.Y Sengo

(Msimamizi)

----------------------------

Tarehe

## IKIRARI

## NA

## HAKIMILIKI

Mimi, **Mohamed Khalfan Yunus,** nathibitisha kuwa, Tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Digirii yoyote.

**Sahihi**........................................................

Haki ya kunakili Tasinifu hii inalindwa na mkataba wa Berne, Sheria ya haki ya kunakili ya mwaka 1999 na mikataba mingine ya sheria za kitaifa na kimataifa zinazolinda mali ya kitaaluma. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama yote au sehemu ya Tasinifu hii, isipokuwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## SHUKURANI

Leo ninayo furaha kubwa moyoni mwangu kwa kufikia hatua hii katika uandishi wa tasinifu hii na masomo yangu ya Uzamivu kwa ujumla. Aliyeniwezesha kufikia hatua hii ni Allah Subhanahu Wataalah anayepaswa kushukuriwa kwa dhati ya kushukuriwa. Ninamshukuru Allah kwa kunijaalia afya njema katika kipindi chote cha masomo yangu. Kwa uchache kabisa nasema Alhamdulillahi Rabbilaalamina.

Shukrani za pili nazitoa kwa familia yangu iliyoko Libya kwa msaada wao mkubwa kwangu ulionisaidia kufika hapa nilipofika. Shukurani za pekee ziwafikie baba na mama yangu ambao ndio walionileta hapa ulimwenguni. Pia napenda kumshukuru mke wangu kwa uvumilivu aliouonesha kwangu katika kipindi chote cha masomo yangu Tanzania na yeye akiwa Libya. Wote kwa pamoja ninasema kwamba sina cha kuwalipa ila Allah ndiye atakayewalipa.

Shukurani zangu za tatu nazitoa kwa msimamizi na mwalimu wangu sheikh, dkt, prof. T.S.Y.Sengo ambaye amefanya kazi kubwa ya kuniongoza katika uandishi wa tasinifu hii mpaka kukamilika kwake. Kila mara alinitia moyo kwamba siku moja nitamaliza masomo haya kwa kufanya juhudi kubwa pasina kuchoka.

Mwisho napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa wanataalimu wote wa idara ya Isimu na Taalimu za Fasihi kwa maoni yao, muongozo wao ulionifikisha hapa nilipofika. Si rahisi kuwataja wote ila kwa niaba yao naomba niwataje wafuatao: prof. E. Mbogo, Dkt. P.P. Lipembe, H. Pembe, H. Jilala na Mama H. Simpassa. Ninasema asanteni sana.

## TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa **Mama yangu Mzazi pamoja na familia yangu yote**. Pia ninaitabaruku kazi hii kwa wananchi wote wa Libya.

# YALIYOMO

Uthibitisho....................................................................................................i

Ikirari na Hakimiliki .........................................................................................ii

Shukurani .......................................................................................................iii

Tabaruku .........................................................................................................iv

Yaliyomo..........................................................................................................v

Ikisiri ...............................................................................................................xi

Vifupisho........................................................................................................xii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI NA USULI WA TATIZO LA UTAFITI.1**

1.1 Mada ya Utafiti ..........................................................................................1

1.1.1 Usuli wa Mada ..........................................................................................1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti...........................................................................1

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti..........................................................................6

1.4 Lengo Kuu la Utafiti ..................................................................................6

1.4.1 Madhumuni Mahususi ..............................................................................6

1.4.2 Maswali ya Utafiti.....................................................................................7

1.5 Umuhimu wa Utafiti ..................................................................................7

1.6 Mipaka ya Utafiti .......................................................................................8

1.7 Vikwazo vya Utafiti...................................................................................9

1.7.1 Utatuzi wa Vikwazo....................9
1.8 Mpango wa Tasinifu....................10
1.9 Muhutasari....................10

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI....................11**

2.1 Utangulizi....................11
2.2.1 Dhana ya Ushairi....................11
2.2.2 Ushairi wa Kiswahili....................12
2.2.3 Dhana ya Shairi....................13
2.2.4 Siasa....................14
2.2.5 Sitiari....................14
2.2.6 Ishara....................14
2.2.7 Taswira....................15
2.3 Siasa katika Ushairi kwa Ujumla....................15
2.4 Siasa katika Ushairi wa Kandoro....................23
2.5 Historia Fupi ya Kandoro....................27
2.7 Muhutasari....................30

**SURA YA TATU: NADHARIA ZA UHAKIKI WA FASIHI....................31**

3.1 Utangulizi....................31

3.2 Nadharia ya Simiotiki ............ 31

3.3 Nadharia ya Umarx ............ 33

3.4 Nadharia ya Ufeministi ............ 34

3.5 Muhtasari ............ 35

**SURA YA NNE: MBINU ZA UTAFITI ............ 36**

4.1 Utangulizi ............ 36

4.2 Usanifu wa Utafiti ............ 36

4.3 Watafitiwa ............ 37

4.4 Usampulishaji wa Watafitiwa ............ 37

4.5 Vyanzo vya Data ............ 38

4.5.1 Data za Msingi ............ 38

4.5.2 Data za Upili ............ 38

4.6 Ukusanyaji wa Data ............ 39

4.6.1 Uchambuzi wa Kimaudhui ............ 39

4.6.2 Mbinu ya Usaili ............ 40

4.7 Uchambuzi wa Data ............ 40

4.8 Mkabala wa Kidhamira ............ 41

4.9 Uhalali, Kuaminika na Maadili ya Utafiti ............ 42

4.9.2 Kuaminika kwa Data ............ 42

4.10 Maadili ............ 43

4.11 Muhutasari ........................................................................................43

**SURA YA TANO: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA ........................................................................................44**

5.1 Utangulizi........................................................................................44

5.1.1 Kandoro na Harakati za Kupigania Uhuru..........................................44

5.1.2 Kandoro Muhamasishaji wa Kisiasa..................................................50

5.1.3 Kandoro na Masuala ya Elimu..........................................................58

5.1.4 Kandoro na Masuala ya Haki...........................................................62

5.1.5 Kandoro na Umiliki wa Ardhi ..........................................................64

5.1.6 Kandoro na Suala la Rushwa ...........................................................66

5.1.7 Kandoro na Dhuluma katika Jamii ....................................................68

5.1.8 Kandoro na Umasikini katika Jamii...................................................71

5.1.9 Kandoro na Demokrasia ..................................................................74

5.1.10 Hitimishi ......................................................................................78

5.2 Ushairi wa Kandoro Katika Kipindi cha Uhuru......................................79

5.2.1 Utangulizi......................................................................................79

5.2.2 Kufanya kazi kwa Bidii ...................................................................79

5.2.3 Kandoro na Uongozi wa Nchi............................................................81

5.2.4 Kandoro na Masuala ya Kijinsia........................................................83

5.2.5 Kandoro na Kuweka Akiba................................................................85

5.2.6 Kandoro na Maisha Bora ........................................................................87

5.2.7 Kudumisha Amani ................................................................................89

5.2.8 Kandoro na Ujamaa na Kujitegemea ...........................................................90

5.2.9 Mapenzi Kwa Taifa..................................................................................97

5.2.10 Kandoro Mshereheshaji wa Sera za Maendeleo ...........................................98

5.2.11 Afrika ni Moja.....................................................................................100

5.2.12 Kandoro na Ushairi wa Kiswahili...............................................................101

5.2.13 Kandoro na Masuala ya Dini ...................................................................105

5.3 Mbinu za Kisanaa katika Ushairi wa Kandoro ............................................108

5.3.1 Utangulizi.............................................................................................108

5.3.2 Matumizi ya Lugha .................................................................................108

5.3.3 Uchanganyaji wa Lugha katika Ushairi wa Kandoro ..................................109

5.3.4 Tamathali za Usemi katika Ushairi wa Kandoro ........................................110

5.3.4.1 Tashihisi.............................................................................................110

5.3.4.2 Taswira na Ishara ..................................................................................111

5.3.4.3 Marudiorudio .......................................................................................112

5.3.5 Matumizi ya Wahusika ............................................................................114

5.3.6 Matumizi ya Mandhari katika Ushairi .........................................................116

5.3.7 Matumizi ya Lugha ya Mkato.....................................................................118

5.3.8 Mwingiliano Matini .................................................................................119

5.3.9 Mbinu ya Mazungumzo katika Ushairi........................................................120

5.3.10 Muundo katika Ushairi wa Kandoro............................................................122

5.3.11 Mtindo katika Ushairi wa Kandoro.............................................................124

5.3.12 Usimulizi Katika Ushairi wa Kandoro.........................................................126

5.3.13 Muhutasari .....................................................................................................127

5.4 Falsafa Katika Ushairi wa Kandoro.............................................................128

5.5 Muhutasari .....................................................................................................133

**SURA YA SITA: MUHUTASARI, HITIMISHI NA MAPENDEKEZO..........135**

6.1 Utangulizi.......................................................................................................135

6.2 Muhtasari ......................................................................................................135

6.3 Hitimishi .......................................................................................................138

6.4 Mapendekezo ................................................................................................145

**MAREJELEO ......................................................................................................147**

**VIAMBATISHI.....................................................................................................155**

## IKISIRI

Nia kuu ya utafiti huu ilikuwa ni kuchunguza masuala ya kisiasa katika ushairi wa Kandoro kwa kutolea mifano mashairi yake. Nia hii kuu imeweza kufanikiwa kutokana na kukamilika kwa madhumuni mahususi matatu ambayo ni: kuainisha dhamira za kisiasa zinazojitokeza katika ushairi wa Kandoro, kueleza mbinu za kisanaa zinazotumiwa na Kandoro katika kuibua masuala ya kisiasa na kubainisha falsafa ya Kandoro kama inavyojitokeza katika ushairi wake. Ili kuwezesha malengo haya kukamilika tumefanya mapitio ya kazi tangulizi zinaohusiana na mada ya utafiti, tumeainisha nadharia zilizoongoza utafiti wetu na baadaye kuainisha mbinu za utafiti zilizotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, Kandoro anaeleza dhamira za kisiasa zinazohusiana na ukombozi wa Mwafrika kutoka katika mikono ya wakoloni na kuweza kujitawala mwenyewe. Ili kufanikisha jambo hili Kandoro anawataka wananchi kuungana pamoja katika kudai uhuru wao. Aliwataka kufanya hivyo kwa kujiunga na chama cha TANU ili kukipa nguvu ya ushindi dhidi ya wakoloni. Baada ya kupatikana kwa uhuru Kandoro aliwataka wananchi kufanya kazi kwa bidii ili kujiletea maendeleo endelevu. Kazi kubwa aliyoihimiza bwana Kandoro ni kilimo ambacho kilitamkwa kuwa ndio uti wa mgongo wa uchumi wa taifa na hayati baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere. Matokeo ya utafiti yanaonesha pia kuwa, dhamira hizi za kisiasa zimeweza kuwafikia wasomaji kutokana na matumizi mbalimbali ya mbinu za kisanaa kama vile matumizi ya lugha ya kitamathali, wahusika, muundo, mtindo na kadhalika katika mashairi ya Kandoro. Vilevile, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, Kandoro ana falsafa ya kimapinduzi, utu, ujamaa na kujitegemea. Mwishoni mwa utafiti huu tumetoa mapendekezo kwa ajili ya tafiti zijazo.

## VIFUPISHO

**CCM** - Chama Cha Mapinduzi

**CHADEMA** - Chama Cha Demokrasia na Maendeleo

**DUP** - Dar es Salaam University Press

**IDS** - Institute of Development Studies

**IKR** - Institute of Kiswahili Research

**JKF** - Jomo Kenyatta Foundation

**MNF** - Mwalimu Nyerere Foundation

**MNP** - Mkuki na Nyota Publishers

**NPL** - National Publishers Limited

**OUP** - Oxford University Press

**TAA** - Tanganyika African Asociation

**TANU** - Tanganyika National Unity

**TPH** - Tanzania Publishing House

**TATAKI** - Taasisi ya Taaluma za Kiswahili

**TUKI** - Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI NA USULI WA TATIZO LA UTAFITI

## 1.1 Mada ya Utafiti

Utafiti huu unafanyika chini ya anuani isemayo: Masuala ya Kisiasa Katika Ushairi wa Kandoro: Mifano Kutoka Katika Mashairi Yake.

### 1.1.1 Usuli wa Mada

Mada hii imeteuliwa kwa sababu hakuna utafiti wa kina wa kifasihi uliokwisha fanyika katika kuchunguza masuala ya kisiasa katika ushairi wa Kandoro. Mada hii ni muhimu kufanyiwa utafiti kwa sababu siasa za leo zimekuwa ni za utapeli, rushwa, ufisadi na wizi wa mali za wananchi ikilinganishwa na ilivyo kuwa katika enzi za utawala wa Mwalimu Nyerere. Utafiti huu utasaidia kutoa mapendekezo juu ya namna siasa za enzi za mwalimu zilivyokuwa zinafanyika na nini hasa zililenga kuwafanyia wananchi. Sababu hizi ndizo kwazo zilizofanya uteuzi wa mada hii ya utafiti kufanyika.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Ushairi ni sanaa ya lugha ya mkato yenye ubunaji, inayosawiri, kuonesha au kueleza jambo, hisi au hali kwa namna yenye kuvutia hisia, katika mpangilio mahususi wa maneno wenye urari wa mizani. Ushairi kwa upande wa utafiti huu unachukuliwa kama ni utanzu wenye historia ndefu hususani katika fasihi ya Kiswahili. Wamitila (2008) anasema kwamba: Wataalamu mbalimbali wanakubaliana kwamba ushairi ndio utanzu wenye historia ndefu kuliko tanzu nyingine za fasihi. Kutokana na ukweli huu ushairi umekuwa ukitumika kama chombo cha kuelezea masuala ya kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi. Itakumbukwa pia ushairi ulitumika kama

chombo cha kutolea elimu kwa wananchi kabla ya ujio wa mfumo wa elimu wa Kimagharibi. Hivyo basi, tunaweza kueleza kwamba: Ushari umetumika katika vipindi mbalimbali vya maisha ya Mtanganyika na baadaye Mtanzania katika harakati za kujikomboa kisiasa, kiutamaduni, kijamii na kiuchumi. Katika utafiti huu tunazungumzia ushairi kama chombo cha ukombozi wa kisiasa katika jamii na kwa kuanzia tunazungumzia namna ushairi ulivyotumika katika kipindi kabla ya ujio wa wakoloni.

Waafrika walikuwa na aina yao ya utawala uliongoza jinsi watu wote katika jamii hizo walivyopaswa kuishi. Utawala huu ulikuwa ni wa Kichifu ambapo Chifu alipewa mamlaka na madaraka ya kuongoza jamii ya watu wake katika uzalishaji mali, utoaji wa huduma mbalimbali kama vile; elimu, afya, ulinzi na usalama kwa wananchi wake. Ili chifu aweze kuyafanya haya yote alihitaji kuwa na uwezo wa kifedha, mali na watumishi wa kumsaidia katika utendaji wa kazi zake. Upatikanaji wa fedha na mali ulitokana na wananchi wenyewe ambapo kupitia kodi na sadaka mbalimbali walizopeleka kwa Chifu, Machifu walipata utajiri mkubwa ambao kwao ndio walioutumia katika kuisaidia jamii kupata huduma mbalimbali pale panapokuwa na majanga kama vile; moto, mafuriko, maradhi na njaa. Ni katika kipindi hiki ushairi simulizi ulitumika katika kuwasifu Machifu kwa ushujaa wao pamoja na mambo mengine kuweza kuisaidia jamii yao pale inapopatwa na shida (Mulokozi; 1986). Katika kipindi hiki zilitungwa, tendi kama vile utendi wa *Mugasha*, *Kachenywanja*, *Sundiata* na *Nyakiiru Kibi* kutaja tendi chache ambazo hasa ziliwasifu Machifu na kuwaonesha kwamba wao ni watu muhimu katika kuisaidia jamii ya watu wao. Hata hivyo, hatujapata kukutana na utendi au aina

nyingine ya ushairi iliyokuwa ikipinga ama kutokubaliana na utawala wa Kichifu ingawa tunatambua kwamba ulikuwepo. Miongoni mwa sababu kubwa ya kukosekana kwa ushairi huo ni kwamba: yeyote aliyebainika kuupinga utawala wa Chifu kwa namna yoyote ile alichukuliwa hatua kali za kisheria, mojawapo ikiwa ni kunyongwa.

Baadaye katika miaka ya 1884 na kuendelea walikuja wakoloni na kutawala Afrika na kuigawanya katika makundi yaliyoitwa Makoloni. Tanganyika lilikuwa ni mojawapo ya Makoloni yaliyokuwa chini ya himaya ya Ujerumani tangu 1884-85 mpaka 1918 na chini ya Uingereza kuanzia 1919-1960. Ujerumani ilitawala Tanganyika kwa mabavu na ubabe dhidi ya raia wa Tanganyika. Wananchi walilimishwa mashamba makubwa kwa ujira mdogo. Vilevile, wananchi walinyang'anywa mashamba yao yaliyokuwa na rutuba na kuachiwa ardhi isiyofaa kwa kilimo. Pia wananchi walilipishwa kodi mbalimbali kwa manufaa na masilahi ya mkoloni na pale walipokataa kufanya kazi hizo walilazimishwa na kuadhibiwa vikali.

Kwa msingi huu, washairi waliandika mashairi yao kuonesha kutoridhishwa na hali hiyo. Hata hivyo, bado ushairi simulizi ndio ulitawala katika kipindi hiki (Mulokozi, 1982). Kwa mfano: Katika kipande cha shairi *Mzungu Migeli,* inadokezwa:

*Mzungu Migeli*
*Mzungu Migeli umwongo*
*Mato yako yanatongo*
*Kwani kuata mpango*
*Kwenda kibanga uani* (Kitogo, 2002).

Inasemekana kwamba, shairi hili ni la kisimulizi ambalo liliimbwa kwa minajili ya kuupiga utawala wa kikoloni wa Kireno. Utawala huu uliahidi kuondoka nchini na kuwaachia wananchi uhuru wao lakini muda ulizidi kwenda bila kuondoka ndio maana washairi wakaanza kutunga na kuimba mashairi kama haya. Utawala wa Kijerumani ulikuwa ni wa udikteta wa hali ya juu ambapo mshairi yeyote aliyeandika shairi kuupinga utawala huo alikamatwa na kufungwa magereza ama kunyongwa. Hali hii iliwafanya baadhi ya washari kuwa waoga katika utunzi wao wa mashairi. Shaaban Robert ni mmoja wa washairi hao aliyeandika shairi la “Woga” lipatikanalo katika *Kielezo cha Fasihi:*

*Nina asili ya woga, woga wangu wa tabia*
*Nikenda nalegalega, sina nguvu napeapea*
*Bali sarara na kinga, mawindoni huchukua.*

Pamoja na hali ya woga aliyokuwa nayo haikumfanya aache kutunga kazi za fasihi zenye kuelezea madhila ya wakoloni la hasha! Badala yake alibuni mbinu mbadala ya uandishi; nayo ni ile ya kutumia nadharia za kidhanaifu. Kupitia nadharia hizi aliandika *Kusadikika na Kufikirika* zilizochambua na kuuanika hadharani uovu wa mkoloni kwa wananchi wa Tanganyika na kwingineko duniani.

Washairi wengine walianza kujitokeza katika harakati za kudai uhuru ambapo Kandoro alikuwa ni kinara wao. Aliandika mashairi mbalimbali kama vile “*Kwetu ni kwao kwa nini*”, “*Siafu Wamekazana*” na *Kura Tatu,* akiwahimiza wananchi kuungana pamoja ili kumuondoa mkoloni. Mashairi yake mengi yalionekana katika magazeti ya *Mamboleo,* na *Baragumu*. Katika kipindi hiki pia walikuwepo washairi wengine kama vile Mathias Mnyampala, Kaluta Amri Abeid, Mwalimu Kihere, Mzee Waziri Kijana, Komba na Abdalatifu Abdallah kuwataja wachache. Washairi

hawa kwa pamoja waliandika mshairi ya kuwahamasisha wananchi kuungana pamoja na kamwe kutorudi nyuma katika harakati za kudai uhuru.

Baada ya kupatikana kwa uhuru Kandoro aliendelea kutunga mashairi mengi yanayohusiana na masuala ya kisiasa, shairi la *Tumshukuru Manani*, ni moja ya mashairi yaliyotungwa kumshukuru Mwenyezi Mungu baada ya kuwezesha kupatikana kwa uhuru. Katika kipindi hiki pia Kandoro anaandika shairi *Kujitawala Kugumu,* akimaanisha kwamba watu wasifikiri kupatikana kwa uhuru kutaleta maendeleo kirahisirahisi na harakaraka tu, bila kufanya kazi kwa bidii. Katika shairi hili anawataka wananchi kushirikiana kwa karibu na serikali yao ili kujiletea maendeleo. Ushirikiano huo, ulihimizwa katika Azimio la Arusha lililotangazwa mwaka 1967. Azimio hili lilianzisha rasmi siasa za Ujamaa na Kujitegemea. Kandoro aliandika kitabu cha ushairi kilichoitwa *Liwazo la Ujamaa* ndani yake kukiwa na mashairi yanayozugumzia nia njema ya serikali ya kuanzisha ujamaa na kuwahamasisha wananchi kuunga mkono siasa hizo. Bila shaka wengi wa wananchi walikubali ujamaa ambapo mwaka 1976 vilianzishwa vijiji vya Ujamaa na Kujitegemea. Kandoro kama kawaida yake alitunga mashairi mengi kuusifu ujamaa lakini hakuandika kuhusu mapungufu yake (ujamaa). Pamoja na kufanya kazi kubwa ya uandishi wa mashairi ya kisiasa katika vipindi tofautitofauti vya maendeleleo ya Tanganyika na baadae Tanzania hakuna utafiti wa kina uliofanyika kutathimini mchango wa Mashairi ya Kandoro katika kuelezea, kuchambua na kudadavua masuala ya kisiasa kwa mtazamo wa kifasihi katika ushairi wake. Utafiti huu umefanywa ili kushughulikia pengo hili la utafiti katika ushairi wa Kiswahili kipitia ushairi wa Kandoro.

## 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Saadan Kandoro ni mmoja wa watunzi wa mashairi aliyepata kusifika na kuheshimika sana katika enzi zake. Kusifika na kuheshimika huko kulitokana na utunzi wake wa ushairi uliogusa nyoyo za hadhira yake kutokana na ufundi wake katika kuimudu fani ya ushairi wa Kiswahili. Hakuwa mtaalamu wa kumudu fani peke yake bali pia dhamira na ujumbe ulioongozwa na falsafa ya kiuanaharakati, utu na mapinduzi. Ushairi wake unaeleza masuala ya kisiasa katika vipindi tofautitofauti vya maendeleo ya Tanganyika na baadaye Tanzania katika kipindi cha ukoloni, harakati za kudai uhuru na baada ya uhuru. Pamoja na masuala ya msingi na muhimu yanayojadiliwa katika ushairi wake amesahaulika si tu kwa wanataaluma lakini pia wanasiasa ambao leo hii wanafanya madhila ya rushwa yalipingwa vikali na Saadani Kandoro katika ushairi wake. Utafiti huu unafanywa ili kubainisha masuala mbalimbali ya kisiasa yanayoibuka katika ushairi wa Kandoro ili kuziba pengo hili la kiutafiti linaloonekana kuwa wazi kuhusu ushairi wa Kiswahili na masuala ya kisiasa kupitia ushairi wa Kandoro.

## 1.4 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kubainisha masuala ya kisiasa yanayojitokeza katika ushairi wa Kandoro.

### 1.4.1 Madhumuni Mahususi

Ili kufanikisha lengo kuu la utafiti huu madhumuni mahususi yafuatayo yanapaswa kukamilishwa.

(a) Kubainisha masuala ya kisiasa yanayojitokeza katika ushairi wa Kandoro.

(b) Kuchunguza mbinu za kisanaa zinazotumiwa na Kandoro katika kujenga masuala ya kisiasa katika ushairi wake.

(c) Kueleza falsafa ya Kandoro kama inavyojitokeza katika ushairi wake.

### 1.4.2 Maswali ya Utafiti

Ili kuwezesha kukamilika kwa madhumuni mahususi ya utafiti huu, maswali yafuatayo yanahitaji kujibiwa.

(a) Ni masuala gani ya kisiasa yanayojitokeza katika ushairi wa Kandoro?

(b) Ni mbinu zipi za kisanaa zinazotumiwa na Kandoro katika kujenga masuala ya kisiasa?

(c) Ni zipi falsafa za Kandoro kama inavyojitokeza katika ushairi wake?

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utatoa umuhimu katika nyanja za kitaalimu, kisiasa, kiutamaduni, kijamii na kiuchumi. Tunaanza kueleza umuhimu wa kitaalimu.

Kwa upande wa taalimu: utafiti huu utakuwa rejeleo muhimu kwa watafiti na wanafunzi wanaojihusisha na taalimu ya fasihi ya Kiswahili, utamaduni na historia ya harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na kuendelea. Vilevile, utafiti huu utatia chachu ya kufanyika utafiti zaidi kumhusu Kandoro na ushairi wake.

Kisiasa: Utafiti utakuwa na umuhimu wa kufafanua kuhusu masuala ya kisiasa yaliyokuwa yakifanyika katika kipindi cha ukoloni na enzi za utawala wa Mwalimu Nyerere ili kuweza kuigwa kwa yale yanayofaa na kuacha yale yasiyofaa na viongozi

waliopo madarakani au wale wanaotarajia kugombea nafasi mbalimbalii za uongozi wa kisiasa.

Kiutamaduni: Utafiti umeonesha uhusiano uliopo baina ya fasihi na utamaduni. Kandoro anaeleza masula ya malezi kwa vijana, umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi na kuheshimiana baina ya wananchi kuwa ndio muongozo sahihi wa kujiletea maendeleo. Masuala haya yote ni sehemu ya utamaduni wa Mtanzania, ambao unapaswa kuenziwa. Kandoro pia anazungumzia kuhusu kukienzi na kukikuza Kiswahili ambayo ni lugha ya Taifa. Suala hili ni muhimu kwa watunga sera kulichukua na kuhakikisha kwamba sera inayotungwa kuhusu lugha inazingatia hili.

Kinadharia: Utafiti huu utakuwa ni daraja la kuonesha kwamba nadharia za uhakiki ni muhimu katika kufanya uhakiki wa kina kuhusu ushairi wa Kiswahili. Uhakiki unaotumia ama kuongozwa na nadharia huwa madhubuti katika kulieleza lile ulielezalo na kutolea hitimisho muafaka.

Pia utafiti huu unaibua mijadala mbalimbali ambayo itatoa fursa kwa watafiti wengine kufanya utafiti na kuchunguza kwa kina ushairi wa Kandoro. Utafiti watakaofanya utakuza machapisho ya kifasihi hususani ushairi na kisha kuuendeleza badala ya kuudumaza.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kubainisha masuala ya kisiasa yanayojitokeza katika ushairi wa Kandoro. Kandoro anaeleza mambo mengi na yenye manufaa kwa makundi ya watu wa nyanja mbalimbali za maendeleo ya mwanadamu lakini kwa

kuwa hatuna muda wa kutosha kuchunguza masuala yote haya ndio maana tukajikita katika masuala ya kisiasa peke yake. Masuala ya kisiasa katika ushairi wa Kandoro yanayoshughulikiwa katika utafiti huu ni ya kipindi cha ukoloni, wakati wa uhuru na kipindi baada ya uhuru na kuendelea. Siasa katika kipindi cha kabla ya ukoloni hakitazungumziwa kwa sababu Kandoro hakuandika ushairi kuelezea maisha hayo ambayo kwayo alikuwa bado hajazaliwa.

## 1.7 Vikwazo vya Utafiti

Kikwazo kikubwa cha utafiti huu ni lugha ambapo mtafiti si mzungumzaji wa Kiswahili kama lugha ya kwanza. Watanzania wengi ni wazungumzaji hodari wa lugha ya Kiswahili hivyo kuonekana kwamba wanazungumza harakaharaka kuliko mtafiti. Muda mdogo ni kikwazo kingine alichokumbana nacho mtafiti. Muda wa miaka mitatu kwa mtu kufanya utafiti wake na kumaliza hali ya kuwa yeye ni mgeni katika nchi hiyo anayosomea ni muda mfupi mno. Ninasema hivi kwa sababu, mgeni anahitaji kwanza muda wa kutosha ili aweze kuyaelewa mazingira na watu wake halafu ndio akili yake itulie kisaikolojia na kisha aanze masomo.

### 1.7.1 Utatuzi wa Vikwazo

Kuhusiana na kikwazo cha lugha mtafiti alilazimika kumtafuta msaidizi ambaye anafahamu vizuri kuzungumza na kuandika Kiswahili na kisha kuwezesha zoezi la usaili na ukusanyaji wa data kufanyika kwa umakini unaostahili. Kuhusu kikwazo cha muda mtafiti alijitahidi kuchanganyikana na Waswahili katika shughuli zao za kila siku katika masoko, viwanja vya mpira, sherehe mbalimbali za harusi, kiserikali na kidini jambo ambalo lilimsaidia sana kuielewa jamii ya Waswahili kwa uharaka. Hii imemsaidia kuweza kumaliza utafiti wake ndani ya muda uliopangwa.

## 1.8 Mpango wa Tasinifu

Tasinifu hii imeundwa na jumla ya sura sita. Sura ya kwanza inahusu utangulizi na usuli wa tatizo la utafiti. Sura ya pili inapitia kazi tangulizi kuhusiana na ushairi wa Kiswahili hasa ule wa Kandoro. Sura ya tatu ni uhakiki na uteuzi wa nadharia huku sura ya nne ikiwasilisha mbinu za utafiti. Sura ya tano ni uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti. Sura ya sita inatoa hitimishi, matokeo na mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

## 1.9 Muhutasari

Hii ni sura ya kwanza katika utafiti huu. Sura hii imetoa utangulizi ambao umejumuisha mambo ya msingi ambayo kwayo utafiti huu umeonekana kuwa na umuhimu wa kufanyika. Mambo hayo ni pamoja na mada ya utafiti, usuli wa mada, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti na madhumuni mahususi ya utafiti. Vipengele vingine ni maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo na utatuzi wa vikwazo vya utafiti na mwishoni ni mpango wa tasinifu. Sura inayofuata inahusu mapitio ya kazi tangulizi kuhusiana na mada ya utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imefanya mapitio ya kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti. Mapitio ya kazi yaliyofayika ni yale yanayohusu fasihi kwa ujumla na mahususi ushairi wa Kandoro. Mapitio haya yanaonesha kwamba, wanafasihi walioandika juu ya ushairi wa Kandoro wameandika kwa ufupi kwa kuwa hawakuwa na Lengo la kuuchambua ushairi huo kwa undani. Wengi wao wameandika makala fupifupi tu juu ya ushairi wa Kandoro na hakuna hata utafiti mmoja uliofanywa kifasihi kwa ngazi ya Uzamili na Uzamivu kama ilivyofanywa katika utafiti huu.

### 2.2.1 Dhana ya Ushairi

Ushairi ni utanzu ambao una historia ndefu katika fasihi ya Kiswahili. Ingawa mpaka leo hakuna makubaliano kuhusu utungo wa kwanza wa kishairi uliandikwa lini, wataalamu wanakubaliana kuwa utanzu huu una historia ndefu. Wapo wataalamu wanaosema kuwa utungo wa kwanza uliotungwa ni utendi wa *Mwanayanga* unaodaiwa ulitungwa na Fumo Liyongo katika mwaka wa 1517 (Wamitila, 2008).

Nao Warren na Wellek (1985) wanasema kuwa ushairi ni utungo utumiao mfumo maalumu wa maneno katika kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Ujumbe unaweza kuwa wa furaha, huzuni au masimulizi ya hadithi fulani.

Krappert (1974) anauona ushairi kama taaluma iliyokamilika katika kueleza ukweli wa maisha katika jamii husika. Naye Raffel (1984) anashadidia hoja hii kwa kueleza kwamba, kukamilika kwa ushairi hutegemea mbinu anazozitumia mshairi katika

kutunga mashairi yake. Mbinu za utunzi wa mashairi hutofautiana baina ya mwandishi mmoja na mwingine.

Pamoja na maelezo kwamba, ushairi ni taaluma, ushairi ni utungo wa mwanzo kabisa kuliko tungo nyingine zote katika fasihi simulizi, Sanka (1994) anaongeza kwamba, ushairi umekuwa chombo muhimu katika kuhifadhi historia, falsafa na utamaduni wa jamii. Anaendelea kuongeza kuwa, ushairi ni zao la jamii husika na hivyo huwa na sifa maalumu kulingana na muktadha lengwa kwa jamii husika.

Maelezo haya kwa ufupi yanatoa mwanga wa kusukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba, ushairi unaelezwa kama ndio utanzu wa mwanzo kabisa kupata kutungwa na mwanadamu katika historia yake. Hii ni sawa na kusema kwamba, ushairi ndio utungo wa mwanzo kabisa katika kueleza na kuchambua masuala ya kisiasa katika jamii. Uelewa huu kuhusu ushairi unatupatia hamu ya kuutafiti ushairi wa Kandoro ili kubainisha ni masuala gani ya kisiasa anayoyazungumzia.

### 2.2.2 Ushairi wa Kiswahili

Mwanafasihi Oslon (1975) anaeleza kwamba: Ushairi wa Kiswahili ni chombo cha kuhamasisha matarajio na matamanio ya Waswahili na jamii kwa ujumla katika kujiletea maendeleo. Anaongeza kwamba, ushairi wa Kiswahili umechukua nafasi kubwa kama chombo cha mawasiliano baina ya wanajamii. Kwa mfano, kama mshairi haridhiki na namna jambo fulani lilivyo au lifanywavyo, hutunga shairi kuelezea jambo hilo. Hii ndio kusema kuwa, Kandoro alitunga mashairi yake akisawiri masuala mbalimbali ya kisiasa nchini jambo ambalo utafiti umelibainisha kwa undani kabisa.

Nao Mulokozi na Sengo (1995) wanasema kwamba: Ushairi wa Kiswahili ni sehemu ya historia ya Afrika Mashariki kwa msingi kwamba, ulikuwepo tangu enzi za usimulizi na kutolea mfano, tungo za Lyiongo zilizoanza kama masimulizi ya shujaa wa kihistoria na ukatungwa utendi kutokana na masimulizi hayo. Maelezo haya nayo yanasukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba, masuala ya kisiasa yanayoelezwa na Kandoro yana uhistoria ndani yake. Kwa mfano, masuala ya uhuru, ukoloni, Ujamaa na Kujitegemea na kadhalika.

Wamitila (2008) anaeleza kwamba, ushairi wa Kiswahili una makundi mawili. Mashairi ya jadi au mapokeo ambayo yanatungwa kwa kuzingatia arudhi au kaida za utunzi wa mashairi kwa kuzingatia vina, mizani, idadi maalumu ya mishororo katika ubeti, vipande na kadhalika. Pili, kuna mashairi huru ambayo yanakiuka kaida hizo na badala yake kutegemea mbinu nyingine za kishairi kama uruwazaji wa kimuundo katika kuuwasilisha ujumbe wake. Ushairi unaotungwa na Kandoro unafuata urari wa vina na mizani na hivyo kuufanya kuingia katika kundi la wanamapokeo. Mawazo haya ya Wamitila ni muafaka sana katika kusukuma mbele utafiti ambapo kwa kuelewa kwamba, aina ya ushairi uandikwao na Kandoro ni wa kimapokeo imetusaidia kuhusisha vipengele kama vina na mizani na utokezaji wa masuala ya kisiasa katika mashairi yake.

### 2.2.3 Dhana ya Shairi

Shairi ni utungo wa sanaa ya lugha wenye mpangilio maalumu wa mishororo au wa kisauti wenye kutumia mbinu za lugha zenye mnato na mbinu nyinginezo za kibalagha na kimtindo zinazomwezesha mtunzi kuwasilisha ujumbe kwa ufupi na kwa mkokotezo mkubwa unaoeleza kisa, hisia, tukio au hali kwa lugha ya mvuto.

Uzito hasa wa shairi upo kwenye uwezo wake wa kuzigusa hisia na mkuruba au uhusiano wake wa karibu na muziki (Wamitila, 2008).

### 2.2.4 Siasa

Siasa ni sanaa au sayansi ya kutawala na kuongoza nchi kwa kutumia taasisi mbalimbali za serikali katika kuongoza na kutawala. Serikali hudhibiti masuala yake ya ndani na yale ya nje ilikuleta uwiano sahihi utakaofanikisha utawala na uongozi bora kwa maendeleo ya wananchi wake. Hivyo basi, tunaposema: Kutawala na kuongoza tuna maana kwamba, siasa ndio huamua hatima ya nyanja nyingine za maisha. Siasa ya nchi ndio iamuayo ni aina gani ya uchumi iwepo nchini, mfumo na mpango mzima wa masuala ya kijamii uweje na kadhalika. Hivyo basi ni sawa na kusema kwamba, si rahisi kutenganisha siasa na mfumo mzima wa maisha ya jamii. Uelewa huu juu ya siasa ndio uliotuongoza katika ubainishaji wa dhamira za kisiasa katika ushairi wa Kandoro.

### 2.2.5 Sitiari

Sitiari ni uhamishaji wa maana toka kitu au dhana moja hadi kitu au dhana nyingine. Vikoa vya maana vinavyohusika katika uhamishwaji huu huwa vinatofautiana angalau kwa sifa moja ya msingi ya semantiki. Kinachohamishwa ni tabia au umbo au kazi ya kitu kwa kukihusisha na tabia au umbo au kazi ya kitu kingine (Kahigi, 1995).

### 2.2.6 Ishara

Senkoro (1982:36) anasema kwamba: Ishara ni dhana au mawazo mbalimbali yanayotumiwa na washairi na wanafasihi mbalimbali katika kazi zao kuwakilisha

vitu, dhana au mawazo mengine. Katika tasinifu hii tunaongelea juu ya ishara zinazopatikana katika diwani teule na kuonesha, kwa msaada wa nadharia ya Simiotiki zinawakilisha au zinaeleza nini katika muktahda wa kijamii.

#### 2.2.7 Taswira

Taswira ni picha wanayoipata wasomaji wa kazi ya fasihi wasomapo kazi husika, taswira hupatikana kutokana na ishara, sitiari, tashibiha na pengine uhalisiamazingaombwe (Senkoro, 1982). Kwa mfano, usomapo diwani teule unakutana na matumizi mengi ya lugha ya Ishara na Taswira.

### 2.3 Siasa katika Ushairi kwa Ujumla

Ushairi kama tulivyosema ni utanzu mkongwe kuliko tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili ndivyo hivyo hivyo ulivyo mkongwe katika kuelezea masuala ya kisiasa. Wapo wanataaluma kadhaa ambao wamefanya utafiti wa kueleza namna ushairi unavyotumika kama chombo cha kuelezea masuala ya kisiasa katika jamii. Katika sehemu hii tunafaya mapitio ya wataalamu hao ili kuweza kuhusianisha na malengo ya utafiti wetu.

Omary (2011) alifanya utafiti katika ushairi wa Kezilahabi na kueleza kwamba, Kezilahabi ni bingwa wa kueleza masuala ya kisiasa katika mashairi yake yasiyofuata urari wa vina na mizani. Aliyasema haya kwa kuwa alikuwa akijibu hoja ya Folova (2003) kwamba Kezilahabi hazungumzii siasa katika *Karibu Ndani* (1988). Anaendelea kueleza kwamba, matumizi ya lugha ya kisitiari, mafumbo na ishara ndiyo yaliyosheheni katika ushairi wa Kezilahabi na kupitia lugha hiyo ndimo masuala ya kisiasa huelezwa na kufafanuliwa. Mawazo haya ni muhimu na yanatoa

mchango mkubwa katika kusukuma mbele utafiti huu. Kandoro ambaye yeye tofauti na Kezilahabi hutunga mashairi yenye kufuata urari wa vina na mizani pia hutumia lugha ya ishara, mafumbo na sitiari. Mambo haya yamewasilishwa katika sura ya tano ya tasinifu hii.

Naye Omari (2009) katika tasinifu yake ya Uzamivu kuhusu mashairi ya bongo fleva anasema kwamba; mashairi ya bongo fleva huchota dhamira mbalimbali kutoka katika bwawa moja kubwa nalo ni bwawa la siasa. Anaongeza kwamba, hata nyimbo za mapenzi ambazo ndizo zilizotawala katika aina hiyo ya mashairi nazo hueleza masuala ya kisiasa. Mawazo haya tunakubaliana nayo na tunaungana nayo mkono kwa kuwa ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti huu. Kandoro kama ilivyo kwa wasanii wa bongo fleva naye amechota dhamira zake za kisiasa katika bwawa la masuala ya kisiasa kama vile ukoloni, uhuru, ujamaa na baada ya hapo mambo haya yamesawiriwa kwa undani katika sura ya tano ya tasinifu hii.

Nao Msuya na Lupokela (2012) wanaeleza kwamba, ushairi hasa ule wa bongo fleva ni muhimu pia katika kueleza masuala ya kisiasa na malezi katika jamii. Wanaeleza kwamba: Viongozi wengi wa kisiasa wanaahidi mambo ambayo hawayatekelezi jambo ambalo linaonesha kwamba hawana maadili ya uongozi. Wanadondoa sehemu ya shairi lililoimbwa na Prof. Jay katika ubeti ufuatao:

*Cha kwanza nitakachofanya nitafuta umasikini*
*Wanafunzi mkafanyie "pratical" mwezini*
*Kwenye mahospitali nitamwaga dawa*
*kama mchanga*
*na nitafungua akaunti kwa kila mtoto*
*Mchanga …*

*Je! Wananchi mmesikia? (Ndio mzee)*
*Kuwa huyu jamaa hatufai (ndiyo mzee)*
*Hatumtaki aondoke zake (ndiyo mzee)*
*Tuna hakikisha hatumchagui (ndiyo mzee)*
*Kwa sababu huyo jamaa ni mnafiki (ndiyo mzee).*

Hapa Professa Jay anaeleza kwamba, wanasiasa walio wengi hawana maadili mema ya uongozi ndio maana wanawadanganya wananchi kuwa watawafanyia mambo fulani yakuwaletea maendeleo halafu hawawatekelezei. Mawazo haya ni muafaka katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba, hata Kandoro naye anaonesha kupitia ushairi wake namna Mwalimu Nyerere alivyokuwa akiwaahidi wananchi juu ya upatakanaji wa bidhaa mbalimbali kama vile vibiriti na kadhalika. Tofauti na wanasiasa wa leo, Nyerere alikuwa akitekeleza mengi ya mambo aliowaahidi wananchi.

Samwel (2012) anaeleza kwamba, mashairi ya mapenzi ya bongo fleva yanabeba ujumbe pia kuhusiana na masuala ya mapenzi. Anasema hivi kwa sababu baadhi ya wanataaluma, wanajamii, waandishi wa habari na wanaharakati mbalimbali wanadai kwamba, mashairi ya bongo fleva yanazungumzia mapenzi kuliko mambo mengine ya msingi. Kwa maoni yake anauona mtazamo huo ni:

> *Kama hakimu aliyetoa hukumu ya kifungo kwa mshitakiwa bila kumpa nafasi ya kumsikiliza kwa makini. Hii inatokana na ukweli kwamba nyimbo hizo za mapenzi za Bongo fleva, zaidi ya hicho kinachoonekana kuwa ni upotoshaji, zinabeba dhamira muhimu sana ikiwemo siasa* (Samwel, 2012:17).

Dondoo hili linathibitishwa kupitia nyimbo mbalimbali kama vile *Babby Gal* ambapo anadondoa hivi:

*Kila ninachofanya unaona hakifai*
*Baby gal mimi nifanyeje?*
*Nimefanya mambo mengi nikuridhishe weee*
*Lakini gal …. Niweje*
*Nifanye kitu gani uelewe*
*Nifanye jambo gani uridhike*
*Baby gal*

*Ulotamani mwenye simu mkononi*
*Ooh nami nikanunua*
*Ulitamani mwenye dread kichwani*
*Ooh kama nywele nilifuga*
*Kama gari, fedha, nyumba nilikupatia*
*Lakini bado penzi letu liliyumba.*

Wimbo huu unawasawiri wengi wa wanasiasa ambao ndoto zao si kunona majimbo yao yanapata maji, shule na kadhalika, bali ni kuona wanapata nafasi walizozitaka ili waishi maisha bora (Madaso, 2009). Mawazo haya ni muafaka katika kusukuma mbele utafiti wetu wa sasa kwa sababu umeonesha kwamba, wimbo ama shairi linaweza kuandikwa kulenga jambo fulani mfano, mapenzi lakini ndani mwake kukawa na masuala ya kisiasa. Mambo haya pia tumeyaona katika ushairi wa Kandoro pale anapoandika juu ya jambo fulani la kijamii lakini kwa upande wa pili kunatokeza masuala mengine ya kisiasa.

Alhabib (2012) amefanya utafiti kuhusiana na taswira katika nyimbo za taarab. Katika utafiti wake huo amebainisha kwamba, wasanii wa nyimbo za taarab hutumia taswira mbalimbali kuchora na kuwasilisha masuala ya kisiasa katika jamii. Miongoni mwa mambo hayo ni rushwa, unyanyasaji wa kijinsia, ubaguzi, udini, ukabila, njaa, maradhi na ujinga. Kwa maelezo yake, mambo haya ni adui mkubwa wa maendeleo ya jamii na umma kwa ujumla. Tunaungana mkono kwa asilimia mia kwa mia na mawazo ya Alhabib (2012) kuwa, matumizi ya lugha ya taswira

yanasawiri kikwelikweli masuala ya kisiasa katika jamii. Hata hivyo, hakuonesha kwa kina ni masuala gani ya kisiasa yanayosawiriwa kupitia nyimbo za taarab kwa kuwa haikuwa sehemu ya madhumuni ya utafiti wake. Utafiti huu kuhusu ushairi wa Kandoro umeonesha namna matumizi ya lugha ambapo kupitia kipengele cha taswira tumeweza kuonesha namna masuala ya kisiasa yanavyoibuliwa katika ushairi wa Kandoro.

Naye Khalifa (2012) amefanya utafiti kuhusiana na masuala ya kijinsia katika ushairi wa bongo fleva. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba, ushairi wa bongo fleva unamsawiri mwanamke katika mtazamo hasi ukimlinganisha na mwanaume kwa kiasi kikubwa ingawa yapo mashairi machache yanayo msawiri mwanamke katika mtazamo chanya. Kimsingi, tunakubaliana na mawazo ya Khalifa (2012) kwa kuwa ni ya kweli na masuala ya jinsia hayajitokezi katika mashairi ya bongo fleva pekee bali hata katika mashairi ya Kandoro. Katika mashairi yake, Kandoro anaonesha kwamba, wanaume ndio waliotoa mchango mkubwa katika kupigania uhuru wa Tanganyika huku wanawake wakiwa msitari wa nyuma. Jambo hili si la kweli kwani wanawake walikuwa msitari wa mbele kabisa ukilingnisha na wanaume lakini kwa kuwa wanawake wanaonekana kuwa ni dhaifu basi ndio maana wanasawiriwa kama hawakutaoa mchango mkubwa. Maelezo zaidi kuhusiana na jambo hili yameelezwa kwa undani katika sura ya tano ya tasinifu hii.

Naye Ismail (2012) anaeleza kwamba, mashairi hutumika kwa kiasi kikubwa kama chombo cha kuelimisha jamii kuhusiana na haki za binadamu. Anaeleza:

> *Muziki wa Bongo Fleva umekuwa mstari wa mbele katika kutetea haki za binadamu kutokana na madhila yanayomkabili binadamu. Ingawa kwa kiasi kikubwa haibainishi kitu gani kifanyike ili kuondokana na madhila haya lakini ukweli ni kwamba muziki wa Bongo Fleva unaonesha jamii ilivyo na inakoelekea.*

Tunaokubaliana kwa asilimia mia kwa mia na mawazo haya kwa kuwa yanasukuma mbele utafiti wetu. Uimarishaji wa upatikanaji wa haki za binadamu hutegemea kwa kiasi kikubwa utashi wa kisiasa lakini pia juhudi na maarifa ya wananchi wenyewe kupigania haki zao. Kandoro naye hakuwa nyuma katika kuwahamasisha wananchi kupigania haki yao ya kupata uhuru kwa udi na uvumba bila kukata tamaa. Maelezo zaidi kuhusiana na jambo hili yametolewa katika sura ya tano ya tasinifu hii.

Naye Bulaya (2012) anafafanua kwamba, ushairi ni sanaa inayotumika kujadili matatizo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni yanayoikabili jamii. Anathibitisha maelezo yake kwa kutolea mfano mashairi ya *Ndiyo Mzee* na *Siyo Mzee* yaliyoandikwa na Professa Jay. Mawazo haya ni sahihi kabisa na tunaungana nayo mkono kwa asilimia mia kwa mia. Tunasema hivyo kwa sababu ni dhima ya kazi yoyote ile ya fasihi kusawiri hali halisi ya maisha katika jamii. Mawazo haya yanatoa mwanga wa kusukuma mbele utafiti wetu kwa kuwa Kandoro naye ameandika aina ya ushairi wenye kusawiri hali halisi ya maisha ya jamii.

Arinaitwe (2011) alifanya utafiti katika kuchunguza jinsi nyimbo za Wanyakole zinavyosawiri janga la UKIMWI katika jamii ya Wanayankole huko nchini Uganda. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba, nyimbo za Wanyankole zinachukua nafsi kubwa katika kutoa elimu kwa umma juu ya kujikinga na maambukizi ya virusi

vya UKIMWI na vilevile, kuhamasisha wananchi kupima kwa hiyari ili kufahamu mustakabali wa afya zao. Mawazo ya Arinaitwe (2011) ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti huu kwa msingi kwamba, unadokeza kuwa ushairi hutumika kuhamasisha wananchi katika kutekeleza ama kutotekeleza jambo fulani. Utafiti wetu nao hauko mbali na mawazo haya kwani hata Kandoro naye ameandika mashairi mengi ya kuhamasisha jamii ingawa si kuhusiana na janga la UKIMWI. Yeye alitunga mashairi mengi yaliyokuwa na nia ya kuhamasisha jamii kuwa msitari wa mbele katika harakati za kudai uhuru na kupigania haki zao.

Low (2011) naye alifanya utafiti kama uleule wa Arinaitwe (2011) ila yeye alijikita katika muziki wa bongo fleva nchini Tanzania. Pamoja na mambo mengine anaonesha kwamba; suala la unyanyapaa kwa wagonjwa wa UKIMWI bado lipo katika jamii tena kwa kiasi kikubwa. Unyanyapaa huo unaenda sambamba na kuwakatisha tamaa ya kuishi wale ambao tayari wamekwisha pata maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Tofauti na watuzi hawa Kandoro hakuwahi hata mara moja kutunga shairi la kukata tamaa au kuwakatisha tamaa wasomaji wake. Mashairi mengi aliyoyatunga yalilenga kuhamasisha na kuwatia moyo wanajamii kwamba, siku moja watapata uhuru wao na wataishi maisha ya raha mustarehe. Matokeo zaidi kuhusiana na hili yameelezwa katika sura ya tano ya tasinfu hii.

Omari (2008) anaeleza kwamba, ushairi hutungwa kwa kutumia lugha mseto na hasa kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza na hata lugha za makabila. Hali hii huufanya ushairi kuwa ni chombo hai cha kuwasilishia ujumbe kwa jamii husika. Tunasema hivi kwa sababu, maisha ya kila siku katika jamii hufanywa huku watu wakichanganya lugha katika mawasiliano yao ya siku hata siku. Huu ndio uhalisia

wa maisha. Tunakubaliana kwa asilimia mia kwa mia na mawazo haya kwa msingi kwamba, suala la kuchanganya lugha halikuanza leo bali hata katika enzi za akina Kandoro lilikuwepo na hata kabla ya hapo. Katika utafiti huu imeoneshwa namna Kandoro alivyokuwa mtaalamu wa kuchanganya lugha za Kiswahili, Kiingereza na Kiarabu. Hata hivyo, tofauti na watunzi wa siku hizi wa mashairi hasa yale ya Bongo fleva uchanganyaji wa lugha ufanywao na akina Kandoro ni wa hali ya juu sana. Kandoro anachanganya lugha pale panapostahili sio kila mahali tu kama wafanyavyo watuzi wa siku hizi.

Vilevile, kunako miaka ya 1970 kuliibuka mgogoro wa ushairi ambapo kundi la wanapokeo liliwashutumu wanausasa kwamba, wana nia ya kuua ushairi wa Kiswahili kutokana na kuepuka kwao kanuni za utunzi wa ushairi. Wanausasa nao waliwaona wanamapokeo kama watu ambao hawakuutakia mema ushairi wa Kiswahili kwa kuwa walizingatia mambo ambayo yanaufanya ushairi wa Kiswahili kudumaa badala ya kuendeana na mabadiliko ya jamii (Njogu na Chimerah, 1999). Mzozo huo ulianza pale Kezilahabi alipoandika Diwani ya *Kichomi* (1974). Mayoka (1984) akaandika kwamba, Kezilahabi haandiki ushairi bali anaandika kitu kingine kabisa kisichofanana na ushairi. Anaendelea kueleza kwamba ushairi wa Kiswahili ni lazima ufuate urari wa vina na mizani kwa kuwa ndio uti wa mgongoro wa ushairi wa Kiswahili. Mawazo haya hayatofautiani na yale ya Kandoro (1978). Hata hivyo, ilitambulika mapema kwamba, kutatokea mgogoro wa ushairi wa Kiswahili katika kuupinga uandishi wa aina hii ndio maana Topan (1974: xi) anaandika kwamba:

> *Kezilahabi anaufuata mtindo mpya wa kuandika mashairi ya Kiswahili. Na hii ndio njia ya kwanza ya kukuza fasihi ya Kiswahili kwa kuiletea mtindo mpya wa kutunga mashairi.*

Topan anauona utunzi wa Kezilahabi kuwa ni moja ya mambo ambayo yanapaswa kuigwa na kupongezwa na kila anayeitakia mema fasihi ya Kiswahili na maendeleo yake. Mawazo haya yanaonesha kwamba, Topan (1974) anaona kwamba, mabadiliko katika Nyanja za uchumi, siasa, utamaduni, elimu-taaluma na kadhalika hulazimu fani mbalimbali nazo kubadilika ili kuendana na mabadiliko hayo. Hili linathibitika pale anaposema:

> *Ulikuwa wakati hapo zamani ambapo mshairi wa Kiswahili alikuwa mwenyeji wa mwambao na visiwani tu. Hivyo, mashairi ya siku hizo yaliandikwa, kufuatana na mila, desturi na sheria za Kipwani. Mawazo yaliyomo huma pia yalihusu maisha na utamaduni wa Kimwambao.*

Mawazo haya kwa hakika yanasukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba, yanaona mbabadiliko katika jamii ni mambo ambayo husababisha aina mbalimbali za fani ya fasihi nayo kubadilika. Hata hivyo, katika utafiti huu tumebaini kwamba, Kandoro hakukubali katakata kwamba, mabadiliko katika jamii yasababishe kubadilika kwa kanuni na sheria za kutunga mashairi. Maelezo zaidi kuhusiana na hili yamewasilishwa katika sura ya tano ya tasinifu hii.

## 2.4 Siasa katika Ushairi wa Kandoro

Wapo wataalamu kadhaa ambao wameandika na kuutafiti ushairi wa Kandoro wakiuhusianisha na masuala ya kisiasa. Mulokozi (1975) anaeleza kwamba Kandoro ni mwanaharakati mashuhuri ambaye amepigania sana katika kuikuza na kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Haya yanapatikana katika shairi lake; *Kitumike Kiswahili*, ambapo aliitaka serikali ya kikoloni kurasimisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika baraza la Wawakilishi wa Tanganyika. Tunakubaliana na mawazo ya

Mulokozi (1975) na kwamba, mawazo haya yanasukuma mbele utafiti wetu. Tofauti na utafiti wa Mulokozi ambao haukwenda mbali zaidi kueleza juu ya harakati hizo za Kandoro, utafiti huu umekuzwa zaidi na kuonesha pia kwa nini Kandoro alipigania matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Mulokozi (1975) anaendelea kuleza kwamba, Kandoro alikuwa ni mmoja kati ya waanzilishi wa TANU mnamo mwaka 1954. Pamoja na kuwa mwanzilishi wa chama hicho pia aliwahimiza wananchi kujiunga katika chama hiki ili kukifanya kiwe na nguvu ya kutosha ili kumuondoa mkoloni. Anaeleza kwamba, shairi la *Siafu wamekazana* ndio linaloshadidia hoja hii. Bila shaka Mulokozi (1975) anaeleza jambo la msingi ambalo kwalo lilimshughulisha sana Kandoro. Kandoro alipenda kuona wananchi wanaungana na kuwa kitu kimoja katika kupigania haki yao ya kupatiwa uhuru wao. Hata hivyo, Mulokozi (1975) hakueleza kwa undani ni namna gani Kandoro alinadi umoja na mshikamao katika ushairi wake kwa kuwa halikuwa lengo katika utafiti wake.

Naye Maguire (1969) anamtaja Kandoro kama mshairi na pia mwanasiasa. Kandoro alikuwa ndiye mwanzilishi wa jumuia mbalimbali huko Ujiji Tabora. Vile vile, alisafiri sehemu mbalimbali kuhamasisha wananchi kufanya kila linalowezekana kuhakikisha kwamba uhuru unapatikana. Maeneo aliyotembelea kuhamasisha watu ni Mwanza, Musoma na kadhalika. Mawazo haya ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu. Ni kweli Kandoro ni mshairi na pia mwanasiasa. Ameandika mashairi mengi kuzungumzia siasa na pia ametumia muda wake mwingi kufanya masuala ya kisiasa. Tofauti na utafiti wa Maguire (1969) ambao haukulenga kuonesha namna masuala ya kisiasa, yanavyojitokeza katika ushairi wa Kandoro, utafiti wetu

umezama kwa kina katika kuwasilisha masuala ya kisiasa kama yanavyojibainisha katika ushairi wa Kandoro.

Kezilahabai (1977) anamueleza Kandoro kama mshairi wa hali ya juu sana katika utunzi wa mashairi yahusianayo na ukombozi wa kisiasa. Mashairi yake yanaonya na kuhamasisha harakati za kisiasa na maendeleo kwa wananchi. Anashadidia mawazo yake kwa kutolea mfano mashairi ya Kandoro, *Kwetu ni Kwao kwa Nini?* na *Shujaa Haogopi Kitu Kilicho Halali Yake.* Dhamira za kisiasa zitokeazo katika beti za mashairi haya ni nzito na muafaka katika kuhamasisha harakati za kisiasa na ukombozi wa nchi kutoka mikononi mwa wakoloni. Mawazo haya ya Kezilahabi (1977) yametoa mwanga wa kusukuma mbele utafiti wetu, kwa msingi kwamba, mashairi ya Kandoro aliyoyataja yana nafasi kubwa katika kuupambanua ushairi wa Kandoro. Nasi pia tumeliona hili na kisha kuyachambua mashairi haya kwa kina na kuonesha ni namna gani yanawasilisha masuala ya kisiasa.

Naye Alli (1978) anamtaja Kandoro kama mhamasishaji na muumini mkubwa wa Ujamaa na Kujitegemea. Anaendelea kueleza kwamba, Kandoro alituonya kupitia diwani yake iliyojulikana kwa jina la *Liwazo la Ujamaa* mara tu baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha. Anaongeza kwamba, katika diwani hii Kandoro ameandika mashairi mengi yenye kuonesha faida za Ujamaa na kuhamasisha wananchi kulikubali na kulipokea kwa mikono miwili Azimio la Arusha. Mambo haya nasi pia tumeyashuhudia katika utafiti huu ambapo tumeona uwezo mkubwa alionao Kandoro katika kuihamasisha jamii kuunga mkono siasa za ujamaa na kujitegemea. Jambo la msingi ambalo Kandoro analisisitiza ni kwamba, Ujamaa ni njia kuu ya kuondoa unyonyaji na dhuluma katika jamii. Jamii ya Kijamaa huwaona

watu wote kuwa ni sawa na hivyo kila mtu ana haki ya kufaidi rasilimali za taifa lake. Mawazo zaidi kuhususiana na suala hili yamewasilishwa katika sura ya tano ya tasinifu hii.

Naye Kiwanuka (1978) kwa upande wake anaeleza kwamba, Kandoro alikuwa ni askari aliyemsitari wa mbele katika uwanja wa vita ambaye hakuchoka kamwe kupigania kuanzishwa kwa jamii ya kijamaa nchini. Mawazo haya ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti huu uliolenga kubainisha masuala ya kisiasa katika ushairi wa Kandoro. Ingawa Kiwanuka (1978) hakuwa na lengo la kuuchambua ushairi wa Kandoro kwa mtazamo wa kisiasa kwa maana ya ni masuala gani ya kisiasa yajitokezayo katika mashairi hayo bado kwa kusema kwamba Ujamaa ni lazima uanzishwe amegusa masuala mengi ya kisiasa ambayo kwayo tumepata mwanga wa namna ya kuyaibua zaidi na zaidi.

Naye Kitogo (2002) anaeleza kwamba, miongoni mwa washairi wakubwa waliopata kuelezea maendeleo ya siasa nchini, Kandoro ni baba yao. Anasema kwamba, Kandoro ameeleza maendeleo ya siasa katika kipindi cha ukoloni, wakati wa uhuru na baada ya hapo. Tunakubaliana na mawazo ya Kitogo (ameshatajwa) kwa asilimia mia kwa mia. Mawazo haya yametusukuma mbele katika kuchunguza ni kwa vipi Kandoro amesawiri maendeleo ya siasa nchini kwa mtazamo wa kifasihi tofauti na Kitogo aliyetazama masuala ya kisiasa kwa mtazamo wa Taaluma za Maendeleo. Kupita mtazamo wa kifasihi tumeweza pia kuainisha mbinu mbalimbali za kisanaa zilizotumiwa na Kandoro katika kuwasilisha ujumbe wa kisiasa kwa jamii.

## 2.5 Historia Fupi ya Kandoro

Kama inavyonukuliwa kutoka kwa Kitogo (2002), Kandoro alizaliwa tarehe 8, mwezi Disemba, 1926 katika mtaa wa Kasingirima, Ujiji mkoani Kigoma. Alipata elimu katika shule za Ujiji shule ya msingi, Mwanahala ya Iringa na kisha akajiunga na chuo cha Ualimu Bwiru kilichoko Mwanza. Baada ya hapo aliajiriwa serikalini na kutumikia nafasi mbalimbali.

Kandoro alioa wanawake watano kwa nyakati tofautitofauti na alikuwa na jumla ya watoto nane. Wakati mauti yanamkuta mwaka 2001 alikuwa na jumla ya wajukuu saba. Katika maisha yake ya kazi amepata kuajiriwa na serikali kwa miaka kadhaa na baadaye akaamua kujiajiri yeye mwenyewe. Alikuwa mwanaharakati wa kisiasa kuanzia mwaka 1940 ambapo alishiriki kikamilifu katika kupigania uhuru. Kwa utashi wake mwenyewe mwaka 1946 Kandoro aliamua kuacha kazi serikalini na kuamua kuwa mkulima, mfanyabiashia na mwanasiasa.

Kimsingi, kwa kipindi ambapo Kandoro hakuwa mwajiriwa tena, alikitumia vizuri kipindi hicho katika kufuatilia masuala ya kisiasa. Kwa mfano, Mwaka 1945 akishirikiana na Bhoke Munanka, Mullas na Mahamud Kitege alianzisha jumuiya iliyoitwa “African Right Ways Association”. Jumuiya hii ilifanya kazi kubwa ya kufanya uhamasishaji wa wananchi kuungana pamoja katika kupambana na mkoloni ili atoe uhuru kwa wananchi waweze kujitawala wenyewe. Kutokana na uimara wa jumuiya hii katika uhamasishaji Kandoro alipewa karantini ya kuondoka mjini Mwanza mara moja na serikali ya Kikoloni vinginevyo atatiwa gerezani. Agizo la kumtaka Kandoro aondoke mjini Mwanza lilisomeka hivi:

*Name: Saadan Abdul Kandoro*
*Tribe: Manyema*
*Chief: Headman …… District Kigoma*

*Whereas I have reasonable cause to believe that the presence of ……. SAADAN ABDUL KANDORO in the Towship of Mwanza is undesirable in the public interest, I herebly require him:*

*To leave the township not later than 1st June 1955*

*(a) To proceed to Kigoma outside the township of Mwanza until further notice.*

*Date 15th June 1955* *Sgd ………………………………………….*

*District Commisionor*

*Mwanza.*

Hata hivyo, Oscar Kambona ambaye baadaye alikuwa Katibu Mkuu wa TANU na Waziri katika serikali ya awamu ya kwanza na ya pili alifanya jitihada za dhati kabisa katika kuhakikisha kwamba, Kandoro anarejeshewa haki yake ya kuishi mjini Mwanza ili aendeleze mashambulizi dhidi ya wakoloni. Baada ya muda mfupi, Kandoro alirejeshewa haki ya kuishi Mwanza na akaendelea na Uanaharakati wa kupigania uhuru.

Vilevile, itakumbukwa kwamba: Mwaka 1952 Kandoro alikuwa Katibu wa jimbo la Kanda ya Ziwa wa Tanganyika African Association (TAA). Mwaka 1954 alikuwa miongoni mwa watu 17 walioanzisha chama Kitukufu cha TANU mjini Dar es Salaaam. Aliendelea akawa Katibu wa TANU Dodoma na Tabora na baadaye akafanywa katibu tawala katika makao makuu ya chama.

Mwaka 1962 aliteuliwa kuwa katibu wa TANU wa wilaya na Kamishna wa wilaya ya Mafia, na 1964 alikuwa Katibu wa TANU na Kamishna wilaya ya Bagamoyo. Alikuwa Mwenyekiti wa kwanza mchaguliwa wa Halmashauri ya Tume ya mwendo mwema TANU, Mwanachama na Mwanzilishi katika jumla ya waanzilishi wa C.C.M. na Mkuu wa Nyumba kumi, Visiga, Kibaha, Mkoani Pwani na kadhalika Magomeni Dar es Salaam. Pia alichaguliwa Uanakamati ya utedaji wa Wilaya ya C.C.M Kibaha na U-mwana Kamati ya Utendaji mkoa wa Pwani na Mwana Halmashauri Kuu wa Chama cha Usanifu wa Lugha ya Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA). Bwana Kandoro alijifunza mashairi alipokuwa mwanachuoni na amekuwa mwandishi wa mashairi toka hapo mashairi yake yametokea katika magazeti mengi kama vile *Mambo Leo* na alipambana kwa maandishi na mabingwa wa mashairi kama vile akina Marehemu Mdanzi Hanasa, Mathias Mnyampala, Shaaban Robert, Salehe Kibwana, Mzee Waziri Kijana na wengineo wengi ambao pia walikuwa marafiki zake. Aidha Bwana Kandoro ameandikiana mashairi kadhaa na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na moja ya mashairi hayo limo katika Kitabu kilichotungwa na Bwana Kandoro, *Mashairi ya Saadani*. Mwaka 1969 aliteuliwa na Chama cha Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania kuwa mmoja wa waamuzi katika mashindano ya ushairi ya Azimio la Arusha. Bwana Kandoro ametunga vitabu vifuatavyo:

1. *Mwito wa Uhuru*.
2. *Mashari ya Saadani*.
3. *Ushahidi wa Mashairi ya Kiswahili*.
4. *Liwazo la Ujamaa*.
5. *Fasihi sahihi*.

Hii ndio historia ya Saadan Kandoro kwa ufupi.

## 2.7 Muhutasari

Katika sura hii mambo yafuatayo yamewasilishwa kwa mawanda yake. Mambo hayo ni dhana ya ushairi, ushairi wa Kiswahili, dhana ya shairi, siasa, sitiari, ishara na taswira. Mambo mengine ni siasa katika ushairi kwa ujumla, siasa katika ushari wa Kandoro na historia fupi ya maisha ya Kandoro. Katika mapitio yote yaliyopitiwa katika kazi tangulizi zilizopo katika sura hii hakuna hata mtaalamu mmoja aliyefanya utafiti wa kina wa kifasihi katika kuutafiti ushairi wa kandoro. Hali hii imefanya kuwepo kwa pengo la utafiti ambalo limehitajia kujibiwa na utafiti huu umefanya kwa minajili ya kuziba pengo hilo. Sura inayofuata inaeleza juu ya nadharia za uhakiki wa fasihi zilizoteuliwa kutumika katika utafiti huu.

# SURA YA TATU

# NADHARIA ZA UHAKIKI WA FASIHI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inapitia nadharia kadhaa ambazo kwanzo zimetumika katika kuuhakiki ushairi wa Kandoro. Ni vema ikaeleweka wazi kwamba, uhakiki ama utafiti wowote ule wa kifasihi ni lazima uongozwe na nadharia muafaka ili uweze kutoa majibu yanayokidhi malengo ya utafiti kama yalivyoorodheshwa na mtafiti. Nadharia ndiyo itoayo mwelekeo wa utafiti; njia, mbinu, upitiaji wa kazi tangulizi na uchambuzi na uwasilishaji wa data za utafiti wote hufanywa kwa kuongozwa na nadharia zilizoteuliwa na mtafiti. Kwa msingi huu utafiti huu umeongozwa na nadharia za Simiotiki, Umarx na Ufeminist. Maelezo ya kina kwa kila nadharia yanatolewa hapa chini kama ifuatavyo:

## 3.2 Nadharia ya Simiotiki

Simiotiki ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo linatumiwa kuelezea mielekeo na makundi fulani ya kihakiki. Makundi hayo na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kuihakiki kazi za kifasihi ambao unaangaza ishara za kifasihi katika kazi hizo. Nadharia hii kwa ujumla inajishughulisha na ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi (Wamitila, 2002:132).

Ishara zinazojitokeza katika kazi za fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadha wa jamii wa kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Chandler (1992) anaeleza kwamba, binadamu ni mtengenezaji na mnyambulishaji wa alama hizo. Wasomaji na watazamaji wa kazi za fasihi hutengeneza maana mbalimbali kupitia ubunifu na tafsiri zao juu ya alama hizo. Mawazo haya yanakamilishwa na yale ya

Chandler (1992) aliposema kuwa, tunafikiri kwa kutumia alama. Alama hizo zinakuwa katika mfumo wa maneno, picha, sauti, harufu, ladha, matendo na mtenda au yambwa. Anaendelea kueleza kwamba, kitu chochote kitakuwa alama kama watu watakifasiri kama kirejelee, yaani kinasimama kwa niaba ya kitu kingine badala ya chenyewe.

Wamitila (2002) anaeleza kwamba, katika lugha kuna vitu viwili ambavyo ni kitaja (a signifier), yaani umbo ambalo alama inachukua na kirejelee (a signified), yaani maana iwakilishwayo na alama hiyo. Kutokana na maelezo haya tunapata uelewa kuwa, kuna kitaja, na kirejelee ambapo mahusiano ya viwili hivyo ni ya kubuni tu, hutegemea utamaduni wa jamii husika. Inawezekana kabisa ikawa hakuna uhusiano kati ya kitaja na kirejelee, lakini kama wanajamii wamekubaliana juu ya matumizi yake basi hutumika na huelewana miongoni mwao. Bathes (1994) akaja na aina tano za misimbo zinazotumika katika kazi za fasihi ambazo kwa pamoja huunda nadharia ya Simiotiki. Aina hizo ni msimbo wa Kimatukio, Kihemenitiki, Kiseme, Kiishara na Kiurejelezi.

Kandoro kama ilivyo kwa baadhi ya washairi wengine anatunga mashairi yake kwa kutumia lugha ya picha, ishara, mafumbo, sitiari, na taswira kali haswahaswa. Nadharia ya Simiotiki imetoa mwongozo muafaka katika kuzichambua aina zote hizo za matumizi ya lugha na kisha kuwezesha kufanikisha madhumuni ya utafiti huu. Nadharia nyingine ni ile ya Umarx, nayo inaelezwa kama ifuatavyo:

### 3.3 Nadharia ya Umarx

Msingi mkubwa wa nadharia hii unatokana na mawazo ya Karl Marx na Fredrich Engels. Karl Marx (1818-1863) anahusisha U-Marx na Nyanja kama vile uchumi, historia ya jamii na mapinduzi (Wamitila, 2002:182). Kimsingi, mawazo ya Marx yanalenga katika kuwataka wanafasihi kuzitazama hali za jamii zao zilivyo na kuzitafutia ufumbuzi kwa maana ya kuzibadilisha kuliko kuzitafsiri tu.

Mawazo ya Karl Marx kuhusu historia na miundo ya kijamii yana nafasi kubwa katika nadharia hii. Umarx ni falsafa ya Kiyakinifu hasa kwa kuwa pana msisitizo mkubwa kwenye msingi wa hali za kiyakinifu za maisha kama mazingira ya kuishi kuliko mawazo katika maisha ya binadamu. Umarx hautegemezi mfumo wake wa kifalsafa kwenye dhana dhahania kama urembo, ukweli au ndoto bali kwenye uhalisi unaonekana (Wamitila, 2002:182). Mfumo wa maisha tulio nao leo ni ule ulioongeza tofauti kati ya walionacho na wasio nacho (utabaka) na kusababisha kuwapo kwa mgogoro wa kitabaka katika jamii za Watanzania na Waafrika kwa ujumla. Kupitia migogoro ya kijamii ndipo masuala mbalimbali ya kisiasa yanapojitokeza na kuwasilishwa kwa jamii kwa njia mbalimbali kama vile kupitia mashairi ya Saadan Kandoro. Kimsingi, nadharia ya Umarx ndiyo mahala pake katika kufanikisha uchambuzi wa matabaka ambayo ndani yake kuna masuala ya umasikini, ujinga na maradhi. Wamitila (2002:183) anaeleza kwamba:

> *Wahakiki wa Ki-Marx wanaamini kuwa daima historia ya binadamu itadhihirisha au kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka ya kiuchumi – jamii. Itakumbukwa kuwa Karl Marx alisema kuwa historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka …. Kitu cha msingi katika maisha ya binadamu ni kula na kunywa, kupata malazi na mavazi na mambo mengine.*

Mambo haya ndiyo humfanya binadamu kupambana ili aweze kuyapata na kisha aweze kuishi maisha mazuri. Wakoloni kwa hakika hawakutoa fursa kwa wananchi kuwa na maisha mazuri kwa kuwa daima wakoloni waliwatumikisha kwa kazi nyingi zenye malipo kidogo. Hali hii iliwafanya wananchi kufanya kila linalowezekana ili waipate haki yao ya uhuru na kisha kupanga mipango yao ya maendeleo itakayowaletea maendeleo. Usomapo ushairi wa Kandoro utabaini kwamba, uwanaharakati wa kitabaka ndio unaotawala katika mashairi hayo. Hivyo basi, nadharia ya Umarx imeongoza vema uchambuzi na uhakiki wa mashairi ya Kandoro kama inavyoonekana katika sura ya tano ya tasinifu hii.

## 3.4 Nadharia ya Ufeministi

Nadharia hii iliibuka kutokana na kazi zilizoasisiwa na Jacques Lacaun. Nadharia hii kimsingi inasaidia kuhakiki matini katika misingi ya kiuchanganuzi nafsia ambao hutazama zaidi tabia na mwenendo wa mwanadamu katika maisha yake ya kila siku. Vile vile, nadharia hii huzingatia kuweko kwa nafsi bandia au nafsi isiyo halisi iliyojengwa kutokana na mielekeo ya kiuana, utaratibu fiche wa kisaikolojia pamoja na taasubi za kiume. Katika utaratibu fiche maumbo halisi ya kiisimu katika akili ya mwanamke hughubikwa na badala yake mambo ya kidhahania huimarishwa. Maumbo haya yasiyo na uhusiano wowote na uhalisia wake kama binadamu ndiyo yanayobainika hususani kupitia lugha na tabia yake. Utaratibu huu ambao ni wa kiishara ndio unaoashiria tofauti za kiuana zinazopatikana katika utamaduni wa jamii.

Kwa mujibu wa mtazamo huu, nafasi ya mwanamke imefungamana na lugha inayomzungumzia, lugha inayoashiria uana wake. Nafasi hii hufinyangwa na jamii

kupitia asasi mbalimbali ili aweze kukubalika katika utaratibu huo wa kiishara. Uchanganuzi nafsia katika mtazamo wa kike, ni nadharia ya uumbaji wa nafsi katika misingi ya Uana. Nadharia hii imeteuliwa kwa mantiki kwamba Kandoro katika baadhi ya mashairi yake ameeleza masuala ya kijinsia. Hivyo, nadharia hii imetoa mwanga wa namna ya kuyachambua na kuyahakiki masuala ya kijinsia na kuyahusisha na masuala ya kisiasa katika ushairi huo wa Kandoro. Masuala hayo yamewasilishwa katika sura ya tano ya tasinifu hii.

## 3.5 Muhtasari

Sura hii imewasilisha nadharia tatu zilizoongoza utafiti huu. Nadharia hizo ni Simiotiki, Umarx na Ufeministi. Kila nadharia imetoa mchango maridhawa katika kuhakiki ushairi wa Kandoro. Nadharia ya Simiotiki imesaidia katika kuainisha picha, ishara, taswira na sitiari mbalimbali katika mashairi ya Kandoro. Nadharia ya Umarx imesaidia katika kubainisha matabaka, unyonyaji, rushwa na ufisadi katika ushairi huo. Nadharia ya Ufeministi kwa upande wake imewezesha kuchambua masuala ya kijinsia kama yanayojitokeza katika ushairi wa Kandoro. Nadharia hizi kwa pamoja zimewezesha kukamilisha hatua zote za uchambuzi na uwasilishaji wa data. Sura inayofuata inaeleza juu ya mbinu na njia za utafiti.

# SURA YA NNE

# MBINU ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha mbinu mbalimbali zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu. Mbinu hizo ni pamoja na usanifu wa utafiti, populesheni, sampuli, usampulishaji, mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data. Tunaanza na usanifu wa utafiti.

## 4.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mpangilio maalumu unaoonesha namna na jinsi utafiti utakavyofanyika ili kuwezesha kujibu maswali ya utafiti husika (Kothari, 2008). Utafiti huu umetumia mbinu ya usanifu ijulikanayo kama uchunguzi kifani katika kukusnaya data. Yin (1994) anasema kwamba, uchunguzi kifani ni aina ya usanifu ambayo mtafiti huteua sehemu au jambo au kitu maalumu ambacho atakifanyia utafiti kati ya vingi vilivyopo ili aweze kukidhi mahitaji ya utafiti wake. Katika utafiti huu, ushairi wa Kandoro ndio ulioteuliwa na kufanyiwa utafiti katika kipengele cha masuala ya kisiasa peke yake. Mbinu hii ya usanifu ni muafaka katika utafiti huu kwa sababu inatoa fursa kwa mtafiti kulitafiti jambo moja kwa muda wa kutosha na hivyo kupata majibu sahihi ya maswali ya utafiti wake (Robson 2007). Vilevile, mbinu hii humuwezesha mtafiti kuzama na kulitafiti jambo moja kwa undani kabisa na kisha kulitolea mahitimishi stahiki (Cresswel, 2009). Isack na Michael (1981) wanasema kwamba, uchunguzi kifani ni mbinu ambayo humwezesha mtafiti kuufanya utafiti wake kwa gharama nafuu. Kwa kutumia mbinu hii kutafiti ameweza kutalii mashairi ya Kandoro katika vitabu vyake mbalimbali kama vile

*Liwazo la Ujamaa*, *Mashari ya Saadan*, *Fasihi Sahihi* na yale yaliyotoka katika magazeti ya *Mamboleo* na *Baragumu*.

## 4.3 Watafitiwa

Watafitiwa hurejelea idadi ya watu, makundi ya watu au vitu vyote ambayo mtafiti amevitumia ama anaweza kuvitumia ili kukamilisha utafiti wake. Kwa upande mwingine watafitiwa huweza kutafsiriwa kama mkusanyiko wa watu au vitu katika hali na mazingira tofautitofauti. Watafitiwa katika utafiti huu ni mshairi Kandoro na kazi zake za ushairi alizopata kuandika. Kazi hizo ni *mashairi ya Saadan*, *Liwazo la Ujamaa*, *Wito wa uhuru*, na *Fasihi Sahihi* na mashairi yaliyotoka katika magazeti ya *Mamboleo* na *Baragumu*.

## 4.4 Usampulishaji wa Watafitiwa

Sampuli ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa katika kundi kubwa na kuwa ndio wakilishi wa kundi hilo lote (Keys, 1980). Sampuli Lengwa na Nasibu ndizo zilizotumika katika kufanikisha ukusanyaji wa data. Sampuli Lengwa ni aina ya sampuli ambayo mtafiti huiteua akiwa na imani kwamba, itampatia data itakayowezesha kukamilisha malengo ya utafiti wake (New man, 2006:22). Kwa msingi huu basi, sampuli lengwa hapa ni kazi za Kandoro za ushairi ambazo tumekwisha zitaja hapo awali. Mtafiti ameteua kazi hizi kwa kuwa anaamini kwamba, zitampatia majibu ya maswali yake ya utafiti. Vilevile, sampuli nasibu nayo imetumika katika utafiti huu. Sampuli nasibu ni ile ambayo hutoa fursa sawa kwa watafitiwa wote kuchaguliwa ili kutoa data za utafiti kama ilivyokusudiwa na mtafiti (Babbie, 1999). Sampuli nasibu imetumika katika kukusanya data kutoka katika mashari yaliyo husika. Pale mtafiti alipobaini ubeti, msitari au kipande cha

msitari wa shairi fulani kuwa kinaibua masuala ya kisiasa alikinukuu katika shajara kwa ajili ya uchambuzi. Hivyo basi, sampuli Lengwa na nasibu zimesaidia kukusanya taarifa muhimu zilizowezesha kutimiza malengo ya utafiti wetu.

## 4.5 Vyanzo vya Data

Kuna aina mbili za vyanzo vya data za utafiti katika utafiti wowote ule wa kitaaluma. Vyanzo hivyo ni vile vya data za msingi na upili. Tuanze na data za msingi.

### 4.5.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine kwa minajili ya utafiti kama huo anaoufanya sasa (Kothari, 1992:95). Hivyo basi, data za msingi katika utafiti huu zimekusanywa katika maandishi ya ushairi ya Kandoro katika vitabu vyake na yale yaliyotokea katika magazeti ya *Mambo Leo* na *Baragumu*. Data za msingi kwa jina lingine hujulikana kama data ghafi yaani mpya. Data hizi ghafi zimewezesha kujibu maswali ya utafiti wetu kama yanavyoonekana katika sura ya tano ya tasinifu hii.

### 4.5.2 Data za Upili

Tofauti na data za msingi, data za upili ni zile ambazo tayari zimekwisha kukusanywa na watafiti wengine na kuchapishwa katika ripoti, makala, tasinifu, magazeti na vitabu mbalimbali. Hii ni mbinu ya kukusanyia data mezani, yaani mtafiti haendi uwandani kuhoji au kufanya mahojiano na watafitiwa. Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa katika maktaba kuu ya Taifa, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili na

Taasisi ya Taaluma za Maendeleo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Data za Upili hutumika kujazilizia data za msingi ili kuwezesha kujibu maswali ya utafiti wetu.

## 4.6 Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data ni kitendo cha kukusanya data kutoka kwa watafitiwa ili kujibu maswali ya utafiti. Ukusanyaji wa data za kitaalimu hufanywa kwa kuongozwa na mbinu mbalimbali. Mbinu hizo katika utafiti huu ni kama ifuatavyo:

### 4.6.1 Uchambuzi wa Kimaudhui

Uchambuzi wa Kimaudhui ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo humpatia mtafiti data baada ya yeye ama msaidizi wake kusoma matini iliyoteuliwa kwa kina. Kutokana na kusoma huko ndipo pale akutanapo na sehemu inayohusiana na malengo yake ya utafiti na kuinukuu katika shajara maalumu (Kothari, 2008).

Mbinu hii imetumika katika kukusanya data za msingi na vilevile data za upili. Katika ukusanyaji wa data za msingi mtafiti na msaidizi wake waliandaa shajara ambalo lilikuwa na vichwa/mada zinazohusiana na malengo ya utafiti ama kile kilichokusudiwa kukusanywa. Baada ya hapo walianza kusoma kazi za Kandoro kama zilivyokwisha ainishwa hapo juu na kila walipokutana na shairi, ubeti wa shari ama mshororo au kipande cha mshororo kinachohusiana na mada zilizoainishwa kilinukuliwa katika shajara hilo. Kazi hii ya usomaji na unukuu iliendelea kwa kazi zote za Kandoro mpaka pale data iliyohitajika ilipopatikana na kisha kuwezesha uchambuzi wa data kama unavyoonekana katika sura ya tano ya tasinifu.

### 4.6.2 Mbinu ya Usaili

Usaili ni mbinu ya kukusanya data kwa njia ya mazungumo ya ana kwa ana baina ya mtafiti na mtafitiwa (Babbie, 1999). Kupitia mbinu hii tumeweza kukusanya data kutoka kwa ndugu mmoja wa karibu na Kandoro ambaye ametupatia data zilizowezesha kujibu maswali ya utafiti kama inavyoonekana katika sura ya nne ya tasinifu hii.

## 4.7 Uchambuzi wa Data

Data zilizokusanywa haziwezi kuwa na maana yoyote mpaka zitakapochambuliwa na kuwasilishwa katika tasinifu. Vilevile, data hizo hazichambuliwi kienyeji kienyeji tu bali pia kuna mbinu muafaka ambazo zinapaswa kufuatwa kadiri zitakavyokuwa zimeteuliwa. Mbinu iliyotumika katika kuchambua data za utafiti huu ni ile ya uchambuzi wa kimaelezo. John (1997) anaeleza kwamba, uchambuzi wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambayo humruhusu mtafiti kusikiliza au kusoma shairi, kisha kuelewa maudhui, falsafa, mtazamo wake na kadhalika. Mbinu hii pia huhusisha uchambuzi wa lugha iliyotumika. Kwa kufanya hivyo, mbinu hii huruhusu utolewaji wa maelezo ya kina juu ya data zilizokusanywa na mtafiti kwa namna ambayo itawezesha kujibu maswali ya utafiti husika.

Uchambuzi wa data umefanywa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Lengo la kwanza lilihusu ubainishaji wa masuala ya kisiasa katika ushairi wa Kandoro. Katika kuchambua na kuwasilisha data za Lengo hili mtafiti amebuni mada kuu na ndogo ndogo ambazo zote kwa pamoja zimeshehenezwa maelezo ya kina yenye kujibu lengo hilo la utafiti. Lengo la pili lilihusu mbinu za kisanaa ambazo zimetumiwa na Kandoro katika kuwasilisha masuala ya Kisiasa katika ushairi wake. Hapa pia

ziliandaliwa mada kuu na ndogo ndogo ambazo kwanzo zimewezesha kukamilika kwa lengo hili la utafiti. Lengo la tatu lilihusu ufafanuzi wa falsafa ya Kandoro ambayo nayo imechambuliwa na kuwasilishwa katika sura ya tano ya tasinifu hii.

## 4.8 Mkabala wa Kidhamira

Kazi ya fasihi ina sifa ya kuchambuliwa kwa kutumia mikabala mbalimbali ya kifasihi kulingana na lengo la mhakiki. Mkabala wa Kidhamira ni mojawapo ya mikabala maarufu katika uhakiki wa kazi za kifasihi. Maelezo haya yanathibitishwa na Taylor na Broad (1984), Benner (1985) na Leininger (1985) kama wanavyonukuliwa na Aronson (1992). Aronson (1992) anaeleza kwamba, mkabala wa kidhamira hutumika kuichambua kazi ya fasihi kwa kuzingatia hatua kuu nne. Hatua ya kwanza ni ya kukusanya data, hatua ya pili ni kuoanisha mada na data husika (kubainisha data zinazohusaina na mada ya utafiti). Hatua ya tatu ni kupangilia data kwa namna ya kuoanisha dhamira kuu na dongondogo. Hatua ya nne ni kuandaa hoja au nyanja zitakazozingatiwa katika uchambuzi wa dhamira baada ya kusoma ama kupitia machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti husika.

Mkabala huu umetoa manufaa makubwa katika utafiti huu, ambapo vipengele vyote vinne vimetumika na kuwezesha kupata uchambuzi makini wa data za utafiti ambapo hii ni hatua ya kwanza. Hatua ya pili ilikuwa ni kubainisha masuala ya kisiasa katika kazi za Kandoro. Baada ya hapo tulizipanga data kulingana na malengo ya utafiti ili kurahisisha uchambuzi. Hatua ya mwisho ilihusisha ujengaji na utetezi wa hoja pamoja na uchambuzi wake uliofanywa katika sura ya tano ya tasinfu hii.

## 4.9 Uhalali, Kuaminika na Maadili ya Utafiti

Uhalali wa mbinu za kukusanyia data ni utaratibu unaowezesha kupatikana kwa data sahihi na za kuaminika (Cohen, na wenzake, 2000). Usahihi wa data katika utafiti huu umedhibitiwa kwa mbinu mbili za ukusanyaji wa data ambazo ni uchambuzi wa kimaudhui na usaili. Mbinu zote hizi zimekuwa zikitoa data ambazo zinafaa kuhusiana na masuala ya kisiasa katika ushairi wa Kandoro. Katika uchambuzi wa data, mkabala wa kidhamira na mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo ndizo zilizotumika katika kukusanyia data, Usahihi wa mbinu hizi unatokana na ukweli kwamba mapungufu ya kila moja hukamilishwa na ubora wa mbinu nyingine.

Vilevile, usahihi wa mbinu na nadharia za uhakiki wa fasihi zilizotumika katika utafiti huu zilijadiliwa katika mjadala baina ya mtafiti na msimamizi wake na wanataalimu wa fasihi katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

### 4.9.2 Kuaminika kwa Data

Kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa/kuzalisha matokeo yaleyale pale utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zile zile (Kothari, 2008). Kuaminika kwa data hujitokeza pale ambapo kuna kuwa na uhusiano ama ulingano katika taarifa zilizotolewa na watu walewale kwa muda tofauti (Furlong na Lovelace, 2000). Katika utafiti huu, kuaminika kwa data kumehakikiwa kwa kutumia mbinu mbili za kukusanyia data na nadharia tatu za uhakiki wa kifasihi zilizotoa jibu moja.

## 4.10 Maadili

Miongoni mwa vitu muhimu anavyotakiwa kuzingatia mtafiti ni maadili ya utafiti yanayohusu kupata kibali cha kufanya utafiti pamoja na kutunza siri za watafitiwa. Hivyo basi, katika utafiti huu, maadili ya utafiti yalizingatiwa kabla na baada ya kukusanya data. Kwa kuwa utafiti wetu ulikuwa ni wa uwandani, na maktabani tumehakikisha kuwa dondoo kutoka katika kazi za Kandoro zimedondolewa kwa usahihi na kufanyiwa uchambuzi wa kifasihi kwa kuongozwa na nadharia tatu za uhakiki wa kifasihi tulizoziteua.

## 4.11 Muhutasari

Katika sura hii tumeeleza mbinu mbalimbali zilizomwongoza mtafiti katika ukusanyaji wa data na kisha uchambuzi wake. Mambo yaliyowasilishwa ni pamajo na usanifu wa utafiti, watafitiwa, usampulishaji pamoja na vyanzo vya data: data za msingi na upili. Mbinu nyingine ni ukusanyaji wa data uliohusisha mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui na usaili. Pia tumeeleza mbinu za uchambuzi wa data, mkabala wa kiuhakiki, uhalali, kuaminika na maadili ya utafiti. Sura inayofuata imewasilisha, kuchambua na kujadili data zilizokusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali kama ilivyoelezwa hapo awali.

# SURA YA TANO

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA

## 5.1 Utangulizi

Hii ndiyo sura mama katika utafiti huu ambayo inawasilisha, kuchambua na kujadili data za utafiti ili kusaidia kutimiza malengo ya utafiti huu. Katika sura hii madhumuni mahususi matatu yamekamilishwa ambapo dhamira mbalimbali za kisiasa zinazotokeza katika ushairi wa Kandoro zimeainishwa na kujadiliwa. Baada ya hapo mbinu za kisanaa zinazotumiwa na Kandoro nazo zimewasilishwa na kujadiliwa na baadaye imeoneshwa falsafa ya Kandoro kuhusu maisha kama inavyojitokeza katika ushairi wake.

### 5.1.1 Kandoro na Harakati za Kupigania Uhuru

Kandoro alikuwa mwanaharakati mashuhuri katika kupigania uhuru wa Tanganyika na kupinga utawala wa kikoloni kuanzia mwaka 1940 mpaka uhuru ulipopatikana na baada ya uhuru (Kitogo, 2002). Jambo lisilopingika ni kwamba, Tanganyika kama zilivyokuwa nchi nyingine za Kiafrika zilitawaliwa na Wakoloni ambao walifanya dhuluma, uonevu, ubaguzi, unyanyasaji na uporaji wa rasilimali za Waafrika na mataifa yao (Mpangala, 1977). Kutokana na hali hii Kandoro hakupenda kunyamazia uovu huo na badala yake aliamua kutunga mashairi mbalimbali kuupinga ukoloni ili kujipatia uhuru na kujitawala. Kupitia shairi lake maarufu *la Kwetu ni Kwao Kwa nini* anasema:

*Kwa nini kwao kwa nini, kuwe*
*kwetu ni kwa nini?*
*Na kwenu pia kwa nini, kuitwa kwao kwa nini?*

*Kwa nini ina yakini, kwetu ni kwao kwa nini?*
*Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini.*

Katika ubeti huu Kandoro anaonesha kuchukizwa na namna Wakoloni walivyotawala nchi yetu ya Tanganyika, huku Watanganyika wenyewe wakiwepo na wakiwa na uwezo wa kujitawala wao wenyewe. Vilevile, Kandoro anaonesha kwamba, si bure kuna jambo ambalo liliwafanya Wakoloni kung'ang'ania kutawala nchi ya Tanganyika ndio maana anasema: *Kwa nini ina yakini, Kwetu ni kwao kwa nini?*

Kimsingi, Wakoloni waling'ng'ania kutawala Tanganyika na Afrika kwa ujumla ili kuendelea kunufaika na rasilimali kama vile madini, mazao ya kilimo, ardhi, rasimali watu, kibarua na waajiriwa waliolipwa ujira mdogo, masoko na maeneo kwa ajili ya uwekezaji (Omary 2011). Mambo haya yaliwawezesha kujipatia utajiri mkubwa uliosaidia kuimarisha viwanda vyao huko Ulaya. Kwa hali hii haikuwa kazi rahisi wao (Wakoloni) kukubali kuyapatia uhuru makoloni yake kwa kuwa walifahamu wazi kwamba, nchi za Afrika zikiwa huru hawatapata fusa ya kunyonya rasilimali zao kwa namna wanavyozinyonya wakiwa kama wakoloni. Pamoja na ugumu huo wa Wakoloni kuondoka Tanganyika na kuwapatia Wanatanganyika uhuru wao, Kandoro hakurudi nyuma katika kuwataka kuondoka, aliongeza kasi ya kuwataka Wakoloni kutenga viti vingi zaidi vya Watanganyika katika Bunge kwa kuwa wao ndio wengi ikilinganishwa na Wazungu pamoja na Wahindi. Anasema:

*Viti tunavyovitaka, tupewe na serikali.*
*Sisi ni wengi hakika, kuliko taifa mbili,*
*Haki isiyo na shaka, tuzidi hata viwili,*
*Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika.*

Kandoro anaitaka serikali ya Kikoloni itenge viti kwa ajili ya wawakilishi wa Tanganyika katika baraza la wawakilishi ili wawe watetezi wa nchi na wananchi wake na hatimaye kuutwaa uhuru uliokaliwa na kung'ang'aniwa na watu wa kuja tu yaani Wakoloni. Kandoro anafahamu kwamba, ni katika bunge ndiyo mambo muhimu yahusuyo nchi na mustakabali wa maendeleo yake huwasilishwa, hujadiliwa na kufikia muafaka wa utekelezaji wake. Kama hivyo ndivyo ni dhahiri kwamba uwepo wa Watanganyika katika baraza ungesaidia kusukuma mbele harakati za kudai uhuru na ukombozi wa Tanganyika kutoka katika makucha ya wakoloni na vibaraka wao.

Si hivyo tu, bali pia, katika kuonesha umuhimu wa bunge katika kusaidia kupatikana kwa uhuru Kandoro anaongezea kwamba, baada ya Watanganyika kupata uwakilishi wao bungeni basi lugha rasmi ya kuendesha mijadala ya bunge iwe ni Kiswahili ili Watanganyika ambo ni wajumbe wa baraza waweze kuchangia mijadala mbalimbali barazani kwa lugha wanayoifahamu viziru. Vile vile, si tu kuchangai mijadala kwa lugha wanayoifahamu lakini pia kuelewa yale yanayo jadiliwa ili kukubaliana nayo ama kuyapinga. Kandoro anasema:

*Baraza la Tanganyika, ambalo la serikali,*
*Ndilo tunalolitaka, litimie Kiswahili,*
*Tupate Waafrika, kuendesha serikali*
*Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika.*

Kwa maoni ya Kandoro, iwapo baraza la Tanganyika litakuwa, na Wawakilishi wa Kiafrika na Kiswahili kikawa ndio lugha kuu ya mawasiliano ni rahisi kwa Wawakilishi hao kuwasilisha mijadala ambayo italeta uhuru na usawa miongoni

mwa Watanzania na Waafrika kwa ujumla. Dondoo hili la Kandoro linaendelea kuonesha kwamba, lugha ya Kiswahili ndiyo iliyotumika katika harakati za kudai uhuru na hivyo kuwaunganisha Watanganyika wote. Ni jambo lisilopingika kwamba, Tanganyika ni nchi yenye wakazi wa makabila zaidi ya 120 ambapo bila ya kuwepo matumizi ya lugha Kiswahili ni dhahiri isingewezekana kuwaunganisha na kuwa kitu kimoja. Kandoro kama anavyofahamika anatoka katika mikoa ya Tabora na Kigoma lakini anapigania matumizi ya lugha ya Kiswahili ambayo ni lugha ya Waswahili wa Pwani ya Afrika Mashariki. Hii inaonesha uzalendo wa hali ya juu aliokuwa nao kandoro katika kuiona Tanganyika inakuwa huru na ili hilo lifanikiwe ni lazima lugha ya Kiswahili iwe ndio kiunganishi cha Watanganyika wote.

Katika msisitizo huohuo wa kutaka umoja na mshikamano kama njia pekee ya kuikomboa Tanganyika kutoka katika mikono ya wakoloni, Kandoro aliwataka Watanganyika kuwa na umoja imara kama vile walivyo Siafu. Anasema:

*Siafu wangetengana kama ingefaa hoja,*
*La sivyo wangegombana, wakaiasi pambaja,*
*Waliona si maana, kuvunja wao umoja,*
*Fimbo yetu ni Umoja, kutengana ni udhaifu.*

Kitogo (2002) anasema kwamba, siafu ni mdudu mdogo sana kiumbo lakini kutokana na Umoja wao katika kutenda shughuli mbalimbali wanaweza hata kumuaangusha mnyama tembo. Kwa hali hii, Kandoro anawafananisha Watanganyika kuwa sawa na siafu kwa maana kwamba, hawana uwezo wa kifedha na silaha kama walivyo wakoloni. Hivyo basi, ili waweze kufanikiwa wanahitaji kuwa na umoja kama anavyosema; "*Fimbo yetu ni Umoja, kutengana ni udhaifu*". Naye Kezilahabi (1977) anaungana mkono na maelezo ya Kitogo (2002) kwa

kueleza kwamba, Kandoro ni mtunzi wa mashari mwenye upeo wa hali ya juu katika utunzi wa mashairi yake. Kezilahabi (977) anayasema haya kwa kudondoa beti kadhaa za shairi liitwalo *Siafu Wamekazana* (1972) kwamba, liliwavuta watu wengi na kujiunga na chama cha TANU. Kezilahabi (1977) ananukuu kama ifuatavyo:

*Siafu Wamekazana,*
*Nyoka amegutuka, ndani ya shimo katuna,*
*Tena amekasirika, hasira zenye kununa,*
*Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna*
*Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.*

*Shimoni ataondoka, hilo nataja kwa jina,*
*Nyoka anajuwa fika, siafu wakiungana,*
*Nguvu zinaongezeka, shimoni watagombana,*
*Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.*

Beti hizi kwa hakika zinatia hamasa kwa Watanganyika kuungana kwa pamoja na kuanza kudai uhuru wao kwa hali na mali. Siafu ni mdudu mdogo sana lakini anaweza kumuangamiza nyoka ambaye ni mdudu mwenye sumu kali ya kuhatarisha maisha ya binadamu pamoja na wanyama wengine. Hivyo, hata kwa Watanganyika ni kazi rahisi sana kwa wao kumuondoa mkoloni na kujinyakulia uhuru wao iwapo wataungana. Kandoro anaonesha kwamba, iwapo Watanganyika wakiungana kwa pamoja katika kudai uhuru wao, mkoloni hana jinsi ni lazima aondoke tena kwa amani bila kumwaga damu. Anasema: *Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna*. Umoja tu ndiyo silaha pekee itakayomwondoa mkoloni na hilo lilifanikiwa.

Kwa upande mwingine Kandoro anaonekana kueleza kwamba, pamoja na Watanganyika wote kukubali kuungana kwa pamoja katika kudai uhuru ni lazima pia kuwe na viongozi ambao kazi yao kubwa itakuwa ni kuwaongoza wananchi katika

harakati hizo. Analisema hili kupitia shairi liitwalo *Ondoka nchini Kwetu,* Katika ubeti ufuatao:

*Watokeze watetezi, labda tutatukuka,*
*Tusifanye uupuuzi, tutazidi kuanguka,*
*Ya jana siyo ya juzi, mambo yanabadilika,*
*Waafrika tu wapi, watokeze watetezi.*

Ili Tanganyika na Afrika nzima kwa ujumla iweze kuwa huru ni lazima wawepo watetezi ambao watakuwa ndio viongozi wa kuendesha mapambano. Viongozi hawa wataandaa mipango na mikakati madhubuti ambayo kwayo harakati za kudai uhuru zitafanikiwa. Tulipofanya usaili na bwana Kibwana Mikidadi aliyepo Dar es Salaam alitueleza kwamba:

> *Ili kujipatia uhuru wetu kutoka kwa wakoloni tulihitaji kuwa na viongozi kama Mwalimu Julius Nyerere ambaye kwa kushirikiana na viongozi wengine aliweza kuandaa mikakati maridhawa iliyotuwezesha kuupata uhuru. Nchi nyingine za Kiafrika nazo pia ziliweza kupata uhuru kupitia viongozi shupavu kama Jomo Kenyatta, Samora Masheli, Keneth Kaunda, Kamuzu Banda, Nelson Mandela na kadhalika. Leo hii tumeshindwa kupambana na adui mdogo tu, umasikini kwa kuwa tuomekosa viongozi shupavu kama hawa niliowataja hivi punde.*

Maelezo katika dondoo hapo juu yanaonesha dhahiri shahidi kwamba, uongozi bora ndio silaha ya mafanikio. Uongozi imara na shupavu na viongozi wapigania uhuru wa Afrika walituwezesha kuwaondoa wakoloni waliokuwa wananyonya rasilimali za Waafrika. Msailiwa ameonesha msisitizo kwamba, kumuondoa mkoloni, haikuwa kazi rahisi lakini viongozi hawa waliweza. Viongozi wa leo wanashindwa kumuondoa adui mdogo tu, umasikini na badala yake wanamzidisha adui huyo kwa

kuruhusu uwekezaji na ubinafsishaji usio na tija kwa wananchi na mataifa yao. Hawa ndio viongozi tulionao katika karne hii ya sayansi na tekinolojia. Ili kuweza kumtokomeza adui umasikini ni lazima viongozi wa Afrika wa leo wajifunze mbinu, mipango na mikakati iliyokuwa inatumiwa na viongozi wapigania uhuru wa Afrika. Lengo si kuichukua mikakati hiyo kama ilivyo bali kuimarisha ili iendane na hali halisi ya maisha ya sasa.

### 5.1.2 Kandoro Muhamasishaji wa Kisiasa

Uhamasishaji ni kitendo cha kuwafahamisha watu juu ya umuhimu wa jambo fulani na kuwataka kulifanya ili lilete manufaa na maendeleo kwa jamii. Saadan Kandoro aliona kwamba, njia pekee itakayowawezesha Watanganyika kupata uhuru wao ni Umoja na mshikamano. Uelewa huu ulimfanya kuchukuwa jukumu la kuhamasisha wananchi kufanya mambo mbalimbali aliyoyapendekeza kama njia ya kujipatia uhuru. Miongoni mwa mambo hayo ni pale anaposema:

*Sasa sikifani chenu, kutawaliwa nchini,*
*Tazameni hali zenu, mtakubali yakini,*
*Watazameni Wenzenu, watu wa Ghana nchini*
*Waafrika njooni, njooni, muandike TANU.*

*Njooni katika TANU, na tusimame foleni,*
*Chama chetu ni cha TANU, msikae ujingani,*
*Kina Sedi, Kina Nuru, hima upesi njooni,*
*Waafrika njooni, njooni mwandike TANU.*

Katika madondoo hapo juu, Kandoro anafanya uhamasishaji wa kuwataka wananchi wajiunge na chama cha TANU ili wakipe nguvu ya kuweza kuvishinda vyama vingine vilivyokuwepo na kisha kuunyakua uhuru kutoka mikononi mwa Wakoloni. Kandoro anaanza uhamasisishaji wake kwa kuwaeleza wananchi watazame hali zao na za wenzao zilivyoduni na kwamba aliyesababisha yote hayo ni mkoloni. Ili

mkoloni huyu aweze kuondolewa ni lazima chama cha TANU kiwe na nguvu inayotokana na wanachama wake ambao watachangia fedha, mawazo na mali nyingine. Ndio maana Kandoro anasema: *Waafrika njooni, njooni mwandike TANU*. Iwapo wananchi watajitokeza kwa wingi na kujiunga na Chama cha TANU kitakuwa na nguvu ya kuweza kuwashinda Wakoloni na washirika wao.

Vile vile, katika madondoo ya Kandoro hapo juu yanaonesha kwamba ili Watanganyika waweze kujikomboa kutoka katika makucha ya wakoloni walihitaji kuwa na taasisi ambayo wataimiliki wao wenyewe. Taasisi ndio yenye uwezo wa kuratibu taratibu mbalimbali zinazohusiana na masuala ya kudai uhuru na taasisi hiyohiyo ndiyo itakayokabidhiwa madaraka ya kuiongoza nchi mara baada ya uhuru kupatikana. Taasisi ndiyo yenye uwezo wa kuhakikisha kwamba, usawa na amani vinapatikana kwa wananchi wake wote. Iwapo uhuru utapatikana na madaraka na mamlaka kukabidhiwa kwa mtu binafsi badala ya taasisi ni dhahiri kwamba mtu huyo ataiongoza nchi hiyo kwa matakwa yake mwenyewe na raia watakosa haki za msingi katika nchi yao. Kandoro aliliona hili ndio maana msisitizo wake ukawa ni katika kuwataka wananchi kujiunga na TANU ili kukifanya kuwa taasisi iliyo makini na mdhubuti kabisa. Akizungumza katika mjadala ulioandaliwa na Kigoda cha Mwalimu Nyerere mwaka 2011, Mzee Kingunge Ngombale Mwiru anasema:

> CCM ni Chama kilichoundwa katika misingi ya Kitaasisi na kina uwakilishi mpaka katika ngazi za chini kabisa za utawala yaani ngazi ya shina na matawi. Msingi huu haukuanza leo bali tangu enzi za TANU. Mwalimu alikifanya chama hiki kuwa ni chama cha wananchi na sio chake yeye ndio maana mpaka leo hii kinaimarika siku hata siku licha ya kuwepo mafisadi wachache wanaokiyumbisha chama chetu.

Mawazo ya mzee Kingunge Ngombale Mwiru yanalandana na yale ya Saadani Kandoro kwamba iwapo Chama kitakuwa kimeundwa kwa misingi ya kitaasisi basi ni dhahiri kwamba, hakitayumbishwa kiasi cha kuporomoka kama ilivyo kwa vyama vingine visivyo na hadhi ya kitaasisi. Kwa msingi huu basi, tunakubaliana na mawazo ya Kandoro kwamba, uimara wa CCM unaoonekana leo unatokana na misingi bora ya Kitaasisi iliyoundwa tangu enzi za chama cha TANU. Kwa maoni yetu, mawazo haya ni ya kiwango cha hali ya juu sana kupata kutolewa na mtunzi wa mashairi na yana mchango mkubwa katika kuzielewa siasa za Tanzania hasa katika mfumo wa vyama vingi vya siasa uliopo sasa.

Kandoro anaendelea kufanya uhamasishaji kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuwa wakweli na waaminifu katika zoezi zima la kupambana katika kupigania uhuru. Iwapao kila mtu atakuwa mkweli na mwaminifu basi uhuru utapatikana na maisha baada ya uhuru yatakuwa ya upendo, amani, umoja na mshikamano. Kandoro anasema:

*Kwa kweli nasikitika, tena naona simanzi*
*Shairi nililoliandika, amepewa kijakazi,*
*Mary hakuliandika, kutunga hivyo hawezi,*
*Sasa natuanze kazi, kutetea Afrika*.

Katika dondoo hili tunaoneshwa kwamba, shairi aliloliandika Kandoro lilipotea na baada ya muda fulani likatokea katika gazeti moja huku mtunzi akitajwa kwa jina la Mary (Kitogo, 2002). Ukweli ni kwamba, shairi hili lilitungwa na Kandoro na si Mary kwani Mary hakuwa na uwezo wa kutunga shairi kama hilo. Anachokisema Kandoro hapa ni suala la kuwa wakweli na waaminifu kwani kudanganya katika utunzi na uandishi kama alivyofanya Mary kutarudisha nyuma harakati za kuleta

ukombozi kwa jamii. Udanganyifu wa aina hii utakwenda mbali mpaka katika kuwarubuni wananchi katika harakati za kudai uhuru wakasahau lengo lao na kujikuta wameingia katika kuwaunga mkono wakoloni.

Vilevile, Kandondoro anaonya juu ya udanganyifu akifahamu kwamba hata baada ya kupatikana uhuru tunaweza kupata viongozi wasio waaminifu ambao watajiingiza katika vitendo vya rushwa na wizi wa rasilimali za nchi. Tunayaunga mkono mawazo ya Kandoro kwa asilimia mia kwa mia tukitambua kwamba tabia ni mazoea.

*Shabaha niliyoitaka, watokee watetezi*
*Kuamsha Afrika, tuache ya upuuzi,*
*Na kujitoa sadaka, kupigania malezi*
*Sasa natuanze kazi, kutetea Afrika.*

Katika dondoo hili Kandoro anahamasisha wananchi kuachana na masuala ya upuuzi na kutia hima katika harakati za kudai uhuru kutoka wa wakoloni. Kandoro alielewa kwamba kipindi kile cha kudai uhuru Waafirka walikuwa ni watu masikini wasio na uwezo wa fedha ndio maana anasema: *Na kujitoa sadaka, kupigania malezi.* Ni dhahiri kwamba, wakoloni walinyonya rasilimali za nchi za Kiafrika na kuwaacha Waaafrika wakiwa hoi taabani. Hivyo, kujitolea kushiriki katika harakati za kudai uhuru ndio njia pekee ambayo ingesaidia katika kuongeza ari na nguvu kwa viongozi waliokuwa msitari wa mbele katika mapambano na Wakoloni.

Kujitolea kunakosemwa na Kandoro ni kama vile kutoa sehemu ya mali zao kama vile mazao, mifugo na kuhudhuria katika mikutano mbalimbali ya hadhara iliyokuwa inaandaliwa na Uongozi wa TANU ili kusikiliza mipango na sera za kumkomboa mwananchi kutoka katika mikono ya Wakoloni. Akizungumza katika kituo cha Televisheni ya Taifa (TBC1) mwaka 2001 Bibi Titi Mohamed anasema:

> *Katika harakati za kudai uhuru, wananchi hasa wanawake walijitolea rasilimali zao kama vile chakula, fedha, mifungo na kujitokeza kwa wingi katika harakati za kudai uhuru hasa mikutanoni. Kuchangia kwao katika harakati hizo kulileta hamasa kubwa katika vuguvugu la kudai uhuru na kwa dhati kabisa kuwezesha kupatikana kwa uhuru. Wanawake walishiriki kuandaa nyimbo za kuwakejeli wakoloni na kuwapamba viongozi wa TANU kuwa ndio tumaini lao*.

Maelezo ya Bibi Titi Mohamed yanaonesha mwitiko wa wananchi kwa mashairi ya Kandoro yaliyowataka kujitolea sadaka ili kufanikisha ukombozi wa nchi yao. Maelezo haya pia yanaonesha kwamba, wanawake ndio hasa waliokuwa msitari wa mbele katika kuwasaidia wapigania uhuru kufanikisha azma yao. Ukweli huu unaonekana hata katika maisha ya leo ambapo wanawake ndio wanaoshiriki kikamilifu katika harakati za kisiasa na chaguzi mbalimbali na kuwapigia kura wagombea mbalimbali hasa wanaume katika nyadhifa za ubunge na udiwani.

Si hivyo tu, bali pia Kandoro alisisitizia sana suala la kupigania malezi ili kuhakisha kwamba vijana na wananchi wote kwa ujumla wanakuwa ni watu wenye heshima na adabu ili hata wakoloni waone kwamba, wanastahili kutoa uhuru kwa watu waliostaarabika. Anasema: *Na kujitoa sadaka, kupigani malezi*. Uhamasishaji huu wa Kandoro ulifanikiwa kwani hata ujumbe wa Umoja wa Mataifa uliotumwa kuja kutazama kama kweli Watanganyika ni watu waliostaarabika na wanastahili kupatiwa uhuru walithibitisha kwamba, Watanganyika ni watu wema, wenye heshima, ukarimu na upendo. Hali hii iliulazimu Umoja wa Mataifa kuwataka Waingereza kutoa uhuru kwa Tanganyika ili wajitawale wenyewe. Hili nalo bila shaka lilifanikiwa na mwaka 1961 Tanganyika ilipewa uhuru wake.

Kwa msingi huu, Watanganyika na baadaye Watanzania wameendelea kujihimu katika kudumisha malezi bora kwa jamii na kuendelea kupata sifa duniani kote kwamba, wao ni wakarimu, wapole, wenye upendo na amani. Nchi jirani na Tanzania zinatamani sana ukarimu na upendo wa Watanzania uhamie nchini mwao ili waishi maisha mazuri. Hata hivyo, kutokana na utandawazi yapo mambo ambayo kwayo maadili ya jamii hupotoshwa na kidogo kidogo Watanzania wanaaza kupoteza ukarimu, upendo, uvumilivu na kuwa wabinafsi wanaojiiingiza katika rushwa na ufisadi mkubwa unaokwamisha jitihada za kujiletea maendeleo. Kwa mfano, serikali imepoteza fedha nyingi kupitia mikataba isiyo na tija iliyoingiwa baina yake na wawekezaji katika sekta mbalimbali ikiwemo ile ya madini. Mikataba iliyoingiwa inaonekana kuwanufaisha zaidi wawekezaji kuliko serikali na wananchi wake. Hili limeweza kufanyika kutokana na ukweli kwamba, watia saini kwa upande wa serikali wamepokea rushwa ndio maana wakakubali kusaini mikataba ya aina hiyo. Hii yote inatokana na kudhoofika kwa malezi ya Watanzania tangu wanapokuwa watoto wadogo mpaka kufikia kuwa watu wazima.

Hata hivyo, ingawa viongozi wetu wanakubali kuingia mikataba ambayo wanafahamu haina tija kwa taifa kwa upande mwingine inaonesha kuwa wawekezaji wa sasa ndio walewale wakoloni wamekuja kivingine na wanaendeleza azma yao ya kunyonya rasimali za mataifa masikini kwa faida yao. Kandoro (1961) kama anavyonukuliwa na Kitogo (2002:82) anasema:

> *We all know that, the British are here to exploit us so as to benefit themselves and that they are not here because they feel sorry for our situation and want to civilize us and bring about development. Such words are the highest point of euphemism aimed at blinding us. As long as they will be there increasingly our*

> *mineral and financial resources would be transported back to their country where their survival depend on us*.
>
> Wote tunatambua kwamba, Waingereza wapo hapa kwa ajili ya kutunyonya ili kujinufaisha wao wenyewe na si kwamba wapo hapa eti kwa sababu wanatusikitikia sana kutokana na hali zetu na wanataka kutustaarabisha na kutuletea maendeleo. Kuendelea kwao kuwepo hapa ndiyo rasilimali zetu kama vile fedha na madini zitaendelea kusafirishwa kwenda nchini mwao ambapo maisha yao yanatutegemea sisi (Tafsiri yangu).

Hii ndio nia na tabia ya mkoloni daima dumu. Hivyo, Kandoro alijitahidi sana kuwahamasisha wananchi kuendelea kupambana mpaka hatua ya mwisho ili kuhakikisha mkoloni anaondoka jambo ambalo lilifanikiwa. Utegemezi wa mataifa ya kigeni kwa nchi za Kiafrika bado unaendelea mpaka leo ambapo rasilimali nyingi zinachukuliwa na wageni hao kupitia mashirika mbalimbali ya kiuwekezaji na kuufanya umasikini kukuwa kwa kasi zaidi katika nchi changa kama Tanzania. Kwa msingi huu basi, nchi kama Tanzania zinatakiwa kuhakikisha kwamba, wale wanaopewa dhamana ya kuingia mikataba kwa niaba ya serikali wanafanya hivyo kwa uaminifu na utalaamu wa hali ya juu. Hili litafanikiwa pale tu miiko ya uongozi itakapowekwa bayana na kila mtu akaielewa na akiivunja basi aadhibiwe kwa mujibu wa sheria. Vilevile, mafunzo muhimu juu ya kusaini mikataba ya kimataifa yatolewe kwa wahusika ili wasiingie katika kusaini mikataba wakiwa mbumbumbu. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ubabaishaji na ufisadi katika kusaini mikataba isiyo na tija kwa taifa.

Kwa upande mwingine tunamuona Kandoro akitoa matumaini kwa wananchi kwamba, uhuru utakaopatikana ni wa watu wote na utawanufaisha wananchi wote kwa kuwa viongozi watakaoiongoza nchi ni shupavu na jasiri tena watenda haki. Hivyo hakuna haja ya mwananchi yeyote kuwa na hofu kwamba, labda uhuru ukipatikana maovu ya kikoloni yataendelea. Anasema kupitia shairi lake liitwalo *Msiogope Mawimbi*, kuwa:

*Kule walikozaliwa, ndiko lapelekwa ombi,*
*Mambo yamefunuliwa, kuna moto wa makumbi,*
*Kigoda kimetwaliwa, na wenyewe Wamatumbi*
*Msiogope mawimbi, ndio mwendo wa ngalawa".*

*Majini hamjatiwa, msijitie mikambi,*
*Ngalawa kutimuliwa, msiogope mawimbi,*
*Liko lililoteuliwa, Kongo si aridhi mbi,*
*Msiogope mawimbi, ndio mwendo wa ngalawa.*

Hapa Kandoro anawatoa wananchi hofu kwamba pengine wakoloni wakiondoka maisha yatakuwa duni la hasha. Anaamini kwamba uhuru ukipatikana haki itatendeka kwa kila mtu bila ubaguzi wa aina yoyote ile. Kandoro anawataka wanachi kutokata tamaa ya mafanikio ya kujitawala wao wenyewe kabla hata hawajaanza kujitawala rasmi. Viongozi wazawa ndio wanaojua vizuri matatizo ya wananchi kwa kuwa nao ni sehemu ya jamii kuliko ilivyokuwa kwa Wakoloni ambao walijali masilahi yao kuliko yale ya wananchi. Kwa hali hiyo basi, wananchi hawana haja ya kuogopa kujitawala. Anawatahadharisha wananchi kwamba, wasiogope mawimbi, ndio mwendo wa ngalawa. Hapa anatumia taswira kueleza kwamba, kwa kuwa mkoloni alitawala Tanganyika kwa miaka mingi basi atakapoondoka kwa mwanzoni itasababisha mapungufu fulani katika shughuli mbalimbali zikiwemo za utoaji huduma na kadhalika. Baada ya muda mfupi kila kitu

kitakuwa sawa na maisha yataendelea kuwa mazuri kuliko ilivyokuwa katika kipindi cha ukoloni. Ni kwa kiwango gani hili lilifanikiwa tazama majadala wa matokeo ya utafiti huu.

### 5.1.3 Kandoro na Masuala ya Elimu

Suala la elimu katika kipindi cha ukoloni lilikuwa tata mno pale ambapo waliopata fursa ya kupata elimu walikuwa ni watoto wa Machifu, Wazungu Waarabu pamoja na Wahindi. Watoto wa Watanganyika wa hali ya chini hawakupata fursa ya kusoma. Kukosa elimu kwao kuliwafanya kuendelea kuwa wajinga na kukosa upeo wa kuona mbali na kuendelea kuwatumikia Wakoloni na kuwanufaisha zaidi. Tunasema kuwanufisha zaidi wakoloni kwa msingi kwamba, watu hao waliokosa elimu hawakuwa na kazi nyingine ya kufanya zaidi ya kuchukuliwa manamba na kutumikia mashamba ya wakoloni. Kandoro kupitia shairi lake la *Tumshukuru Manani* alilotunga mnamo mwaka 1961, anasema:

*Shuleni hatukutiwa, ili tuwe ujingani,*
*Fasi hatukupatiwa, kutiwa utajirini,*
*Kutwa kucha huzomewa, kama majitu haini.*

Ubeti huu unaeleza mambo kadhaa; kwanza likiwa ni lile la Watanganyika kutopewa nafasi ya kupata elimu. Yapo mambo yaliyopangwa na kufanywa na Wakoloni ili kuhakikisha kwamba Waafrika hawapati elimu na hata kama wakiipata basi ni elimu iliyo duni isiyoweza kuwafangua macho na kuona mbali. Miongoni mwa mambo hayo ni lile la kuweka malipo ya ada kama kigezo muhimu cha wanafunzi kupokelewa na kujiunga na shule. Kwa hali ilivyokuwa, Waafrika wengi hawakuwa na kipato cha kuwatosha kwa ajili ya matumizi ya chakula nyumbani sembuse ada ya

kumlipia mwanafunzi? Hiki kilikuwa ni kikwazo kikubwa kwa watoto wa Waafrika kukosa elimu. Kitogo (2002:86) anasema:

> *In education for instance, the government contributed for each sudent 30/= for European pupils. 15/= shillings for Asians and only 3/= shilling for Africans."*
>
> Katika upande wa elimu kwa mfano, serikali ya Kikoloni ilichangia shilling 30/= kwa mwanafunzi wa Kizungu, shilling 15/= kwa mwanafunzi wa Kiasia na shilling 3/= tu kwa mwanafunzi wa Kiafrika" (Tafsiri yangu).

Dondoo hili linaonesha namna mzazi wa mtoto wa Kiafrika alivyoachiwa na serikali mzigo mkubwa na kulipa ada ya mtoto wake huku wakitambua bayana kwamba kipato cha Waafrika ni duni.

Jambo la pili lililofanywa na wakoloni katika kuwazuia watoto wa Kiafrika kupata elimu bora ni lile la kutowapa nafasi ya kusoma katika shule zilizotoa elimu bora ambazo nyingi ya hizo zilitengwa kwa ajili ya Wazungu na zile za kati kwa ajili ya Wahindi na Waarabu. Ubaguzi huu unaoneshwa na Kandoro pale anaposema: *Fasi hatukupatiwa, kutiwa utajirini*. Hii inaonesha kwamba, hata kama mzazi wa mtoto wa Kiafrika alipata kuwa na uwezo wa kumlipia mwanae kusoma katika shule zilizotoa elimu bora bado asingeruhusiwa kutokana na ubaguzi wa rangi uliokuwepo wakati huo.

Kwa mantiki hiyo basi, Waafrika walibaki kuwa masikini wa kutupa kutokana na kukosa elimu. Kandoro anasema: *Fasi hatukupatiwa, kutiwa utajirini.* Hii inaonesha kwamba, mtu akipata elimu basi ataondokana na umasikini kisha anakuwa tajiri. Kuwanyima Waafrika nafasi ya kupata elimu ilikuwa ni namna ya kuwafanya

kuukosa utajiri. Kutokana na hilo Waafrika walizarauliwa sana na Wakoloni. Kama asemavyo kandoro: *Kutwa kucha kuzomewa, kama majitu haini.* Hapa Kandoro anatumia taswira kumaanisha kwamba, Mwafrika alifanyishwa kazi yoyote ile aliyoitaka mkoloni kwa malipo kiduchu. Kandoro alichukizwa na hali hii ndio maana akaamua kuandika mashairi ya kuwahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi katika harakati za kupigania uhuru na kumuondoa mkoloni ili kuwepo na usawa katika elimu nchini.

Mawazo ya Kandoro kuhusu elimu na utajiri hayapingiki mahali popote hata wale waliosema Afrika inakabiliwa na maadui watatu yaani ujinga, maradhi na umasikini wanakubali kwamba, ujinga ndiye adui mkubwa kuliko maadui wengine. Dawa ya ujinga ni elimu ambapo mtu akisoma ataondoa ujinga na ndio utajiri wenyewe. Kandoro anaeleza kuwa:

*Maadui twaambiwa, ni watatu twabaini,*
*Ujinga twasimuliwa, ni adui namba wani,*
*Na maradhi, yametiwa, pamoja Umasikini.*

Pamoja na mambo mengine ubeti huu unaonesha kwamba, elimu ni utajiri mkubwa ambao utasaidia kufuta ujinga na kisha kufanikisha harakati za kutokomeza maradhi na umasikini.

Kandoro hakuishia tu katika kueleza umuhimu wa elimu kwa jamii bali pia alipata kutambua kwamba, kusoma si jambo jepesi na linahitaji juhudi, na bidii binafsi za msomaji. Katika shairi lake la *Soma sana kwa bidii* anasema:

*Kusoma ni nuru yako, asomae hafifii,*
*Kusoma ni sifa zako, jina halikuwa hii.*

Kandoro anawahamasisha watu kusoma kwa bidii kwa sababu elimu watakayoipata itawasaidia wao binafsi katika maisha yao yote. Vilevile, elimu hiyo itawasaidia watu wanaowanzunguka katika kupambana na hima mbalimbali za maendeleo. Kwa mfano; kama kijana atakuwa amesomea fani ya Ualimu basi atafundisha katika shule iliyopo pale kijijini na kisha kupatikana wasomi wengine wa baadaye. Ndio maana Kandoro anasema *Kusoma ni nuru yako.* Elimu ni mwanga ambao si tu hutumika katika kumwangazia yule aliyesoma bali pia wale wanaomzunguka na jamii kwa ujumla.

Kwa upande mwingine, Kandoro anaonesha kutambua kwamba, elimu bora hupatikana kutokana na mambo mengi likiwemo lile la miundo mbinu bora ya shule. Anasema:

*Mungu shule ibariki,*
*Itoe watoto wema, wasio wabaramaki,*
*Wawe watoto ulama, wasiwe wenye hamaki,*
*Wenye nguvu za kusoma, kuipigania haki,*
*Mungu shule ibariki, itoe watoto wema.*

Ubeti huu unamuonesha Kandoro akiomba dua kwa Mwenyezi Mungu kuwa azijaalie shule kuwa ni mahali salama pa kuweza kujenga maadili ya wanafunzi ili waweze kuwa na maadili mema na nidhamu iliyotukuka. Mawazo haya ya Kandoro ni muhimu na yana ukweli fulani kuhusu shule, nidhamu na maendeleo ya wanafunzi. Hata hivyo, Kandoro amesesahau kwamba, Miundombinu ya shule na nidhamu ya wanafunzi haviwezi kujengwa kwa kumuomba Mwenyezi Mungu peke yake bila ya wahusika kuchukua hatua muafaka.

Nchini Tanzania kwa mfano, katika kipindi cha Mwaka 2001-2010 zimejengwa shule za serikali za sekondari katika kila kata. Hili limefannikiwa kwa kiasi kikubwa sana ambapo kila kata inamajengo kadhaa ya madarasa kwa ajili ya kidato cha kwanza mpaka cha nne. Kwa bahati mbaya zipo baadhi ya shule ambazo majengo yake yamejengwa chini ya kiwango na yameanza kuporomoka na kubomoka. Hii inaonesha kwamba, waliopewa dhamana ya kukamilisha majengo haya hawajayajenga kwa kiwango kinachotakiwa kutokana na kuchukua rushwa kwa waliopewa zabuni za ujenzi wa majengo hayo. Hii yote inaonesha kwamba, kumuomba Mwenyezi Mungu pekee hakutasaidia kitu kama hatua madhubuti za kisheria hazitachukuliwa dhidi ya mafisadi na wala rushwa. Kwa kufanya hivyo, shule zitajengwa kwa kiwango kinachotakiwa na kuzifanya kuwa na miundo mbinu imara ambayo itadumu kwa miongo kadhaa ijayo.

### 5.1.4 Kandoro na Masuala ya Haki

Haki za binadamu ni jambo linalotawala katika taarifa za habari mbalimbali duniani hasa kutokana na mapigano ya wenyewe kwa wenyewe yanayoendelea katika nchi kadhaa kama vile; Siria, Kongo, Israel na Palestina pamoja na nchi kadhaa za Afrika ya Magharibi ikiwemo Mali. Mambo haya yanatokea kwa sababu kuna watu au jamii ama kikundi fulani kinadai kudhulumiwa haki zake na kundi lingine katika jamii. Katika kudai ama kupigania haki zao wahusika hutumia njia mbalimbali kama zile za mazungumzo ambayo huleta muafaka na wengine hutumia njia ya mapigano ambayo kwayo huongeza ukiukwaji wa haki za binadamu. Kandoro anasema kwamba, ipo haja ya kila mtu kupigania haki yake na nchi yake kwa gharama yoyote iwayo. Anasema kupitia shairi la *Shujaa Haogopi Kilicho Halali Yake* kuwa:

*Hutetea nchi yake, asiichafue mtu,*
*Yu tayari peke yake, kuutembelea mwitu,*
*Shujaa haogopi kitu, kilicho haali yake*.

Katika ubeti huu Kandoro anaonesha kwamba, haki huwa haitolewi kirahisi rahisi tu ni lazima ipiganiwe. Hapa anawataka Watanganyika kupigania haki yao ya kuupata uhuru wao na kamwe wasirudi nyuma kwa kuwa shujaa haogopi kitu kilicho halali yake. Ilikuwa ni halali kwa Watanganyika kupata haki ya kusoma, matibabu, kuajiriwa na kulipwa mishahara mizuri, kuchagua na kuchaguliwa kuwa viongozi pamoja na haki nyinginezo lakini haki zote hizi walinyimwa na mkoloni. Katika kusisitiza haja ya kudai haki hizi, Kandoro kupitia shairi lake la *Haki huvunja mlima*, anasema:

*Hakika nimebaini, walimu walivyosema,*
*Edita usinihini, shairi litoe hima,*
*Kiongozi wa jeshini, haogopi lawama,*
*Haki huuvunja milima, niliambiwa shuleni*.

Kandoro anaonesha kutokataka tamaa ya kudai haki ya kuupata uhuru kutoka kwa wakoloni akiamini kwamba siku moja itapatikana kwa kuwa haki ya mtu huwa haipotei.

Katika kuonesha kwamba Watanganyika walinyimwa haki zao za msingi, watunzi mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili walijitokeza na kuandika kazi mbalimbali za kudai haki. Kwa mfano; Shaaban Robert katika riwaya zake za *Kusadikika* na *Kufikirika* ameandika kwa urefu kuhusu madhila ya wakoloni dhidi ya haki za binaadamu katika Tanganyika. Katika *Kusadika* kwa mfano, Shaaban Robert anasema:

> *Damu ya mtu ni halali kumwagwa kwa kafara kama imebidi kuokoa maisha ya Mfalme, Malikia, mtoto au jamaa na nyumba ufalme na kuwa mfalme ana uwezo kwa sheria hii kuamuru kuchinjwa kwa mtu au watu wa hali au umbo ambalo linahitajiwa kwa kafara* (uk. 43).

Kwa hali hii, sababu ya kudai haki na kufanya mapinduzi inalazimu kutekelezwa ili kujenga jamii katika msingi ya haki na usawa bila kujali rangi, kabila, dini wala jinsia (Chuachua, 2011). Hivi ndivyo namna haki za Watanganyika zilivyovunjwa na wakoloni. Kandoro hakupenda kuona haki hizo zinaendelea kuvunjwa ndiyo maana akawataka watu wajitokeze kwa dhati kabisa bila woga wowote katika kudai haki zao. Baada ya kutoa maelezo juu ya kupigania haki kwa ujumla sasa tuangazie haki ya umiliki wa ardhi.

### 5.1.5 Kandoro na Umiliki wa Ardhi

Ardhi ni rasilimali muhimu katika maendeleo ya jamii ama taifa lolote lile liwalo duniani. Tunasema hivi kwa sababu ni katika ardhi ndio shughuli zote za kiuchumi, kisiasa na kijamii hufanyika. Mataifa ya Ulaya yamepata maendeleo makubwa waliyonayo leo kutokana na kutumia ardhi ya Makoloni waliyotawala. Wakulima na wafugaji ambao ndio huunda kundi kubwa la wananchi hutegemea ardhi katika shughuli zao za kila siku za kilimo na ufugaji. Haki hii kwa kiasi kikubwa waliikosa katika kipindi cha ukoloni. Kupitia shairi la *Kwetu ni kwao kwa nini*, Kandoro anasema:

> *Mtu huuliza nini, kitu hiki cha nani?*
> *Kitu hiki ni cha nini, na hiki kitu cha nani*
> *Nacho kinaitwa nini? ni cha nani kwa nini?*
> *Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini*?

Katika ubeti huu Kandoro ana shangaa kwa nini wakoloni wanaendelea kukalia ardhi ya Watanganyika ambao wamejikuta hawana ardhi nzuri kwa ajili ya Kilimo. Bila shaka kupitia maneno, “kwa nini” na “nini” yanayojitokeza katika ubeti huu, mshairi anawataka wananchi kujiuliza maswali kadhaa. Kwa mfano; kuna sababu zipi zinazowafanya wakoloni kuendelea kukalia ardhi yao? Kujiuliza swali hili kutawafanya kuongeza ari ya kudai ardhi yao ili wajikomboe na kujitegemea wao wenyewe. *Kwetu ni kwao* kwa sababu wananufaika na rasilimali zilizopo nchini ikiwemo ardhi na *kwao kwetu kwa nini* kwa sababu ni masoko ya bei ya chini ya bidhaa zitokazo nchini mwetu kupitia nguvu zetu na ardhi yetu. Ufahamu huu ulipowafikia wananchi wengi ikawa rahisi kumuondoa mkoloni katika Tanganyika. Katika ubeti mwingine anasema:

*Mtu kwao kuthamini, ijapokuwa jiweni,*
*Pia alale mtini, na baraza liwe chini,*
*Nile matunda porini, kuitwa kwenu kwa nini*?
*Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini*?

Katika ubeti huu mshairi anaelezea umuhimu wa mtu kuwa na umiliki wa sehemu yake ya ardhi ambayo atafanya kuwa makazi yake. Kwake yeye, kuwa na sehemu ya ardhi ni jambo la msingi hata kama mtu hana uwezo wa kujenga nyumba nzuri ya kuishi lakini anamiliki ardhi-hiyo inatosha. Hata kama mtu anaishi juu ya mti lakini mti huo si upo juu ya ardhi? Hata kama mtu anaishi kwa kula matunda, matunda hayo si yanapatikana katika ardhi? Kwa nini wakoloni waichukue ardhi yetu na kutusababishia shida ya chakula na malazi? Kwa Kandoro maswali haya yalimlazaimu kujifunga mkanda na kuwahamasisha wananchi wote kuunga mkono juhudi za kumuondoa mkoloni na utawala wake.

### 5.1.6 Kandoro na Suala la Rushwa

Rushwa ni kitendo cha mtu kujipatia kipato kisicho halali yake ili atoe huduma fulani kwa mtoa rushwa (Mpangala, 2007). Rushwa ni tatizo ambalo linakwamisha sana maendeleo hasa pale inapokuwa imetolewa ili mzabuni fulani aweze kushinda zabuni. Mzabuni huyu anatoa rushwa halafu anapewa kazi labda ya ujenzi wa barabara. Mzabuni huyu atalazimika kujenga barabara kwa kiwango cha chini ili aweze kufidia gharama alizotoa kama rushwa. Hali hii inaifanya serikali kutumia fedha nyingi na kile kinachojengwa hakidumu kwa muda uonaopaswa na hivyo kuilazimu serikali kujenga tena barabara hizo kwa gharama nyingine na kumbe fedha hizo zingetumika katika kutoa huduma nyingine.

Rushwa ni tatizo ambalo limedumu katika serikali zote nne zilizoiongoza nchi hii tangu kupatikana kwa uhuru. Kandoro kupitia shairi lake la *Rushua* anasema:

*Japo ni mwenye elimu, mwenye mali na akili,*
*Mwenye hadhi na fahamu, na fundi wa kujadili,*
*Ingawa awe hakimu, hukumu za mawakili,*
*Abadani si halali, kula rushua haramu*.

Kupitia ubeti huu, mshairi anaonesha kwamba rushwa katika jamii huchukuliwa na watu wa aina mbalimbali hasa wasomi. Wasomi ambao ndio hutegemewa na wale wasio na elimu katika kuwaongoza na kuwaletea maendeleo wao ndio namba wani katika kudai na kupokea rushwa. Vilevile, mshairi anaitaja idara ya mahakama kuwa nayo imo katika mkondo wa rushwa pale mahakimu wake wanapodai rushwa ili waweze kupindisha sheria na kudhulumu haki za baadhi ya raia. Sulala hili ni baya na lina athari kubwa katika ustawi na mustakali wa taifa.

Si hivyo tu, bali pia Kandoro anaendelea kuonesha kwamba, jamii imekuwa ikiwatukuza wapokea rushwa badala ya kuwapinga, kuwafichua na kuwafikisha katika vyombo vya sheria. Kandoro anaonesha kwamba, mpokea rushwa hupewa sifa na nyadhifa mbalimbali kutokana na fedha ama utajiri alioupata kwa njia ya rushwa. Anasema:

*Vyeo adhimu adhimu, wakadhalika na mali,*
*Pia na kukuheshimu, na kukusifu akili,*
*Vyote watakukirimu, zindukana taamuli,*
*Abadani si halali, kula rushua haramu.*

Ubeti huu unarejelea yale yanayotokea katika maisha ya kila siku ya jamii. Katika jamii ya leo mtumishi akihamishwa kutoka kitengo cha kukaa ofisini katika mamlaka ya mapato na kupelekwa katika kitengo cha ushuru wa forodha watu husema huyu mtu ameshakuwa tajiri. Ameshakuwa tajiri kwa maana kwamba, atachukua rushwa ya kutosha kumfanya kuwa tajiri. Ikatokea bahati mtumishi huyu akawa si mla rushwa na akastaafu bila ya kuwa na chembe ya utajiri iliyodhaniwa na watu basi atachekwa na kuonekana mpumbavu aliyekithiri.

Mtazamo huu umewafanya baadhi ya watumishi kuongeza kasi ya kutenda vitendo vya rushwa ili wajilimbikizie mali wasionekane kuwa ni wapumbavu pale watakapostaafu bila ya kuwa na utajiri uliotegemewa na wengi. Hali hii imesababisha rushwa kukithiri na kupewa msamiati ujulikanao kama “ufisadi”. Method (2012) anasema:

> *Nchini Tanzania suala la ufisadi limeibuliwa na wanasiasa Miaka ya hivi karibuni. Matumizi ya neno*

> *hilo yalianza kushika kasi katika kile kilichoitwa orodha ya aibu iliyotolewa na Chama cha upinzani cha CHADEMA (CHAMA Cha Demokrasia na Maendeleo) kikitaja majina ya viongozi mbalimbali waliowatuhumu kuhusika na ufisadi. Kashfa kama vile ya ununuzi wa rada, utoaji wa zabuni kwa kampuni hewa ya Richmond, na uchotaji wa mabilioni ya fedha katika akaunti ya madeni ya nje ya Benki Kuu ya Tanzania (EPA) kulipanua muamko wa Watanzania katika suala la Ufisadi.*

Hapa tunaoneshwa mfumo wa rushwa ulivyotandawaa kiasi cha kuitwa ufisadi. Hii yote inasababishwa na tamaa ya kutaka utajiri wa harakaraka miongoni mwa watumishi wa serikali. Kandoro anaendelea kuonya kwamba:

> *Kula rushwa haramu, amekataza Jalali,*
> *Na serikali naamu, na wao wamekubali,*
> *Hiyo haramu adhimu, si shuruti iwe mali,*
> *Abadani si halali, kula rushua haramu.*

Tunakubaliana na Kandoro kwamba, rushwa si jambo zuri na lina athari kubwa kwa jamii kwa ujumla. Mafundisho ya dini yana nafasi kubwa katika kupunguza vitendo vya rushwa nchini kama yatatolewa kwa namna inayofaa. Hata hivyo, mafundisho ya dini peke yake hayatoshi kutokomeza vitendo vya rushwa na badala yake sheria kali zichukuliwe dhidi ya waliohusika na wanaoendelea kushiriki katika kutoa na kupokea rushwa.

### 5.1.7 Kandoro na Dhuluma katika Jamii

Dhuluma ni kitendo cha kuchukua mali ya mtu na kujinufaisha nayo bila ya kumpatia mwenye mali sehemu ya faida hiyo na kisha kuididimiza mali yote. Dhuluma katika siasa imesambaa tena kwa kiasi kikubwa. Tunawaona wabunge kwa mfano, wananadi sera kwamba, wakipatiwa nafasi za ubunge watatekeleza ahadi

walizotoa kwa wananchi. Hata hivyo, hali huwa si hivyo punde tu wachaguliwapo. Wabunge wengi wanapochaguliwa huhama kutoka katika majimbo yao na kuhamia mijini hasa Dar es Salaam. Madaso (2009) kama anavyonukuliwa na Samwel (2012) anasema:

> *Wanasiasa walio wengi ndoto zao si kuona majimbo yao yamepata maji, shule na kadhalika, bali ni kuona wanapata nafasi walizozitaka ili waishi maisha bora.*

Naye Kandoro hayuko nyuma katika kuonesha namna dhuluma inavyojitokeza katika jamii za Kiafrika. Kwa mfano, katika shairi la *dhuluma* anaeleza:

> *Roho zetu zatuuma, mambo mawi kutendewa,*
> *Yote Afrika nzima, hatuishi kuonewa,*
> *Afrika inasema, uhuru unatakiwa,*
> *Twachoka kudhulumiwa, roho zetu zatuuma.*

Hapa tunaoneshwa namna Afrika inavyodhulumiwa rasilimali zake na watu wa mataifa ya nje na wale wa ndani pia. Watu wa mataifa ya nje wanaozungumzwa hapa ni wawekezaji hasa wale waliowekeza katika sekta ya madini. Wadhulumaji wa ndani ni wale wanaoshirikiana nao aidha katika kusaini mikataba na kadhalika nao pia wananyonya rasilimali za taifa kwa masilahi yao wenyewe. Dhuluma ni jambo baya na hakuna mtu anayekubali kudhulumiwa kirahisi rahisi tu. Kandoro anashadidia hoja hii pale anaposema kwamba:

> *Nani mpenda dhuluma, apenda kudhulumiwa*
> *Nani mpenda kutuma, akapenda kutumiwa*
> *Hima yatupeni nyuma, msopenda kufanyiwa*
> *Twachoka kudhulumiwa, roho zetu zatuuma.*

Hapa Kandoro anaonesha kwamba, hakuna mtu anayependa kudhulumiwa bali wapo watu wanaopenda kudhulumu rasilimali za watu wengine. Vilevile, hakuna mtu anayependa kutumiwa. Bali yeye hupenda kutumia watu wengine kwa masilahi binafsi. Tukirejelea mfano wa wabunge na viongozi wengine kwa kisiasa unaweza kuona namna wanavyowatumia wananchi katika kujinufaisha wao binafsi na huku wakikataa katakata kutumika katika kuwasaidia wananchi kujikomboa kutoka katika umasikini. Tunasema wanatumia wananchi kujinufaisha kwa sababu ni wananchi ambao ndio huwachagua viongozi hao ambao hunufaika kutokana na kura za wananchi hali ya kuwa wananchi hawanufaiki kutokana na kura walizopiga. Kandoro anamalizia kwa kituo kisemacho: *twachoka kudhulumiwa, roho zetu zatuuma*. Kwa maoni yetu tunamini kwamba, haitoshi tu kusema kwamba “tumechoka” kwa maneno tu bila kutumia vitendo na hapa Kandoro anawataka wananchi kuonesha kwa vitendo kwamba, kweli wamechoka kudhulumiwa. Hii itaonekana kwa wao (wananchi) kuacha kuwachagua viongozi ambao ni wadhulumaji na kuwapa uongozi watu waaminifu na wenye uchungu na maendeleo ya umma. Hata hivyo, hali haiko hivyo kwani katika sehemu nyingi bado wanawachagua viongozi walewale wasiosaidia kuleta maendeleo katika jamii. Hapa jamii inapaswa kubadilika kama kweli imechoka kuonewa kama anavyosema Kandoro (1978) kuwa:

*Tuwapinge mabeberu,*
*Wasifike kutudhuru,*
*Tuwanyime na nafasi,*
*Ya kutugawanya sisi,*
*Wajilaumu wenyewe,*
*Waingiwe na kiwewe,*
*Tumechoka kuonewa,*
*Tumechoka kuchezewa*.

Neno mabeberu hapa halina maana ya wageni peke yake bali hata viongozi ambao tunao wasiojali masilahi ya taifa nao pia ni mabeberu kwa sababu wanajali masilahi yao tu. Iwapo tutafanikisha kuwapinga mabeberu basi Kandoro anasema kwamba itasaidia kuwafanya:

*Wajione wamekosa*
*Waanze kujitakasa*
*Ilazimike lazimu*
*Wenyewe watuheshimu*
*Wauwache ukorofi*
*Kutughilibu kwa tofi*
*Tumechoka kuonewa*
*Tumechoka kuechezea.*

Ili kufanikisha azma hii ni lazima mapinduzi makubwa ya kifikira yafanyike kwa wananchi vinginevyo mambo yataendelea kuwa hivyohivyo kila siku iendayo kwa Mungu. Baada ya kutoa maelezo marefu juu ya dhuluma sasa tuielezee dhamira ya umasikini kama inavyojitokeza katika ushairi wa Kandoro. Dhamira hiyo inajitokeza kama ifuatavyo:

### 5.1.8 Kandoro na Umasikini katika Jamii

Umasikini ni moja kati ya maadui watatu wa maendeleo ya taifa letu na mataifa mengi ya bara la Afrika. Maadui hawa walitangazwa na raisi wa Kwanza wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mara tu baada ya kupata Uhuru. Maadui wengine wawili ni ujinga na maradhi (Kandoro, 1978). Serikali zote nne zilizopata kuitawala Tanganyika na baadaye Tanzania zimeandaa na kutekeleza sera na mikakati mbalimbali ya kuutokomeza umasikini nchini. Mkakati maarufu unaotekelezwa hivi sasa ni ule unaoitwa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kutokomeza Umasikini Tanzania (MKUKUTA). Mkakati huu umeainisha maeneo kama vile afya, elimu, maji na barabara kama maeneo muhimu

yanayohitaji kuimarishwa ili kufanikisha jitihada za kuutokomeza umasikini. Kandoro kama walivyo washairi wengine ametunga mashairi kadhaa kuwahamasisha wananchi kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha kwamba mikakati kama vile MKUKUTA inatekelezwa kama inavyopasa. Katika shairi lake la *Tuupinge Usikini* anasema:

*Sisi ni tai turuke, tusigaragare chini,*
*Tukaapo tunyanyuke, tusiikae vitini,*
*Lengo letu tuinuke, tutambuke usikini,*
*Tuupinge uskini, ndwele ujinga vitoke.*

Hapa mshairi anawataka wananchi kujifunga mkanda katika kufanya kazi kwa bidii ili kupambana na umasikini. Mshairi anawataka wananchi kuachana na starehe na shughuli zisizo na tija na badala yake wajikite katika kufanya shughuli za uzalishaji mali. Ndiyo maana anasema: *Tukaapo tunyanyuke; tusikae vitini.* Hii haina maana mtu asipate muda wa kukaa na kupumzika la hasha, bali asikae akabweteka. Hii itasaidia kuundoa umasikini kama anavyosema Kandoro: *Lengo letu tuinuke tutambuke uskini.* Katika ubeti mwingine Kandoro anaeleza kwamba:

*Tuupinge upingike, bila mzaha nchini,*
*Wenyewe tushughulike, na majembe mkononi,*
*Na mavuno yavunike, yajae tele ghalani,*
*Tuupinge uskini, ndwele ujinga vitoke.*

Katika ubeti huu Kandoro anawataka wananchi wasikate tamaa katika harakati za kupambana na umasikini. Anayasema haya kwa sababu anatambua kwamba, kupambana na umasikini si kazi rahisi. *Tuupinge upingike, bila mzaha nchini,* msitari huu unaonesha kwamba katika kupambana na umasikini kuna vikwazo vingi lakini vikwazo hivyo visiwafanye wananchi kukata tamaa. Kwa mfano, mshairi anaeleza kwamba; *wenyewe tushughulike, na majembe mkononi* akimaanisha kwamba Kilimo

ndio tegemo la wananchi wengi katika kupambana na umasikini. Hivyo basi, katika kilimo kuna hima mbalimbali kama vile; uhaba wa mvua na wadudu waharibifu wa mazao. Pamoja na kuwepo kwa hima hizi Kandoro anawataka wananchi wasikate tamaa na badala yake waongeze juhudi katika kupambana na umasikini. Anaendelea kueleza kwamba kama wananchi wataongeza juhudi katika uzalishaji mali basi hili lifuatalo litawezakana.

*Usikini utoweke, ukae mbali pembeni,*
*Na sisi tutaoneka, tunawirike mwilini,*
*Nchi zetu zinemeke, ziwe na matumaini,*
*Tuupinge usikini, ndwele ujinga vitoke.*

Maono haya ya Kandoro yataweza kufanikiwa pale tu wananchi watakapojibidisha katika kufanya kazi kwa ustadi na umakini mkubwa. Hata hivyo, Kandoro amesahau kwamba, kujibidisha kwa wananchi peke yake katika kilimo hakuwezi kutokomeza umasikini kama serikali na wadau wengine hawatatekeleza wajibu wao kama ipasavyo. Kimsingi, ni jukumu na wajibu wa serikali kuhakikisha kwamba, inawashirikisha wananchi wake katika uaandaji wa sera na mikakati mbalimbali ya utokomezaji wa umasikini na masuala mengine. Kwa mfano, katika uandaaji na uundaji wa MKUKUTA ushirikishwaji wa wananchi haukufanywa kama inavyopaswa. Badala yake ni watu wachache tu walishirikishwa katika uundwaji wa mkakati huo. Hali hii inaufanya mkakati kutotekelezwa kwa kiwango kilichokusudiwa kwa sababu wananchi walio wengi hawaelewi chochote kuhusu mkakati huo. Katika maeneo ambayo ushirikishwaji wa wananchi umefanyika vizuri basi utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo katika maeneo hayo umefanikiwa

kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano; tukitazama maeneo kama ya ujenzi wa sekondri za kata yamefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa sababu wananchi wamekuwa wakishirikishwa katika hatua zote za uandaaji na utekelezaji wa mradi huo. Wananchi walishirikishwa katika kuamua ni wapi shule ijengwe, kila kaya ichangie shilingi ngapi au mali yenye thamani gani, shule ikishajengwa ipewe jina gani na kadhalika. Mambo yote haya kufanywa na wananchi, huwafanya kuona mradi kuwa ni wa kwao na wao ndio wanaopaswa kuutekeleza. Kwa msingi huu basi, ni dhahiri kwamba, ushirikishwaji wa wananchi katika hatua za awali za uaandaji wa mradi na utekelezaji wake ni jambo la muhimu sana katika mafanikio ya mradi wenyewe. Baada ya maelezo haya tutazame masuala ya Demokrasia kama yanavyoelezwa na Kandoro.

### 5.1.9 Kandoro na Demokrasia

Demokrasia ni dhana pana inayoangaliwa katika miktadha ya kiliberali na kijamii. Wanauliberali wanaieleza demokrasia kama ni uhuru alionao mtu mmojammoja katika jamii wa kufanya chochote atakacho bila kuvunja sheria za nchi. Vilevile, anao uhuru na haki ya kushirikishwa katika maamuzi mbalimbali yahusuyo maendeleo yake binafsi na ya taifa lake kwa ujumla (Mpangala, 1977; 2004).

Wana wa Ujamaa kwa upande wao wanaieleza demokrasia, kuwa ni mfumo wa maisha ambao umejengewa katika misingi halisi ya maisha ya Mwafrika. Kwamba, demokrasia ni lazima iegemee katika matakwa ya walio wengi miongoni mwa wanajamii na sio matajiri wachache (Nyerere, 1963). Kandoro ameizungumzia demokrasia ya Kijamaa kwa kiasi kikubwa katika kazi zake mbalimbali za ushairi alizopata kuandika. Kwa mfano: Mnamo mwaka 1958 Chama cha TANU kiliafiki

sheria ya Kikoloni iliyoelekeza kwamba, kila mwananchi anatakiwa kupiga kura tatu kwa wagombea wa nafasi mbalimbali za Uongozi. Kura moja kwa Mzungu, nyingine kwa Muhindi na nyingine kwa Mwafrika. Kandoro ambaye hakuhudhuria mkutano huo, alipopewa taarifa hizo alikasirika sana kwa kuwa yeye aliliona hili kama ni changamoto ya kurudisha nyuma mapambano dhidi ya kudai uhuru (Kitogo, 2002). Katika shairi, *Kura Tatu*, anaeleza kwamba:

*Kulazimishwa watu, shauri wasilotaka,*
*Hiyo ni ajabu kwetu, twajifumbata twacheka,*
*Fakiri haneni kitu, mbele ya wenye madaraka,*
*Hatutaki Tanganyika, kura ya watu watatu.*

Hapa Kandoro anaonesha kwamba, misingi ya demokrasia ilikiukwa katika kuwataka wananchi kupiga kura tatu badala ya kura moja. Hii si demokrasia kwa sababu ya *Kulazimishwa watu, shauri wasilotaka*. Wananchi wanapoamua jambo kwa utashi wao bila ya kulazimishwa wala kushurutishwa hiyo ndiyo demokrasia ya kweli.

Katika ubeti huo hapo juu Kandoro anaibua sula la msingi kuhusiana na masula ya demokrasia. Anasema: *Fakiri haneni kitu, mbele ya wenye madaraka*. Hii inaonesha kwamba, demokrasia ya kweli haiwezi kupatikana kwa watu masikini na badala yake ni wale matajiri tu ndio wanaotawala, kuamua na kupanga kila jambo kwa namna wanavyotaka wao. Kwa hili tunaungana mkono na Kandoro kwa asilia mia kwa mia. Hata katika kugombea nafasi ya uongozi tu, mfano; ubunge, si rahisi kukuta mtu masikini anashinda kiti hicho dhidi ya tajiri mwenye uwezo mkubwa wa

mali na fedha. Hata hivyo, pamoja na umasikini wa wananchi Kandoro aliona kwamba ni wajibu wa kila mwananchi kuitafuta demokrasia na kuhakikisha kwamba inatekelezwa. Anasema:

*Kura moja kwa watatu, watu gani wametaka,*
*Itajwe kura kwa mtu, kwa moja tunataka,*
*Ili tuchague watu, kwa kura isiyo mipaka.*
*Hatutaki Tanganyika, kura ya watu watatu.*

Hapa Kandoro anaenesha kuwa, kuidai demokrasia ya kweli ambapo mtu mmoja atapiga kura kwa mgombea mmoja anayemtaka kulingana na sifa na vigezo vyake. Wakoloni walifahamu fika kwamba, Watanganyika ni wengi kuliko Wazungu na Wahindi na iwapo kila mtu atapiga kura moja ni dhahiri Wagombea wa Kizungu na Kihindi hawatashinda katika chaguzi. Kwa msingi huo basi, wakaamua kutumia mbinu ya kura tatu ili Wagombea wa Kizungu na Kihindi nao waweze kushinda chaguzi dhidi ya Wagombea wa Kiafrika.

Katika demokrasia ya kweli watu wote hushirikiana na kujaliana hata kama wapo wachache ambao pengine kwa njia moja ama nyingine hawakubaliani na mtazamo ama msimamo wa wengi. Hii inatokana na msemo kwamba: *Majority rule, minority right* (Mpangala, 2004). Kandoro alilifahamu hili na alipoona wakoloni wanachelewesha kutoa uhuru wakihofia pengine watabaguliwa na utawala mpya wa Tanganyika aliwatungia ubeti kuwataarifu kwamba, wasihofu wao watoe tu uhuru halafu haki zao na za Watanganyika zitaheshimiwa. Katika shairi lake la *Kura Tatu* anasema:

*Twadai tarehe yetu, kutawala Tanganyika,*
*Twaomba uhuru wetu, ndio tunaoutaka,*
*Haki zenu na za kwetu, tutalinda bila shaka*
*Hatutaki Tanganyika, Kura ya watu watatu.*

Katika msitari wa tatu mshairi anasema, *Haki zenu na za kwetu, tutalinda bila shaka*. Hii ni kuwahakikishia wakoloni kwamba, katika demokrasia ya kweli watu wote hupewa haki zao stahili bila ubaguzi wowote kama wao walivyokuwa wakiwatendea Watanganyika. Hii kwa hakika ndio demokrasia ya kweli.

Vilevile, katika kuonesha kwamba, Kandoro alikuwa ni muumini wa demokrasia ya kweli, utaona utenzi wake wa maneno katika kudai uhuru. Anasema: *Twaomba uhuru wetu, ndio tunaoutaka.* Neno "Twaomba" katika msitari huu ni neno la kistaarabu na ni nadra kutumiwa na wanasiasa wa siku hizi. Mkoloni aliwatesa wananchi wa Tanganyika lakini wanapodai haki yao wanatumia maneno ya staha na heshima. Hali hii iliwafanya kushangaa na kujiuliza maswali mengi kwamba inakuwaje mtu anadai haki yake halafu anatumia neno "kuomba au naomba"? Bila shaka huu ndio utamaduni wa Mtanganyika ambao ni tofauti kabisa hata na wa nchi za jirani kama Kenya. Wananchi na Wanasiasa wa Kenya kwa mfano; hutumia neno "nataka" kitu fulani sio "naomba" kitu fulani. Hata hivyo, viongozi wa kisiasa hasa wa vyama vya upinzani wameacha kabisa kutumia neno "naomba" na badala yake wanatumia "nataka". Akizungumza katika mkutano wa hadhara Kiongozi mmoja wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kuhusu kukamatwa na kufikisha katika vyombo vya sheria mafisadi wote waliotafuna fedha za serikali anasema:

> *Tunaitaka serikali ya Rais Kikwete wakamate mafisadi wote na kuhakikisha kwamba sheria inachukua mkondo wake. Tunasema tunaitaka na sio kuiomba serikali kufanya hivyo kwa sababu hizi sio enzi za kuombana. Tukiendelea kuwaomba kama tulivyokuwa tunafanya huko nyuma wanatuona*

> *wapuuzi na wanaendelea kulindana. Tunawapa muda, wasipofanya hivyo tutaingia barabarani.*

Dondoo hili linaonesha kwamba, siasa za siku hizi zinaanza kubadili utamaduni wa Mtanzania. Hili linaonekana hata katika kampeni za kisiasa ambapo baadhi ya wagombea hutumia lugha za matusi na udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya wagombea wengine. Baada ya kutoa maelezo ya kina dhidi ya dhumuni mahususi la kwanza sasa tuone hitimishi lake kama ifuatavyo:

### 5.1.10 Hitimishi

Katika sehemu hii tumeonesha namna Kandoro alivyokuwa msitari wa mbele katika kupigania uhuru wa Tanganyika. Alifanya hivyo kwa kuibua madhila na maovu ya wakoloni dhidi ya Watanganyika kama njia ya kuwapa wananchi hamasa ya kupambana na Wakoloni katika kudai uhuru wao. Katika kuonesha hilo sura hii imemtaja Kandoro na harakati za kudai uhuru kama; Kandoro mhamasishaji wa kisiasa, Kandoro na masuala ya elimu, Kandoro na masuala ya haki, Kandoro na Umiliki wa Ardhi, Kandoro na Suala la Rushwa, Kandoro na dhuluma katika jamii, Kandoro na Umasikini na Kandoro na demokrasia. Kandoro aliyazungumza mambo haya katika kipindi cha ukoloni ili serikali ya Kikoloni iliyoshindwa kuyatafutia ufumbuzi iondolewe na serikali mpya ya Wazawa itakapokabidhiwa nchi waweze kutekeleza kama inavyopaswa. Harakati za Kandoro pamoja na wanaharakati wengine zilisaidia kwa kiasi kikubwa kupatikana kwa uhuru mnamo mwaka 1961 tarehe 9 mwezi Disemba. Nini mwendelezo wa Kandoro katika ushairi wake katika kipindi cha uhuru? Hili ndilo suala linalowasilishwa katika sehemu inayofuata.

## 5.2 Ushairi wa Kandoro Katika Kipindi cha Uhuru

### 5.2.1 Utangulizi

Katika sehemu hii tunaonesha mawazo ya Kandoro juu ya nini kifanyike ili vikwazo vya maendeleo vilivyowekwa na mkoloni viweze kutatuliwa. Kandoro anaonesha kuwa, ana ari kubwa ya kuhakikisha kwamba, wananchi wote wanapata maendeleo na wanakuwa na maisha mazuri. Maendeleo haya yatapatikana iwapo tu kila mwananchi atafanya kazi kwa juhudi na maarifa tena wa kujituma kikamilifu. Sehemu hii inaeleza kwa undani mambo ambayo yanapaswa kutekelezwa na kila mwananchi ili kujiletea maendeleo endelevu kama yanavyojitokeza katika ushairi wa Kandoro. Mambo hayo ni haya yafuatayo:

### 5.2.2 Kufanya kazi kwa Bidii

Baada ya kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika washairi mbalimbali waliandika mashairi yao kwa nia ya kuhamasisha ujenzi wa jamii mpya yenye kuzingatia misingi ya usawa na haki ili kujiletea maendeleo endelevu. Miongoni mwa mambo waliyohamasisha kufanywa na wananchi ni kufanya kazi kwa bidii. Kufanya kazi kwa bidii ya kujituma ndio njia muafaka ya kuleta maendeleo katika jamii. Katika shairi lake la *Tumshukuru Manani* anasema:

*Uhuru tumejaliwa, sasa na tufanye nini,*
*Wananchi twaambiwa, tufanye kazi nchini,*
*Ardhi kufukuliwa, iwe kazi namba wani,*
*Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa*.

Hapa Kandoro anaeleza kwamba, Uhuru umekwishapatikana na kinachotakiwa ni kuchapa kazi kwa bidii na si vinginevyo. Baadhi ya wananchi walidhani kwamba, uhuru ukipatikana basi kila kitu watakipata tu hata bila ya kufanya kazi. Kandoro

alilitambua hilo na hapa anawataka wananchi kufanya kazi kwa bidii ili kuleta maendeleo nchini. Kazi kubwa anayoinadi bwana Kandoro ni kilimo katika mstari wa tatu wa ubeti hapo juu anasema kwamba: *Ardhi kufukuliwa, iwe kazi namba wani*. Neno *kufukuliwa* hapa limetumika kiishara kuashiria kilimo ambacho ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Tanganyika katika enzi hizo na hata leo.

Kandoro anaeleza kwamba, katika enzi hizi za uhuru wananchi wanatakiwa wafanye kazi kwa bidii na katu wasibweteke kufikiri kwamba kuna mtu kutoka sehemu nyingine atakayewaletea maendeleo. Anaendelea kuonya kwamba, iwapo wananchi na serikali yaoa watakaa chini na kuanza kutegemea misaada ya wahisani badala ya kufanya kazi ni dhahiri kwamba, nchi itarudi katika mikono ya Wakoloni. Anasema:

*Ijapo tukitolewa, fedha kutoka London,*
*Ya kwamba tuliletewa, na viongozi nchini,*
*Na iwapo mtalewa, mtarudi utumwani,*
*Tumshukuru maanani, uhuru tumejaliwa.*

Kandoro anawataka wananchi wasitazamie kupata fedha kutoka “London” akimaanisha wahisani wa maendeleo kwa kuwa hiyo ni hatari ambayo itarudisha nyuma maendeleo ya nchi na kuufanya uhuru uliopatikana kuwa hauna maana yoyote. Katika msitari wa tatu anatumia neno “mtalewa” kumaanisha kuridhika na utegemezi wa misaada kutoka nje basi kamwe maendeleo hayatapatikana.

Katika msisitizo wa Kilimo Kandoro anawataka wananchi kulima mazao ya aina mbalimbali ili kupata chakula cha kutosha na pia kuuza kile cha ziada ili waweze kumudu gharama za mahitaji mengine kama nguo na malazi. Katika shairi *Rudi Haraka* anasema:

*Juma njoo nikutume, nenda upesi shambani,*

*Ufike uchume kunde, usiyachume mahindi,*
*Maagizo yashike, uzivunje mbaazi.*
*Rudi haraka haraka, njiani usikawie.*

Katika ubeti huu mshairi anataja kunde, mahindi na mbaazi kama mfano wa mazao ambayo wananchi wanapaswa kuyalima ili kujiletea maendeleo. Katika shairi lingine anasema:

*Limeni fedha mchume, muifanye mipango*
*Shuleni wana wasome, wafikie kiwango*
*Kirudi nchini watuone, yamekwisha masimango*
*Uhuru una kiungo, wanyonge kufuta kodi.*

Iwapo wananchi watajibidisha katika kilimo ni dhahiri kwamba, watapata fedha kwa ajili ya kufanyia shughuli mbalimbali za kimaendeleo kama vile kuwasomesha watoto wao. Katika ubeti huu, pia Kandoro anazungumzia suala la mipango. Anawataka wananchi baada ya kufanya Kilimo, kuvuna mazao yao na kuuza baadhi wakapata fedha basi fedha hizo wasizitumie kibubusa na badala yake wazifanyie mipango. Mipango hiyo ndiyo itakuwa dira na mwelekeo wao katika mafanikio. Mipango hii haitakiwi kuishia katika fedha peke yake bali katika masuala mengine ya kijamii na kiutamaduni pia. Huu ndio wasia wa Kandoro kwa wananchi, ambao ukifuatwa vizuri utaleta maendeleo kwa wananchi na nchi nzima kwa ujumla.

### 5.2.3 Kandoro na Uongozi wa Nchi

Baada ya kupatikana kwa uhuru Tanganyika ilihitaji kuwa na viongozi imara na shupavu ambao watafanikisha jitihada za kuwaondolea wananchi adha walizoachiwa na wakoloni. Uongozi imara ulitegemewa kuanzia kwa kiongozi mkuu wa nchi yaani

Rais na kisha kufuatiwa na mawaziri. Kandoro kupitia shairi *Nyerere Pokea hicho* anaandika hivi:

*Linda sasa nchi yako, pokea uizatiti*
*Ufute macho yako, uketi mshike kiti*
*Na Mawaziri wenzako, mshike nchi kwa dhati*
*Nyerere kalia kiti, uichunge nchi yako.*

Hapa Kandoro anamtaka Mwalimu Nyerere kuwa kiongozi makini katika kuiongoza nchi ya Tanganyika. Katika msitari wa kwanza anasema: *Linda sasa nchi yako, pokea uizatiti*. Msitari huu unamtaka mwalimu Nyerere kuwatumikia wananchi wake kwa moyo wake wote baada ya kuipokea nchi kutoka kwa wakoloni. Inafahamika kwamba, Nyerere alipokea nchi kutoka kwa wakoloni ikiwa haina chochote zaidi ya umasikini uliokithiri. Neno "Uizatiti" katika msitari wa kwanza linamtaka Nyerere kuuondoa umasikini katika jamii kwa njia yoyote ile iwayo tena kwa uharaka zaidi. Vile vile, Kandoro anamtaka Nyerere na Mawaziri wake wawe ni viongozi wema wasiopenda rushwa na dhuluma. Hili linaonekana pale anaposema: *Na Mawaziri wenzako, mshike nchi kwa dhati*.

Kwa upande mwingine Kandoro anauona uongozi wa nchi changa iliyotoka kupata uhuru kama mzigo mkubwa na mzito sana. Kupitia shairi *Kujitawala Kugumu* anasema:

*Ni mume si mwanamke, aliniambia fahamu*
*Mtawaliwa mcheke, cheko ya kumlaumu,*
*Na tena yapambazuke, kujitawala, kugumu*
*Kujitawala kugumu, tujikongoje tufike.*

Katika ubeti huu mshairi anaonesha kuwa kukubali kutawaliwa ni suala baya. Hivyo ni wajibu wa kila mtu kuhakikisha kwamba, anapambana asitawaliwe bali ajitawale

mwenyewe. Hata hivyo, baada ya hapo anapaswa pia afahamu kwamba kujitawala ni kazi ngumu si rahisi kama inavyoweza kufikiriwa. Hivyo basi, Nyerere anafahamishwa na Kandoro aelewe kwamba, kujitawala si kazi rahisi bali inahitaji uvumilivu wa hali ya juu pamoja na busara isiyo na kifani. Vilevile, wananchi nao wanaelezwa watambue kwamba, kujitawala ni kugumu na wanapaswa kuwa wavumilivu wakati serikali ikifanya jitihada za kuleta maendeleo nchini. Pamoja kwamba kujitawala ni kugumu, mwishoni mwa ubeti, Kandoro anatoa tumaini kwamba: *tujikongoje tufike*. Hii ina maana kwamba, wananchi pamoja na viongozi wao wakishirikiana pamoja, mafanikio yatapatikana kwa urahisi zaidi. Anaendelea kuwataka wananchi wafanye yafuatayo:

*Utawala tuushike, una mambo maalumu*
*Yafaa twerevuke, tujinyanyue makamu,*
*Sherehe tuziepuke, vinanda na densi tamu*.

Kandoro anaonya kuwa tabia na vitendo vya anasa visifanywe na wananchi na badala yake wajibidishe katika kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili kuisaidia serikali yao katika kuletea nchi na wananchi wake maendeleo endelevu.

### 5.2.4 Kandoro na Masuala ya Kijinsia

Mwanamke amechukuliwa kama kiumbe duni na asiye na uwezo wa kutoa mawazo mazuri ya kusaidia mafanikio kama ilivyo kwa wanaume kwa muda mrefu sasa. Mwanamke amekuwa akihusishwa na shughuli za ndani huku masuala kama ya kupigania haki na uhuru kuonekana kuwa ni ya mwanaume na si mwanamke. Katika shairi la *Nyerere Pokea hicho* anasema:

*Wanaume twapiga heko, mbele hawaendi mabinti*
*Ile sheria ya mboko, mheshimiwa mdhibiti,*
*Inatakiwa kwako, sasa twaijenga nchi,*
*Nyerere kalia kiti, uichunge nchi yako.*

Katika ubeti huu Kandoro anaonekana kuwadharau wanawake kuwa hawawezi kusimama msitari wa mbele katika kudai haki zao na kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo. Mawazo haya ya Kandoro hayana mashiko yoyote kwa kuwa si kweli kwamba, wanawake hawako au hawawezi kukaa msitari wa mbele katika kupigania haki na kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo. Waandishi kama Shaaban Robert wamemchora mwanamke kama kiumbe muhimu katika mafanikio ya mwanaume. Tendi mbalimbali kama ulivyo ule wa *Fumo Lyongo* unaonesha kwamba, shujaa wa Kiafrika hakuweza kufanikiwa katika ushujaa wake bila kupata msaada na mwongozo kutoka kwa mwanamke. Katika kuendelea kuonesha namna alivyo na mtazamo hasi kuhusu wanawake, Kandoro anasema:

*Ni mume si mwanamke, aliniambia fahamu*
*Mtawaliwa mcheke, cheko ya kumlaumu,*
*Na tena yapambazuke, kujitawala kugumu*
*Kujitawala kugumu, tujikongoje tufike.*

Kandoro anaonesha kwamba, mwanamke ni kiumbe anayependa kutawaliwa na mwanaume kamwe hapendi kutawaliwa. Haya tunayapata katika ubeti wa shairi hapo juu kwamba ni mwanaume na si mwanamke aliyemweleza Kandoro kwamba mtu anayetawaliwa anatakiwa achekwe kicheko cha kumlaumu. Kwa maoni yetu wapo wanawake wengi tu ambao hupinga kutawaliwa na hufanya harakati mbalimbali katika kujikomboa. Mfano wa wanawake hao ni akina bibi Titi Mohamed na wengineo. Kupitia beti hizi za ushairi Kandoro anaonekana kutowatendea haki

wanawake kutokana na kuwashusha hadhi kwamba ni wao ni watu wa nyuma duniani. Mawazo haya ya Kandoro yanatokana na mfumo dume ambao umeitawala jamii katika historia ya maendeleo ya mwanadamu tangu karne na karne. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni yameibuka makundi na taasisi mbalimbali zinazotetea usawa wa kijinsia katika jamii. Hii imesaidia kupunguza kasi ya mfumo dume katika jamii ambapo mpaka sasa wapo wanawake ambao wameshika madaraka makubwa katika nchi na mashirika makubwa duniani. Kwa msingi huu hakuna sababu ya kuendelea kuwadharau wanawake kuwa ni duni mbele ya wanaume kwani wapo pia baadhi ya wanawake ambao hutekeleza majukumu yao vizuri kuliko hata wanaume. Hii yote inaonesha kwamba, mwanamke na mwanaume wote ni sawa ila tu fursa nyingi huchukuliwa na wanaume kuliko wanawake ndio maana wanawake wanaonekana kama hawana uwezo wa kufanya mambo kama wafanyavyo wanaume. Hata hivyo, pale wanawake wanapopata fursa kwa mfano, bungeni tunaona namna wanavyoichachafya serikali pale inapolegalega katika utekelezaji wa sera za maendeleo. Huu ni uthibitisho tosha kwamba mwanamke na mwanaume wote ni sawa.

### 5.2.5 Kandoro na Kuweka Akiba

Waswahili wana methali yao isemayo akiba haiozi. Kandoro alifanya kazi kubwa ya kuwahimiza wananchi kuhakikisha kwamba wanajiwekea akiba ya fedha katika benki ili wazitumie baadaye katika kujiletea maendeleo. Ilizoeleka kwa wananchi wengi kuficha fedha zao majumbani mwao badala ya kuweka katika benki. Kupitia shairi lake la *Mwalimu katukataza* anasema:

*Fedha ziweke benkini, hazina ya mwanga,*
*Ziandikwe kitabuni, na cheki wapewa kwanza,*

*Zapokewa kwa saini, faida zajiongeza,*
*Mwalimu katukataza, kuzizika fedha chini*.

Hapa tunaoneshwa kwamba, iwapo wananchi wote watawekeza fedha zao katika benki basi taifa linaweza kupiga hatua kubwa kimaendeleo. Tunasema hivi kwa sababu fedha hizo zitatumika kama sehemu ya mikopo kwa wananchi wanaojishughulisha na biashara, kilimo pamoja na ujenzi wa nyumba za kisasa. Vilevile, serkali itatumia fedha hizo katika kutolea huduma mbalimbali kama vile za afya, maji, barabara, umeme na pembejeo za kilimo. Haya yote kwa pamoja yataharakisha maendeleo kwa taifa.

Vilevile, katika ubeti huu Kandoro anaonesha kwamba mtu anapohifadhi fedha zake katika benki basi zinakuwa katika mikono salama. Mwananchi anapoweka fedha zake benkini anakuwa na uhakika kwamba, zipo katika mikono salama na haziwezi kuibwa ama kupotea kama akihifadhi fedha hizo nyumbani kwake. Fedha zikihifadhiwa nyumbani zinaweza kuteketea kwa moto na mwananchi akaendelea kuwa mtu masikini kupindukia.

Si hivyo tu bali pia, mshairi anatoa elimu kwa wananchi juu ya namna watakavyohudumiwa katika benki ili kuhakikisha usalama wa fedha zao unapatikana. Kwanza mwananchi anatakiwa afahamu kwamba, anapopeleka fedha zake benki ni lazima ziandikwe katika kitabu na kisha apatiwe cheki. Baada ya hapo anapotoa fedha ni lazima asaini katika kitabu ama karatasi inayohusika ndiyo fedha zitolewe. Mambo haya yote yanahakikisha usalama wa fedha za mwananchi

atakapozipeleka benki. Pia Kandoro anaeleza faida nyingine ya kuweka fedha benki kuwa ni kupewa riba ambayo huongeza kiasi cha fedha katika fedha zilizowekwa na mwananchi.

Mawazo haya ya Kandoro ni muhimu na tunakubaliana nayo kwa asilimia mia kwa mia kwa msingi kwamba; ujenzi wa jamii mpya ya Tanganyika ulihitaji fedha za kutosha kwa kuwa nchi iliyokabidhiwa na wakoloni kwa viongozi wa Tanganyika huru ilikuwa ni masikini sana. Njia pekee ya kupata fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ilikuwa ni kukopa katika benki zilizokuwapo nchini wakati huo. Kama hivyo ndivyo, serikali ingekopa nini hali ya kuwa wananchi wanahifadhi fedha zao chini ya ardhi nyumbani na benki zikikosa fedha? Kampeni ya kuwahamasisha wananchi kubadili namna ya kutunza fedha zao kwa kuzipeleka benki ni njia muafaka iliyosaidia jitihada za serkali za kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma bora na stahiki.

### 5.2.6 Kandoro na Maisha Bora

Uhuru ulipopatikana mnamo mwaka 1961 wananchi walifurahi wakiamini kwamba, kila moja atakuwa na maisha bora. Maisha bora hapa yalifasiliwa kama upatikanaji wa huduma muhimu za kuendesha maisha ya kila siku kwa wananchi wote bila ubaguzi wa aina yoyote kama ilivyokuwa katika kipindi cha Wakoloni. Bila shaka hili ndilo lilikuwa tegemeo la viongozi wapigania uhuru. Kandoro hakuwa nyuma katika kukampenia suala hili pale anaposema katika shairi lake la "*Soma sana kwa Bidii* (1966:70) kuwa:

> *Ujenge maisha yako, na uyajengee kwa dhihii*
> *Soma bila mnung'uniko, usome ukifurahi,*
> *Shika kwa mikono yako, soma ukitalii,*

*Soma sana kwa bidii, ujenge maisha yako*.

Hapa Kandoro anaonesha kwamba, ili mwananchi aweze kujenga maisha yake kwa namna inayopasa basi ni lazima apate elimu ndiyo itakuwa mkombozi wake. Kutafuta elimu hakuna rika ndio maana Kandoro hakutaja kundi fulani maalumu ndio linalopaswa kusoma bali ameeleza tu kwa ujumla, kwamba kusoma ni wajibu kwa kila mtu anayetaka kujenga maisha yake. Ni elimu bora pekee itakayowezesha kila mtu kuweza kufanya shughuli zake kwa namna inayofaa ili aweze kupata tija na kisha kufanikisha ujenzi wa maisha yake.

Kimsingi, ili kuhakikisha kwamba, wananchi wote wanapata elimu, ili waweze kujenga maisha yao serikali ilianzisha elimu ya watu wazima. Kupitia utaratibu huu, watu wazima ambao hawakupata fursa ya kusoma katika kipindi cha ukoloni walipata nafasi ya kusoma na kisha kuendelea na shughuli zao. Watu wazima walijifunza kusoma na kuandika pamoja na stadi mbalimbali za kazi kama kilimo, ufugaji, ususi, ufinyanzi na kadhalika. Kupitia aina hii ya elimu, taifa liliweza kufuta ujinga kwa kiwango kikubwa.

Kwa upande wa elimu ya msingi ambayo ilifanywa kuwa ni ya lazima kwa kila mtoto aliyefikisha umri wa kuanza shule ilitolewa bure kwa watoto wote bila kujali rangi, kabila, dini wala jinsia. Serikali pia ilihakikisha kwamba, shule zote zinapata miundombinu muhimu ili elimu itakayotolewa iwe ni bora na yenye manufaa kwa maisha ya wananchi wote. Kandoro anasema: *Soma bila nung'uniko, usome ukifurahi* akiwa na maana kwamba, serikali imeshaandaa mazingira mazuri ya

kujisomea na kilichobaki ni mwanafunzi mwenyewe kufanya jitihada ili kuhakikisha kwamba, maisha yake anayajenga vizuri.

### 5.2.7 Kudumisha Amani

Tanzania ni nchi ambayo inafahamika kama kisiwa cha Amani. Hata katika harakati za kudai uhuru, wananchi wakiongozwa na viongozi wao walidai uhuru kwa njia za amani na utulivu pamoja ustahamilivu. Baada ya uhuru kupatikana Kandoro alitunga shairi kuwataka wananchi kuendelea kuilinda nchi yao pamoja na kuelimisha juu ya amani. Katika shairi la *Kuhanisika si vyema* anasema:

*Tupiganie amani, tulinde nchi mapema*
*Mapema tuwe njiani, wasi kutuandama*
*Tuwakinge mipakani, wabaki kushika tama*
*Kuhanisika si vyema, tupiganie amani.*

Kandoro anaona ni jambo la ajabu sana kuupata uhuru kwa njia ya amani halafu tena tuipoteze amani kirahisi rahisi tu. Hivyo anaona kwamba itakuwa ni kuhanisika. Anaendelea kusema:

*Tupiganie amani, kwa akili na hekima*
*Busara ziwe vichwani, tupigane tukipima*
*Tusimame mipakani, kuhanisika si vyema*
*Kuhanisika si vyema, tupiganie amani*

*Lingine nalibaini, pia nalo nalisema*
*Sisi wana Watanzania, tusiwe nayo tamaa*
*Tukumbuke ya zamani, tulivyofanywa wanyama*
*Kuhanisika si vyema tupiganie amani.*

Katika beti hizi Kandoro anasisitiza juu ya kupigania amani tena kwa kutumia busara ya hali ya juu. Kandoro anafahamu kwamba, binadamu hakosi kasoro na kukosana ama kupigana miongoni mwao ni jambo la kawaida kwa mwanadamu. Kandoro

anapendekeza kwamba, haya yafanyike kwa ustaarabu, busara na kuvumiliana ili yasiipoteze amani adhimu tuliyonayo leo. Kandoro anasema: *Tukumbuke ya zamani, tulivyofanywa wanyama*. Kwa mujibu wa Kandoro, hii inatosha na hatuna haja tena ya kutaka kurudi katika hali hiyo bali *kuhanisika si vyema, tupiganie amani*. Hili ndilo jambo la msingi la kufanywa na kila mwananchi.

Mawazo haya ya Kandoro ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti huu hasa katika kipindi cha vyama vingi vya siasa vilivyopo hivi sasa. Katika siasa za vyama vingi zinazoendelea nchini kumekuwepo na sintofahamu nyingi ambapo mara kadhaa kumetokea mauaji ya watu katika mikutano ya hadhara ama maandamano yanayofanywa na chama cha upinzani cha CHADEMA. Sintofahamu hizi zinahatarisha kudumu kwa amani tuliyonayo hivi leo. Ni vema vyama vya siasa na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vihakikishe kwamba, amani inadumishwa kwa kuendesha mambo yake kwa amani, utulivu na kuvumiliana pamoja na kuheshimiana.

### 5.2.8 Kandoro na Ujamaa na Kujitegemea

Mnamo mwaka 1967 kupitia Azimio la Arusha serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilianzisha siasa za Ujamaa na Kujitegemea. Siasa hizi zilileta mapinduzi katika sekta mbalimbali za maendeleo kama vile kilimo, afya, maji, barabara, viwanda na umeme kutaja chache. Nia ya kuanzisha Ujamaa na Kujitegemea ni kuhakikisha kwamba wananchi wote wanaishi katika maisha ya usawa, haki na amani (Nyerere, 1969). Kufuatana na nia njema iliyokusudiwa katika Azimio la Arusha watunzi mbalimbali wa ushairi wa Kiswahili waliandika mashairi kulisifu na

kulipamba Azimio la Arusha. Miongoni mwa washairi hao ni Kandoro ambapo 1978 alitunga kitabu cha Ushairi kiitwacho *Liwazo la Ujamaa* chenye shairi lisemalo:

> *Natoa liwazo la Ujamaa,*
> *Wataolipenda wale jamaa,*
> *Sio wale watu walokomaa,*
> *Katika dhuluma wazitendazo.*

Hapa anaonesha kwamba, Azimio la Arusha lilianzisha siasa za Ujamaa na Kujitegemea ili kupinga dhuluma katika jamii kwa maana kwamba, rasilimali za taifa zitatumiwa kwa usawa na wananchi wote. Hata hivyo, Kandoro anatahadharisha kwamba mafisadi na wadhulumaji hawatakubali kuanzishwa kwa ujamaa kwa kuwa wanajua kwamba huo ndio utakuwa mwisho wao. Hii inaonekana ni kweli kwa kuwa ndivyo ilivyokuwa pale Waziri Mkuu Edward Moringe Sokoine alipopambana na wahujumu uchumi na kutaifisha mali zao zote.

Hata hivyo, pamoja na kuwa na hofu kwamba, wadhulumaji watalikataa Azimio la Arusha aliendelea kuwahimiza wananchi wote kulipokea kwa mikono yao miwili na kuhakikisha kwamba dua zote watakazokuwa wanazifanya pia waombe kukubalika kwa Azimio la Arusha na siasa zake za Ujamaa na Kujitegemea. Anasema katika ubeti mwingine kwamba:

> *Tushikamane kushikamana,*
> *Tudumishe penzi la ujamaa,*
> *Hata kila siku Jumapili na Ijumaa.*
> *Dua zetu wote ziwe ni nguzo.*

Hapa Kandoro anawafanya wananchi walione suala la ujamaa kuwa ni muhimu na lina manufaa katika maisha ya wananchi wote ndio maana anawataka waombe dua ili likubalike. Vilevile, Kandoro anaonesha kwamba umoja na mshikamano ni jambo

muhimu miongoni mwa wanajamii ili kuhakikisha kwamba Azimio la Arusha linakubaliwa na wananchi wote. Kwa maana nyingine ni sawa na kusema kwamba hata wale wanaopinga kuanzishwa kwa Azimio la Arusha ni dhahiri kwamba, watashindwa iwapo wananchi wote wataungana na kuwa kitu kimoja kwa kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Katika shairi jingine la *Mjamaa Kazi Yako Kutuongoza Maisha* Kandoro anataka watu wote wajipambe na kujivisha vivazi vya ujamaa ili kuunadi ujamaa kwa wananchi wenzake. Anasema:

*Mjamaa elimisha, Ujamaa ulioko,*
*Kuneemesha maisha, ya wenzako na ya kwako,*
*Mpaka yatakapoisha, uende kwa mola wako,*
*Mjamaa kazi yako, kutuongoza maisha*.

Kandoro anamtaka kila mwananchi kuupenda ujamaa na kisha baada ya hapo kueleza faida zilizomo katika ujamaa kwa wananchi wengine. Miongoni mwa faida hizo ni maisha mazuri kwa kila mwananchi katika kipindi chote cha maisha yake. Katika ubeti mwingine anasema:

*Mjamaa huamsha, kutangaza badiliko,*
*Maadui humtisha, na hatishiki tishio,*
*Hoja zake huzidisha, kwa vitabu na tamko,*
*Mjamaa kazi yako, kutuongoza maisha*.

Hapa Kandoro anaonesha kwamba, ujamaa hutekelezwa kwa vitendo na si maneno peke yake. Waswahili wana methali yao isemayo, *maneno matupu hayavunji mfupa*. Pia anasema kwamba, maadui wa ujamaa watamtisha mtu afuataye siasa za ujamaa kwa vitisho mbalimbali lakini kamwe huwa haogopi vitisho hivyo daima yeye ni

kusonga mbele tu. Pia Kandoro anaeleza kwamba, mjamaa hupaswa kutoa hoja madhubuti dhidi ya wale wote wanaopinga Ujamaa na Kujitegemea. Hoja hizo huchotwa katika vitabu, Iikiwa na maana kwamba, kila mjamaa ni wajibu kujifunza ili aweze kuufahamu vyema ujamaa na asitetereke katika kuutetea dhidi ya maadui.

Si hivyo tu bali pia, Kandoro anawataka viongozi kuumanisha maneno na vitendo vyao kuhusu Ujamaa na Kujitegemea. Haipendezi kiongozi kuhubiri ujamaa na kisha kutenda ubepari. Katika ubeti mwingine anasema:

*Uchafu kuusafisha, kwataka imani kwako,*
*Kwamba uchafu rabusha, kudhuru maisha yako,*
*Utoe na kuonesha, kwamba uchafu hauko,*
*Mjamaa kazi yako, kutuongoza maisha*.

Hapa msanii anatumia lugha ya picha kuwataka viongozi wote kuwa msitari wa mbele katika kutekeleza siasa za Ujamaa na Kujitegemea. Iwapo viongozi watahubiri ujamaa na kutenda ubepari wafahamu kwamba chuki na huzuni ya wananchi juu yao itadhuru maisha yao na hawataishi vyema kama wadhaniavyo. Anawataka viongozi wasibaki na hata chembe kidogo ya unyonyaji wa mali na rasilimali za wananchi badala yake wajisafishe. Anasema: *Utoe na Kuonesha, kwamba uchafu hauko*.

Kandoro anasema, ujamaa ni kupendana na kushirikiana na anaonya kuona wananchi wakichukiana na kununiana. Anasema:

*Kwetu ni aibu sana, watoto wa Ujamaa,*
*Iwapo wajibizana, na sura zikadumaa,*
*Vipaji kukunjiana, hao si wanaujamaa*
*Watoto wa ujamaa, hucheza wakipendana*.

Hapa mshairi anaonya wananchi kutofanya majibizano ambayo yatasababisha kutoelewana na kuumpinga ujamaa. Ikiwa hilo litatokea basi itakuwa ni aibu sana kwa wanaujamaa. Hata hivyo, kwa maoni yetu tunaona kwamba, Kandoro anazuia uhuru wa kujieleza na kutoa maoni kwa kila mwananchi kuhusu Ujamaa na Kujitegemea. Anawataka watu wote kuwa na mawazo yanayofanana jambo ambalo haliwezekani. Suala jipya kama Ujamaa na Kujitegemea linapoanzishwa nchini linahitaji kujadiliwa kwa uwazi na kila mwananchi kupata nafasi ya kushiriki. Lakini hili halikufanyika na ndio maana hata Kandoro naye anazuia jambo hilo kufanyika.

Vile vile, Kandoro anaonesha kwamba, Ujamaa na Kujitegemea ni kufanya kazi na si lelemama. Katika shairi la *TANU inasema kweli* anasema:

> *Tulime bila kusita, kujitegemea hali,*
> *Tufanye kazi kupita, japo ndani ya meli,*
> *Kazi kwetu iwe kwata, kuunyoosha mwili,*
> *TANU inasema kweli, kwamba tutashinda vita*.

Hapa mshairi anawataka wananchi kufanya kazi hasa kilimo kwa juhudi na maarifa ili kuleta maendeleo nchini. Ujamaa na Kujitegemea maana yake ni kufanya kazi za uzalishaji mali kwa ajili ya matumizi ya jamii katika maisha yake ya kila siku bila kupata mapungufu ya aina yoyote. Anasema, ni muhimu kwa kila mwananchi kufanya kazi yake kwa umakini na ustadi mkubwa ili kuleta maendeleo. Vilevile, hakuna haja kwa mwananchi kuchagua kazi. Kila mtu katika kazi yake ahakikishe kwamba anajituma na kuitekeleza vizuri kwa manufaa yake yeye mwenyewe na wananchi wenzake. Huu ndio Ujamaa na Kujitegemea.

Kwa upande mwingine, Kandoro anazungumza juu ya viongozi kwamba, wao wako sawa na wananchi na wao si tabaka la juu. Misingi ya Ujamaa na Kujitegemea inatamka kwamba, binadamu wote ni sawa na hakuna aliyebora kuliko mwingine kwa msingi huu hakuna haja ya kiongozi yoyote kujivuna kupitia uongozi wake. Kupitia shairi *Mwiko mwanasiasa* anasema:

*Kumkemea si kitu, ijapo kiwe kisa,*
*Pindi awe kufuatu, na heshima amekosa,*
*Wewe mwenye kitu, kwani unayo fursa,*
*Ni mwiko mwanasiasa, kujivunia watu.*

*Tanzania nchi yetu, kukaripia twasusa,*
*Ndio uongozi wetu, kuinyanyua siasa,*
*Imesema TANU yetu, kukaripia ni kosa*
*Ni mwiko mwanasiasa kujivunia watu*!

Hapa Kandoro anawaonya viongozi kuacha tabia ya majivuno mbele ya wananchi na badala yake wanapaswa kuwatumikia wananchi kikamilifu kwa kuwa wananchi ndio waliowachagua viongozi hao. Mawazo haya ya Kandoro ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa minajili kwamba, katika enzi hizi hali haiko kama Kandoro anavyofikiria. Viongozi wa leo wanaishi katika nyumba nzuri tofauti kabisa na zile za wananchi wao waliowachagua katika majimbo ya uchaguzi. Hawaendi majimboni mwao mpaka kipindi cha uchaguzi katika harakati za kuomba kura kwa wananchi. Hii ni sehemu tu ya ufahari na majivuno walionayo wengi wa viongozi wa siasa wa siku hizi.

Hata hivyo, ingawa Kandoro anazungumzia wanasiasa kuacha kujivuna, vile vile anawataka na wananchi wote pia kujiepusha na tabia hiyo mbaya isiyo na tija kwa maendeleo ya mwanadamu. Anasema:

*Asilani hajivuni, kwa kitu asichoweza,*

*Yamkini hakiguni, hathubutu kukibeza,*
*Wala haoni huzuni, ni tayari kujifunza,*
*Usichojua uliza, mjamaa hajivuni.*

Mjamaa hapaswi kujivuna na badala yake anatakiwa aulize kile asichokijua na ataelekezwa kwa anayejua nae hajivuni atamwelekeza tu na kisha ataelewa kila kitu kuhusu kile alichokuwa hakijui. Miongoni mwa wale wasiojivuna ni Mwalimu Nyerere ambaye Kandoro anamsifu kwa kusema:

*Maneno mengi kinywani, unapozungumza,*
*Yanaingia kichwani, kwa raha twasikiliza,*
*Na hiyo nayo ni fani, ya mtu kuitunza,*
*Usichojua uliza, mjamaa hajivuni.*

Hapa anaeleza kwamba, mwalimu Nyerere alikuwa ni kiongozi asiyejivuna na alitumia muda wake mwingi katika kutoa elimu juu ya maisha kwa wananchi wote wakati wote wa uongozi wake.

Pia Kandoro anautukuza ujamaa kwa sababu utasaidia katika kuifanya nchi isiwe tegemezi kwa mataifa tajiri na kuweza kujitegemea yenyewe. Kupitia shairi lake la *Ombaomba Nchi haiendelei* (1978) anasema:

*Mali zetu hawatwai, tusishiriki kuomba,*
*Nao hawatuchezei, wala mafundi warumba,*
*Sauti zisilegei, zingurume kama simba,*
*Maisha ya ombaomba, nchi haiendelei.*
*Na sisi tusilegei, nje hatuna wajomba,*
*Bora tusitegemei, kuinuka kwa kuomba*
*Huko ni kujikebei, taifa la ombaomba,*
*Maisha ya ombaomba, nchi haiendelei.*

Katika beti hizi Kandoro anaonesha kwamba, kuombaomba ni kubaya. Ikiwa nchi itakuwa ombaomba ifahamu kwamba kila itakachosaidiwa basi itakirudisha kwa gharama kubwa zaidi ya ile iliyopewa. Vilevile, anaonya kwamba, nchi haiwezi

kupiga hatua ya maendeleo kwa kuombaomba kwani daima cha kuomba huwa hakitoshelezi hata siku moja. Njia pekee ya kuiepusha nchi kuwa ombaomba ni kufanya kazi kwa juhudi na maarifa. Hili litawezekana pale tu nchi itakapotekeleza vizuri siasa za Ujamaa na Kujitegemea.

Kwa upande mwingine Kandoro anawataka wananchi kujiamini kwamba, wao wanaweza kuiletea nchi maendeleo bila kutegemea misaada kutoka kwa wahisani wa maendeleo. Hili analisema katika ubeti ufuatao:

*Mali zetu hawatwai, tusishiriki kuomba.*
*Nao hawatuchezei, wala mafundi warumba,*
*Sauti zisilegei, zingurume kama simba,*
*Maisha ya ombaomba, nchi hailendelei.*

Katika msitari wa tatu anasema: *Sauti zisilegei zingurume kama simba* akiwa na maana kwamba, wananchi wanapaswa kujiamini na katu wasikate tamaa kwa kuwa hakuna mtu atakayewaletea maendeleo zaidi ya wao wenyewe. Na hili litawezekana pale ambapo nchi itakuwa chini ya misingi ya Ujamaa na Kujitegemea na si vinginevyo.

### 5.2.9 Mapenzi Kwa Taifa

Usomapo ushairi wa Kandoro utagundua kwamba, ni mtu aliyeipenda sana nchi yake. Kwa mfano, katika shairi, *Mapenzi Yangu Moyoni Taifa Kuliko Mali*, anasema:

*Naomba ujahili, moyoni mwangu moyoni,*
*Neno hili si kaliki, kwani ndilo langu oni*
*Wala si kitendawili, kwa ndugu wanachuoni,*
*Mapenzi yangu moyoni, taifa kuliko mali.*

Katika msitari wa mwisho tunaoneshwa kwamba Kandoro aliipenda sana nchi yake kuliko jambo lingine lolote hasa mali. Hili linathibitishwa hata na aina ya maisha aliyoishi. Mtafiti alifanya usaili na mmoja wa ndugu wa Kandoro ambaye alieleza kuwa:

> *Kandoro hakuwa mtu tajiri, amefariki akiwa masikini. Aliwahi kushika nyadhifa kubwa serikalini. Kwa mfano, Kandoro alikuwa mkuu wa wilaya kwa miaka kadhaa, mjumbe katika halmashauri kuu ya chama na nyadhifa nyinginezo lakini amefariki akiwa masikini. Ukimlinganisha Kandoro na viongozi wengine ambao wameshika mamlaka aliyopata kuyashika utaona tofauti kubwa. Asilimia kubwa wana uwezo mkubwa wa fedha na mali. Kandoro aliipenda sana nchi yake kuliko mali na utajiri.*

Maelezo katika dondoo hapo juu yanalandana na ubeti huu:

> *Usingizi mi silali, maisha nilale chini,*
> *Pindi nisipate mali, nife na umasikini,*
> *Taifa silidhalili, kulitoa maanani,*
> *Mapenzi yangu moyoni, Taifa kuliko mali.*

Kandoro anasema kwamba, yu radhi kulala chini na kuendelea kuwa masikini lakini taifa lake lisonge mbele. Haya ndiyo mapenzi ya Kandoro kwa taifa lake la Tanganyika na baadaye Tanzania.

### 5.2.10 Kandoro Mshereheshaji wa Sera za Maendeleo

Sera ni dira ama mwelekeo wa kufanikisha jambo fulani kwa manufaa ya watungaji na watungiwa wa sera hiyo. Sera ni mwongozo ambao huelekeza jinsi na namna jambo/mradi fulani unavyopaswa kutekelezwa ili kuleta maendeleo kwa taifa. Kwa msingi huo, serikali hutunga sera mbalimbali kwa lengo la kuwaletea wananchi wake maendeleo. Sera hutungwa na Serikali huku watekelezaji wake wakiwa ni wananchi. Kandoro kama kawaida yake ametunga mashairi ya kuwahamasisha wananchi

kutekeleza sera za maendeleo kwa tija na ufanisi mkubwa. Katika shairi *Vita vya kufa na Kupona* anasema:

> *Ndugu rijali nchini, wanali wa majina,*
> *Na wake wenye thamani, wenye kuja wa kutona,*
> *Vita viko uwanjani, kusiwe mpiga kura,*
> *Vita kufa na kupona, silaha jembe kwapani?*
> *Wapi wenye Liwatani, wasichana wavulana,*
> *Na wazee wa zamani, twendeni tukifuatana,*
> *Mkitujaza imani, vita kwenda kupambana,*
> *Vita kufa na kupona, silaha jembe kwapani.*

Katika beti hizi Kandoro anawahimiza wananchi kutekeleza sera ya serikali ya Kilimo cha kufa na kupona ili kukabiliana na njaa kali iliyoikumba nchi katika miaka ya 1970. Katika kufanya hivyo anaonesha kwamba utekelezaji wa sera hiyo ulihitaji ushiriki wa kila mtu akitaja makundi yote katika jamii. Hapa Kandoro anaonesha kwamba, anafahamu umuhimu wa wananchi kushiriki katika utekelezaji wa sera za maendeleo na kwamba bila wao sera hizo haziwezi kutekelezeka ipasavyo na kuliletea taifa maendeleo. Mawazo haya ni muafaka na tunaungana nayo mkono kwa asilimia mia kwa mia. Katika kutia msisitizo wa kutekeleza sera, Kandoro anawaasa wananchi kwa maneno yenye kuuchoma moyo pale anaposema:

Tusirudi utumwani, kutawaliwa kwa dona,

> Dona kungoja melini, ni fedheha kuyaona,
> Bora kufia kondeni, hatufi na tutapona,
> Vita kufa na kupona, sila jembe kwapani.

Kandoro anaonya kwamba, kutokufanya kazi ya kilimo kwa juhudi na maarifa kutawafanya wananchi kurudia hali ya utumwa kama ilivyo kuwa katika kipindi cha ukoloni. Hivyo ni wajibu kwa kila mwananchi kuhakikisha kwamba anatekeleza sera ya serikali ya kilimo cha kufa na kupona ili kuhakikisha kwamba, nchi inakuwa na

chakula cha kutosha. Wananchi waliitikia mwito wa serikali na Kandoro na kwa hakika shida ya njaa ilitoweka nchini.

### 5.2.11 Afrika ni Moja

Dhana ya kwamba Afrika ni moja inaeleweka hata kwa Wakoloni wenyewe. Akizungumza katika moja ya hotuba zake Mwalimu Nyerere anasema kwamba: siku moja alikutana na ujumbe wa mataifa yaliyoendelea kujadili juu ya mambo mbalimbali ya maendeleo. Kabla hata mkutano haujaanza viongozi wa Ulaya walianza kumuuliza maswali na habari za mataifa kadhaa ya Afrika. Licha ya kwamba Mwalimu Nyerere anatoka Tanzania aliulizwa habari za Kongo, Rwanda, Burundi, Afrika ya Kusini na kadhalika. Hii inaonesha kwamba Afrika ni moja na kiongozi wa taifa fulani la Afrika anachukuliwa kama pia ni kiongozi wa taifa lingine. Kandoro naye anaiona *Afrika kama ni nchi moja* kupitia shairi la *Afrika ni Moja*. Anasema:

*Nenda na nyuma ukija, Nyerere muheshimiwa,*
*Ziipeleke zetu hoja, Kwa nduguzo wasifika,*
*Haifai ngoja ngoja, kwani yalia Afrika,*
*Hii Afrika ni moja, ni nchi ya Wafrika.*

Katika msitari wa mwisho anasema kwamba: Afrika ni moja na matatizo yao yanafanana kwani ilitawaliwa na watu walewale waliokuwa na nia mbaya ya kunyonya rasilimali za Waafrika. Kwa msingi huu, Afrika inapaswa kukaa pamoja ili kupanga mipango ya namna ya kupambana na Hima/Changamoto za maendeleo na kubadilishana, uzoefu ili kujiletea maendeleo. Kandoro anasema:

*Wakoloni walikuja, kugawana Afrika,*
*Nchi wakachanjachanja, na kuiweka mipaka,*
*Mfano mbuzi kuchinja, na nyama kuibanika,*

*Je, leo hii ni nchi ya Waafrika Kweli*?

Katika ubeti huu Kandoro anaonesha kwamba, Afrika ni nchi moja ila ilitenganishwa na wakoloni kwa masilahi yao binafsi. Masilahi hayo ni kugawana rasilimali kama vile madini, ardhi, maji, masoko na nguvu kazi ya Afrika kutaja rasilimali chache. Kandoro anawataka Waafrika watambue kwamba, wao walikuwa ni kitu kimoja kabla ya ujio wa Wakoloni na kwamba wasije wakalisahau suala hilo hata siku moja.

Mawazo haya ya Kandoro ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti huu kwa msingi kwamba, umoja wa Afrika ni jambo lililopigiwa debe na kunadiwa sana na viongozi wa Afrika akiwepo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Kwame Nkuruma, Jomo Kenyatta, Kamuzu Banda, Keneth Kaunda na wengineo. Hata hivyo, hilo halikuweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa kutokana na ubinafsi wa viongozi wa sasa wa bara la Afrika. Ubinafsi unawafanya kufikiri kwamba, iwapo watafanikisha kupatikana kwa umoja imara wa Afrika basi watapoteza sehemu kubwa ya utawala na mamlaka yao. Kupoteza mamlaka na madaraka maana yake ni kupoteza utajiri wanaoupata kupitia wizi wa fedha na rasilimali za nchi wanazoziongoza. Kwa hali hii ndoto ya Kandoro ya kutaka kuona Afrika inakuwa nchi moja kama ilivyokuwa kabla ya ujio wa Wakoloni inabaki kuwa ni ndoto tu isiyotekelezeka.

### 5.2.12 Kandoro na Ushairi wa Kiswahili

Katika miaka ya 1970 kulikuwa na mjadala mkubwa kuhusiana na ushairi wa Kiswahili. Wataalamu wa Kiswahili kama Njogu na Chimerah (1999) wanauita mjadala huo kuwa ni mgogoro wa ushairi. Mulokozi na Kahigi (1979) nao wanauita mgogoro wa Ushairi wa Kiswahili. Mgogoro huu ulihusisha pande mbili ile ya

wanausasa na wanamamboleo. Kambi ya wanausasa iliongozwa na Euphrase Kezilahabi, Jared Angira, Ebrahim Hussein, Kulikoyela Kahigi na Mugyabuso Mlinzi Mulokozi. Kambi ya wanamapokeo iliongozwa na Jumanne Mayoka, Saadan Kandoro, Abdilatifu Adballah, Mathias Mnyampala, Mdanzi Hanasa Mzee Waziri Kijana na Sudi Andanenga kwawataja wachache. Mgogoro ulianza pale Kezilahabi alipotunga diwani ya *Kichomi* ikiwa na mashairi yasiyofuata arudhi ya ushairi wa Kiswahili iliyozoeleka kwa wanamapokeo. Euphrase Kezilahabi alipotunga mashairi yasiyofuata urari wa vina na mizani ambapo kwa wanamapokeo hiki kilionekana kama ni kitendo cha kuuangamiza ushairi wa Kiswahili. Tazama mfano wa shairi hili:

*Azimio sasa ni mabaki ya chakula*
*Kwenye sharubu za bepari*
*Kalamu inayovuja*
*Katika mfuko wa mwanafunzi*
*Vumbi zito*
*Baada ya ng'ombe kupita*
*Hakunyolewa*
*Hakupewa kalamu mpya*
*Na njia haikuzibwa*
*Kilichosalia sasa*

*Ni punje za ulezi*
*Zilizosambazwa jangwani*
*Na mpandaji kipofu*

Huu ni ubeti kutoka katika shairi la *Azimio* Kezilahabi (1988:27) ambalo halifuati urari wa vina na mizani. Utunzi wa mashairi ya aina hii uliwachukiza sana wanamapokeo ambapo pamoja na mambo mengine Kandoro alimwomba Mwalimu Nyerere apige marufuku uandishi wa aina hiyo wa ushairi katika Kiswahili. Mulokozi katika mazungumzo anaeleza kwamba:

> *Saadan Kandoro ni mtunzi wa mashairi ya Kiswahili katika mkondo wa wanamapokeo anayeheshimika sana. Kutokana na heshima aliyokuwa nayo siku moja alipata kumuomba Baba wa Taifa apige vita ushairi wa Kisasa kwa kuwa unakiuka kanuni za urari wa vina na mizani kama ilivyo katika ushairi wa wanamapokeo. Hata hivyo, baba wa Taifa hakukubaliana na Kandoro kwa kuwa alifahamu kwamba sanaa inahitaji ubunifu na kamwe haibaki katika umbo lake la asili daima dumu...*

Dondoo hili ndilo lililotufanya tuzungumzie juu ya Kandoro na ushairi wa Kiswahili kwa kuwa linaonesha kwamba, mgogoro wa ushairi ulihusisha siasa. Kandoro katika kuuelezea ushairi wa Kiswahili anasema kwamba:

> *Kumeshatolewa tafsiri kwa maelezo tafauti tafauti na wataalamu wa ushairi wa Kiswahili. Kilicho muhimu hapa ni kwamba ingawa wataalamu hao wamelieleza shairi la Kiswahili kwa maneno tafauti lakini kwa ujumla wao wamekubaliana kuwa shairi la Kiswahili ni lazima liwe na vina na mizani. Vitu viwili hivi ni kama roho ya shairi la Kiswahili ingawa si hivyo pekee vilikamishalo hata likastahili kuitwa "Shairi". Shairi hata likiwa limeandikwa kwa lugha ya Kiswahili na hata liwe limeandikwa na nani, maadamu vitu hivi viwili havimo miongoni kwa alivyoyovitumia kulitungia, basi haliwi ni shairi la Kiswahili* (1978:61-62).

Katika dondoo hili Kandoro anaonesha kwamba, pamoja na mambo mengine ushairi wa Kiswahili ni lazima uwe na vina na mizani. Mawazo haya ya Kandoro yanapingana na yale ya Mulokozi (1975:46) ambaye anaeleza kwamba:

> *Ushairi wa Kiswahili hautambuliki sana kwa muundo wake bali historia yake, lugha yake, utamaduni na masuala ya kijamii unayoyaeleza. Hivi ndivyo vitu vya msingi lakini siyo vina na mizani ndiyo hutofautisha ushairi wa Kiswahili na ushairi mwingine duniani.*

Mawazo haya ya Mulokozi hayakubaliwi kabisa na wanamapokeo ambao wanaendelea kueleza kwamba: Ushairi ni ule wenye vipande vilivyo na ulinganifu wa mizani zisizo pungufu wala zilizozidi; na vipengele hivyo viwe vimetandwa na

maneno ya mkato maalumu na yenye lugha nyoofu tamu na laini, lugha ambayo ina uzito wa fikira, lugha ambayo ni tetelezi kwa ulimi utakaoitamka, tamu kwa mdomo utakaoisema, tumbuizi kwa masikio yatakayosikia na yenye kuathiri moyo uliokusudiwa na kama ulivyokusudiwa. Huu ndio utungo ufaao kupewa jina la "Ushairi" katika ushairi wa Kiswahili. Mawazo haya hayakubaliki hata kidogo kwa wanausasa. Shairi sio lazima liwe na lugha tamu wala telezi ndio liitwe shairi. Suala la utamu ni gumu sana kupimika kwa kuwa si kila mtu anaweza kusema kitu fulani ni kitamu. Wapo ambao wanaweza kusema kitu hiki ni kitamu sana wengine wakasema hakina utamu kabisa kwa wakati uleule. Suala la msingi ni kwamba, huo unaoitwa ushairi unaoeleza nini na unatumia mtindo wa lugha ya mkato? Kama hivyo ndivyo basi hilo latosha kuwa shairi–mtazamo wa wanausasa. Akinukuu shairi la Mulokozi, Kandoro (1978:84-85) anasema:

*Umbo na pia wazole, ninataka kuhusisha*
*Sinchi mizani sichele, vina kunitetemesha*
*Hili vazi la umbile, si faradhi kulivisha*
*Muhali wazo kufisha, kwa kufungwa na ukale.*

Mulokozi anaafiki kwamba, si lazima kuendelea na vazi hilo hilo moja siku hata siku na badala yake yanahitajika mabadiliko ili kuifanya sanaa iendane na hali halisi ya jamii kwa wakati uliopo na unaokuja.

Kimsingi, mashairi ya kisasa na ya kimapokeo yanakubalika na yote yanaendelea kutumiwa na wasanii katika mashairi yao wanayotunga kila siku. Hivyo si jambo la manufaa leo hii kuanza kuzungumza kwamba aina hii ya ushairi ni bora kuliko nyingine. Wasanii wa muziki wa bongo fleva kwa mfano wanatumia mashairi ya kisasa kwa wingi sana katika kuwasilisha nyimbo zao kwa hadhira iliyokusudiwa na

kwa kiasi kikubwa nyimbo zao hukubalika kwa wasikilizaji wake. Kwa kutumia ushairi wa kisasa wanamuziki wa bongo fleva wamejipatia ajira wao binafsi na vile vile, katika makampuni ya uzalishaji, usambazaji na uuzaji wa nyimbo za bongo fleva. Vilevile, mapato yatokanayo na muziki huu hutumika katika kuongeza pato la taifa kupitia kodi mbalimbali zitolewazo katika tasinia ya muziki wa bongo fleva.

Taaluma ya ushairi imeendelea kupiga hatua siku hata siku ambapo kwa sasa wapo washairi ambao hutunga mashairi yao kwa kutengeneza maumbo ya picha mbalimbali. Kwa mfano: Mshairi Kithaka wa Mberia hutunga mashairi katika umbo la wanyama mbalimbali kama vile paka, panya, simba na kadhalika. Vilevile, hutunga mashairi kwa kuumba maumbo kama vile pembe tatu, duara, na kadhalika. Hii yote inaonesha kwamba: mjadala kuhusu ushairi ni lazima uwe na vina na mizani umepita na sasa washairi wana jambo jipya la kujadili na kuzungumzia. Haya ndio maendeleo katika taaluma ya ushairi ambayo ni sanaa na sanaa ni taaluma hai.

### 5.2.13 Kandoro na Masuala ya Dini

Dini ni mfumo kamili wa maisha anaoufuata mwanadamu katika kuendesha maisha yake ya siku hata siku. Dini hutoa mwongozo wa namna ya kutenda ama kutotenda jambo fulani kwa masilahi ya mtendaji na jamii yake kwa ujumla. Kwa upande wa idadi ya dini ni nyingi lakini zinazotambulika kwa kuwa na wafuasi wengi ni Uislamu na Ukiristo. Katika *Liwazo la Ujamaa* Kandoro anasema:

> *Tushikamane kushikamana*
> *Tudumishe penzi la ujamaa,*
> *Hata kila siku, Jumapili na Ijumaa,*
> *Duwa zetu wote ziwe ni nguzo.*

Maneno *Ijumaa* na *Jumapili* katika dondoo hapo juu yanaonesha kwamba, Kandoro anatambua kwamba, wengi wa Watanganyika ni Waislamu na Wakristo. Kwa kufanya hivi tunamwelewa Kandoro katika namna kadhaa kuhusiana na masuala ya dini na siasa. Mosi, tunaelewa kwamba Kandoro alifahamu kwamba, dini ina nafasi kubwa katika kufanikisha masuala ya kisiasa katika jamii. Ni katika dini ndipo wananchi/waumini hufunzwa umuhimu wa kujenga amani na utulivu katika jamii zao. Vilevile, kudumisha upendo na kutendeana haki miongoni mwao hufunzwa katika mafundisho ya dini zao. Mambo haya kwa pamoja ndio huwawezesha watawala wa kisiasa kutawala vizuri na kupanga sera nzuri za maendeleo na ustawi wa wananchi wao. Iwapo dini hazitatoa mafunzo hayo na kuwajenga waumini wake katika misingi hiyo basi kuitawala nchi itakuwa ni kazi ngumu sana.

Pili, tunapata uelewa kwamba, Kandoro hakuwa na ubaguzi wa dini katika uhamasishaji wa masuala ya kisiasa. Anaamini kwamba, sera ya Ujamaa na Kujitegemea ni ya wananchi wote na si ya watu wa dini fulani na kwamba ili ifanikiwe ni dhahiri watu wote hao wanapaswa kuiunga mkono. Kwa dhana hii Kandoro hatofautiani sana na Shaaban Robert alipoandika *Siku ya Watenzi Wote*. Shaaban Robert hata hivyo, alifikia hatua ya juu zaidi pale aliponadi kwamba, dini zote mbili yaani Uislamu na Ukiristo ziungane pamoja na kuwa kitu kimoja. Alifikia kutoa ushauri huu kwa kuwa hakuona tofauti za msingi zilizopo baina ya dini hizo na kwamba zote zipo kwa minajili ya kumuongoza mwanadamu katika kutenda mema na kuacha mabaya. Ingawa Kandoro hakufika katika hatua hii lakini naye pia hakubagua Watanzania kwa misingi ya dini zao.

Tatu, tunapata kufahamu kwamba, suala la kutenganisha dini na siasa ni la kinadharia zaidi kuliko vitendo. Viongozi wa siasa akiwemo Mwalimu Nyerere alikuwa msitari wa mbele katika kunadi kwamba ni marufuku kuchanganya dini na siasa. Dini zifanye kazi zake na siasa ziendelee na kazi yake. Hata hivyo, tunapokuja katika utendaji tunabaini kwamba, vitu viwili hivi vinategemeana sana na kamwe haviwezi kutenganishwa kwa dhati yake.

Nne, tunapata uelewa kwamba, Kandoro alitaka wananchi waombe dua ili siasa za Ujamaa na Kujitegemea zikubaliwe na wananchi kwa kuwa ni muhimu sana kwa manufaa ya wananchi wote. Kwa kufanya hivyo, hakutaka mwananchi yoyote alipuuze na kutotilia maanani siasa za Ujamaa na Kujitegemea. Mawazo haya yalichukuliwa na wananchi walio wengi ambapo siasa za Ujamaa na Kujitegemea zilikubaliwa na mara moja utekelezaji wake ukaanza kwa mafanikio makubwa.

Tano, tunapata kufahamishwa kwamba, sera ya Ujamaa na Kujitegemea haikuwa na mtazamo au chanzo kutoka dini yoyote kati ya Uislamu na Ukiristo. Iwapo kungekuwepo na mawazo ya aina hiyo ni wazi kwamba Kandoro asingewataka wananchi wa dini zote kuombea dua siasa za Ujamaa na Kujitegemea. Hivyo kwa kuliombea dua kwa pamoja kunawafanya wananchi wote kuliona Azimio la Arusha na Siasa zake kuwa ni mali yao na wanapaswa kulitekeleza kikamilifu kwa masilahi yao wote.  Mambo haya kwa hakika ndio tunayoyapata kuhusiana na Kandoro na masuala ya dini katika uhamasishaji wa masuala ya kisiasa.

## 5.3 Mbinu za Kisanaa katika Ushairi wa Kandoro

### 5.3.1 Utangulizi

Kandoro kama walivyo washairi wengine anatumia mbinu mbalimbali za kisanaa kuwasilisha ujumbe wa kisiasa kwa hadhira iliyokusudiwa. Mbinu za kisanaa ni jinsi au namna kazi ya fasihi ilivyosanwa na msanii kwa njia ambayo itampendeza msomaji wake na kuvutiwa kuisoma ama kusikiliza kazi hiyo zaidi na zaidi. Mbinu hizi huonekana katika vipengele vya fani kama vile matumizi ya lugha, mandhari, muundo, mtindo na wahusika kuvitaja vichache. Katika kubainisha mbinu mbalimbali za kisanaa zinazotumiwa na Kandoro tunaanza na kipengele cha matumizi ya lugha.

### 5.3.2 Matumizi ya Lugha

Lugha ndicho chombo kitumikacho kuwasilishia maudhui kwa hadhira ya kazi ya kifasihi. Saadan Kandoro ametumia lugha za aina mbalimbali katika mashairi yake huku lugha fasaha ya Kiswahili ikiongoza. Mbinu hii inamfanya msomaji kuyapata maudhui ya kisiasa kwa ufasaha wake na kwa dhati kabisa. Kwa mfano katika shairi *Ondoka nchini Kwetu* Kandoro anasema:

*TANU inalia sana, wote wanachama wetu,*
*Wanakulilia, bwana, uondoke hapa kwetu,*
*Bwana tafadhali sana, ondoka nchini mwetu,*
*Ondoka nchini mwetu, mwisho mwa mwaka huu.*

Katika shairi hili msanii anatumia Kiswahili sanifu kwa maana ya kueleweka barabara kwa msomaji wake bila kupata taabu ya kutafuta maana ya shairi. Katika shairi lingine la watokeze watetezi anasema:

*Watokeze watetezi, labda tutatukuka,*
*Tusifanye upuuzi, tutazidi kuanguka,*

*Ya jana siyo ya juzi, mambo yanabadilika,*
*Waafrika tu wapi, watokeze watetezi.*

Hapa msanii anaendelea kutumia Kiswahili fasaha ambacho kwacho dhamira ya ukombozi wa Afrika inajitokeza kwa uwazi na msomaji hatumii muda mrefu kutafakari ndipo aweze kuelewa maana ya shairi husika. Mbinu hii kwa ujumla imesaidia sana kuufanya ushairi wa Kandoro kukubalika na kupendwa na wasomaji wengi. Pamoja na utumizi wa Kiswahili fasaha, Kandoro ametumia pia mbinu ya kuchanganya lugha inavyothibitishwa hapa chini.

### 5.3.3 Uchanganyaji wa Lugha katika Ushairi wa Kandoro

Kuchanganya lugha ni kutumia lugha zaidi ya moja katika kazi ya kifasihi kama mbinu ya kuwasilishia ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Msanii Kandoro ametumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika ushairi kupitia baadhi ya mashairi yake. Katika shairi lake la *Tumshukuru maanani,* Kandoro anaandika:

*Maadui twaambiwa, ni wa watatu twabaini,*
*Ujinga twasimuliwa, ni adui namba wani,*
*Na maradhi, yametiwa, pamoja twaasikia.*

Katika msitari wa pili wa ubeti huu mshairi anasema ujinga twasimuliwa, ni adui namba wani". "Namba wani" ni neno lililoandikwa kwa silabi za Kiswahili lakini kwa asili ni neno la Kiingereza "Number One". Kandoro ametumia neno hili kuonesha msisitizo kwamba ujinga ni adui mkubwa sana wa maendeleo ya binadamu na hivyo kila mwananchi anapaswa asome kwa bidii ili aweze kupata elimu itakayomkomboa maishani. Vilevile, matumizi ya lugha hii ni kuonesha ukubwa wa tatizo la ujinga lilivyokuwa kubwa na waliosababisha hali hiyo ni wakoloni. Hapa msanii anawapandisha wananchi hasira ili wasirudi nyuma katika harakati za kudai

uhuru. Msanii Kandoro ametumia pia lugha ya kitamathali katika mashairi yake kama inavyooneshwa hapa chini.

### 5.3.4 Tamathali za Usemi katika Ushairi wa Kandoro

Matumizi ya tamathali za usemi yanajitokeza kwa kiwango kikubwa katika ushairi wa Kandoro. Tuanze na kipengele cha tahihisi.

#### 5.3.4.1 Tashihisi

Tashihisi ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa na msanii kuvipa uwezo wa kutenda kama binadamu viumbe wasio na uwezo wa kibinadamu. Katika shairi la *Ondoka nchini Kwetu* Kandoro anasema:

*TANU inalia sana, wote wanachama wetu,*
*Wanakulilia bwana, Uondoke hapa kwetu,*
*Bwana tafadhali sana, ondoka nchini, mwetu,*
*Ondoka nchini mwetu, mwishoni mwa mwaka huu.*

Hapa tunaambiwa kwamba *TANU inalia sana,* kimsingi TANU haiwezi kulia mwenye uwezo huo ni mwanadamu. Kandoro ametumia tamathali hii kuonesha kwamba, wananchi ambao ni wanachama wa TANU wamechoshwa na hila na madhila wanayotendewa na wakoloni na hivyo wanawataka waondoke nchini. Aidha kwa kukutumia tamathali hii Kandoro anaonesha ustaarabu na uvumilivu wa wananchi katika kudai uhuru wao kwa amani na utulivu. Hawakudai uhuru kama mtu mmoja mmoja bali kwa umoja na mshikamano kupitia chama chao cha TANU. Katika shairi jingine la *Siafu Wamekazana* Kandoro anaandika:

*Siafu wamekazana,*
*Nyoka amegutuka, ndani ya shimo katuna,*
*Tena amekasirika, hasira zenye kununa,*
*Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna,*
*Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.*

Tashihisi kadhaa zinajitokeza katika ubeti huu hapo juu; Kwanza ni ile inayooneshwa kwa siafu kutenda kama binadamu pale wanapoungana pamoja kudai haki yao ambayo ni uhuru. Pia tunaambiwa *nyoka* amenuna na shimoni anajikuna. Nyoka hapa ana rejelea mkoloni ambaye kutokana na umoja uliooneshwa na wananchi katika kudai uhuru wao amepata bumbuwazi na haelewi nini cha kufanya zaidi ya kutoa uhuru na kuondoka nchini. Matumizi ya pisha na ishara pia yanatumiwa sana na Kandoro katika ushairi wake kama ifuatavyo:

#### 5.3.4.2 Taswira na Ishara

Matumizi ya ishara na taswira hutumika hasa katika tanzu za ngano, methali, vitendawili na habari za kimafumbomafumbo (Senkoro, 2006). Mifano ya Senkoro imeweka pembeni ushairi ambapo bila shaka una matumizi makubwa ya taswira na ishara. Kandoro ni miongoni mwa washairi wanaotumia taswira na Ishara katika kuwasilishia ujumbe wa kazi zake. Katika shairi la *Siafu wamekazana* tunaambiwa:

*Shimoni ataondoka, hilo nataja kwa jina,*
*Nyoka anajua fika, siafu wakiungana,*
*Nguvu zinaongezeka, shimoni watagombana,*
*Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.*

Hapa msanii anatumia *nyoka* na *siafu* kitaswira na ishara. *Nyoka* ni mkoloni na *siafu* ni wananchi. *Nyoka* ni mdudu mwenye sumu kali yenye kuhatarisha maisha na usalama wa mwanadamu na wanyama wengine. Sumu ya nyoka inafananishwa na udhalimu wa mkoloni dhidi ya wananchi katika shughuli mbalimbali za uchumi kwa

malipo kidogo yasiyoendana/kulingana na ugumu na ukubwa wa kazi. Dhamira ya kufanya hivyo ilikuwa ni kumdunisha mwananchi ili aendelee kufanya kazi za mkoloni kila siku na kumtajirisha mkoloni huku yeye mwananchi akiendelea kuwa masikini wa kutupa. *Siafu* ni taswira inayopigwa kwa wananchi kwamba, wao ni wadogo kwa maana ya uwezo wa mali elimu na kila kitu lakini umoja wao ndio silaha muhimu itakayomwondoa mkoloni. Taswira hizi zimetumiwa kwa ufundi na ustadi mkubwa na Kandoro katika kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira iliyokusudiwa. Katika shairi la *Kuiga Bila Utafiti* anaeleza:

*Nao ni wenye mizungu,*
*Tangu karne za tangu,*
*Ndio waundaji vyungu,*
*Fitina kuipikia*.

Katika shairi hili msanii anatumia taswira kama *mizungu* kuonesha kwamba, wakoloni walikuwa wanafanya kila njia kuhakikisha kwamba, wananchi wanachukia na kuacha tamaduni zao na kufuata zile za wakoloni. Kwa hali hii anawaonya wanaushairi wa kisasa kuacha kuiga mambo bila kuyafanyia utafiti wa kutosha. Kwa kufanya hivyo utamaduni wa Mtanzania na Mwafrika kwa ujumla utapotea kabisa. Haya ndio mawazo ya Kandoro kuhusu kuiga mambo bila kufanya utafiti wa kina. Mbinu nyingine inayotumiwa na Kandoro katika kujenga dhamira za mashairi yake ni ile ya Marudiorudio kama inavyowasilishwa hapa chini:

#### 5.3.4.3 Marudiorudio

Mbinu ya marudiorudio ni ya kisanaa inavyotumiwa na wanafasihi katika kazi zao ili kuonesha msisitizo wa jambo au wazo fulani analotaka liifikie jamii. Kandoro katika ushairi wake ametumia marudiorudio ya aina mbalimbali kama vile marudiorudio ya

fonimu, neno na msitari. Tuanze na marudiorudio ya fonimu. Fonimu ni kitamkwa cha msingi katika neno ambacho huweza kubadilisha maana ya neno. Fonimu katika ushairi wa Kandoro huonekana kurudiwarudiwa pale anapoweka vina vya ushairi wake. Katika shairi *Kura Tatu*, anasema hivi:

*Kuwalazimisha watu, shauri wasilotaka.*
*Hiyo ni ajabu kwetu, twaifumbata twacheka,*
*Fakiri haneni kitu, mbele ya wenye madaraka,*
*Hatutaki Tanganyika, kura ya watu watatu.*

Hapa msanii anatumia vina kati na vina mwisho ambapo kina kati ni “tu” na kina mwisho ni “ka” katika mistari mitatu ya kwanza huku ule wa mwisho kina kati kikiwa na “ka” na kina mwisho ni “tu”. Msomaji wa shairi hili hupata msisitizo wa dhamira zilizopo katika ubeti huu kutokana na marudiorudio ya fonimu “ka” na “tu” pale asomapo au asikilizapo shairi hili. Sauti “ka” ni sauti ya ukali yenye kuonesha kutoridhishwa na jambo fulani ambalo ni kura tatu iliyoanzishwa na serikali ya Kikoloni. Fonimu “tu” nayo huonesha kutokukubaliana na jambo fulani lililopendekezwa na mtu mwingine. Kwa pamoja marudiorudio ya fonimu hizi humfanya msomaji kuwa mzingativu na maudhui humuingia barabara kabisa.

Marudiorudio mengine ni yale ya maneno katika beti za shairi. Hapa msanii hurudia neno zima katika ubeti si kwa makusudi bali kwa madhumuni maalumu. Katika shairi la *Kwetu ni Kwao kwa Nini* Kandoro anasema:

*Mtu huuliza nini, kitu hiki cha nini?*
*Kitu hiki ni cha nani, na kitu hiki cha nini?*
*Nacho kinaitwa nini, ni cha nani kwa nini?*
*Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini?*

Katika ubeti huu maneno “nini”, “kwetu”, na “kwao” pamoja na “nani” yanajitokeza kwa kurudiwarudiwa kwa kiasi kikubwa. Marudiorudio haya yanaonesha msisitizo kwamba, mkoloni ni lazima aondoke nchini na kuwaachia wananchi nchi yao kwa kuwa yeye mkoloni ananufaika sana na nchi hii na wazawa wakiendelea kuwa masikini kadiri siku zinavyozidi kusonga mbele.

Vilevile, Kandoro anafanya marudio ya nusu msitari katika baadhi ya mashairi yake. Katia shairi *Ondoka nchini kwetu*, anasema:

*TANU inalia sana, wote wanachama wetu,*
*Wanakulilia bwana, uondoke hapa kwetu,*
*Bwana tafadhali sana, ondoka nchini mwetu,*
*Ondoka nchini mwetu, mwishoni mwa mwaka huu,*

Kipande cha msitari *Ondoka nchini mwetu*, kimerudiwa mara mbili katika ubeti huu. Hii inaonesha msisitizo kwamba, wananchi wamechoshwa na uonevu na mabavu ya wakoloni na sasa wanataka uhuru wao. Mbinu hii ya marudiorudio imetumiwa kwa kiasi kikubwa na Kandoro katika ushairi wake. Mbinu nyingine inayotumiwa na Kandoro katika kuwasilisha maudhui ya ushairi wake ni matumizi ya wahusika kama inavyowasilishwa hapa chini.

### 5.3.5 Matumizi ya Wahusika

Wahusika ni wale ambao msanii anawatumia katika kuwasilisha maudhui kwa hadhira iliyokusudiwa. Wahusika wanaweza kuwa watu, vitu, wadudu, wanyama na madubwana. Matumizi ya wanyama na vitu hutumika katika kazi za fasihi simuizi kama vile ngano, visasili, vigano na kadhalika. Matumizi ya wahusika katika kazi za fasihi huhusishwa na utendaji wa matendo mbalimbali ambayo hupatikana katika riwaya, tamthilia na hadithi kuliko katika mashairi. Hata hivyo, wapo washairi

ambao hutumia wahusika katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa Kandoro ni miongoni mwa washairi hao. Katika shairi *Siafu wamekazana* anatumia wahusika wanyama katika kuwasilisha ujumbe. Anasema:

*Siafu wamekazana,*
*Nyoka amegutuka, ndani ya shimo katuna,*
*Tena amekasirika, hasira zenye kununa,*
*Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna,*
*Siafu amekazana, nyoka amekasirika.*

Dondoo hili linaonesha matumizi ya wahusika wanyama katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. *Nyoka* ni mkoloni na *siafu* ni wananchi ambao wanapambana katika vita ya kudai uhuru wao.

Vilevile, Kandoro anatumia wahusika wanadamu katika mashairi yake. Katika shairi la Afrika ni moja anasema:

*Nenda na nyuma ukija, Nyerere muheshimiwa,*
*Zipeleke zetu hoja, kwa nduguzo wasifika,*
*Haifai ngoja ngoja, kwani yalia Afrika,*
*Hii Afrika moja, ni nchi ya Waafrika.*

Hapa msanii anamtumia Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kuwasilisha maudhui yahusianayo na Umoja wa Afrika. Mwalimu Nyerere alikuwa kiongozi mashuhuri katika kupigania umoja wa Afrika na aliheshimika duniani kote kwa kazi hiyo. Msanii anapomtumia mhusika huyu, bila shaka inamfanya msomaji kuyapata maudhui barabara kwa kuwa mhusika mtajwa anahusika sana na yasemwayo katika shairi husika. Pia katika shairi la *Rudi Haraka* tunaoneshwa matumizi ya mhusika binadamu pale anaposema:

*Juma njoo nikutume, nenda upesi shambani.*
*Ufike uchume kunde, usiyachume mahindi,*
*Maagizo yashike, usivuruge mbaazi,*

*Rudi haraka haraka, njiani usikawie*.

Hapa Kandoro anamtumia mhusika Juma ambaye anampa maagizo mbalimbali ambayo kwayo anatoa maudhui kadhaa kwa msomaji ama msikilizaji wa shairi hili. Maudhui hayo ni kama vile jamii hii ya akina Juma inajishughulisha na Kilimo cha mazao kama vile kunde, mahindi na mbaazi ili kuendeshea maisha yao. Hivi ndivyo namna wahusika wanavyotumika katika mashairi. Mbinu nyingine ya kisanaa inayotumiwa na waandishi wa ushairi katika kujenga dhamira ni mandhari. Kandoro anatumia mandhari kama ifuatavyo:

### 5.3.6 Matumizi ya Mandhari katika Ushairi

Mandhari ni mahali ambapo kazi ya fasihi hufanyikia ili kuwasilisha maudhui kwa hadhira iliyokusudiwa kama ilivyokusudiwa na mwandishi wa ushairi husika. Matumizi ya mandhari huonekana katika riwaya, tamthilia na hadithi fupifupi. Hii haina maana kwamba, ushairi hautumii mandhari, la hasha! Kezilahabi (1983) anaeleza kwamba, kuna mandhari halisi na mandhari isiyohalisi. Kandoro anatumia mandhari halisi katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira ya ushairi wake. Kandoro anatumia mandhari ya kipindi cha ukoloni, mapambano ya kudai uhuru na baada ya kupata uhuru. Kupitia shairi lake la *Kitumike Kiswahili* anasema:

*Vitu tunavyovitaka, tupewe na Serikali,*
*Sisi ni wengi hakika, kuliko taifa mbili*
*Haki isiyo na shaka, tuzidi hata viwili,*
*Kitumike Kiswahili, baraza la Tanganyika*.

Hapa msanii anaonesha mandhari ya Kikoloni kwamba, Wafrika walikuwa ni wachache kuliko Wazungu na Wahindi katika baraza la Tanganyika. Hii ni mandhari ya Kinyonyaji kwa sababu Waafrika ndio wengi ukilinganisha na Wazungu na Wahindi lakini katika nafasi za uwakilishi wao ni wachache. Pia msanii anatoa

mandhari nzima ya baraza hilo kwamba lugha ya Kiingereza ndiyo iliyokuwa inatumika na si Kiswahili. Waafrika wengi hawakuwa na ujuzi wa kuzungungumza lugha ya Kiingereza kwa hiyo hata wawakilishi katika baraza la Tanganyika walikuwa ni watazamaji tu wasiofahamu nini kinaendelea katika mijadala mbalimbali ya baraza hilo.

Si hivyo tu, bali pia Kandoro anatumia mandhari ya uhaba wa bidhaa baada ya kupatikana kwa uhuru. Hali hii iliwafanya wananchi kuishi maisha magumu kwa kukosa baadhi ya bidhaa muhimu walizozihitaji katika kuendeshea maisha yao. Kandoro anasema:

*Muheshimiwa katamka, ndiye Nyerere Mwalimu,*
*Vibiriti vitawaka, na mengine ya muhimu,*
*Uhuru tumeushika, ujenzi watulazimu,*
*Ametamka Mwalimu, vibiriti vitawaka.*

Kitendo cha mwalimu kutoa tamko kama hili kinaonesha kwamba, kulikuwa na tatizo la uhaba wa bidhaa muhimu katika maisha ya wananchi. Hata hivyo, baada ya muda kupita tatizo hilo lilitatuliwa na vibiriti pamoja na bidhaa nyingine zikaanza kupatikana kwa wingi na urahisi kwa wananchi wote. Pia katika shairi hili tunaoneshwa mandhari ya Tanganyika kiuchumi na kijamii ilikuwa duni sana wakati huo na ilihitajia kujengwa upya hasa pale anaposema: *Uhuru tumeushika, ujenzi watulazimu*. Ujenzi wa jamii mpya ulifanyika na kwa kiasi fulani maendeleo yalipatikana ingawa kulikuwa na mapungufu ya hapa na pale. Mbinu nyingine ya kisanaa anayotumia Kandoro ni ile ya lugha ya mkato.

### 5.3.7 Matumizi ya Lugha ya Mkato

Lugha ya mkato ni ile ambayo neno halitajwi likamaliziwa bali hufupishwa ili kupatikana kwa vina na mizani ya mashairi ya mshairi husika. Kandoro anatumia lugha ya aina hii kwa kiasi fulani katika ushairi wake. Kwa mfano, katika shairi la *Tumshukuru Manani,* anasema:

> *Shuleni hatukutiwa, ili tuwe ujingani,*
> *Fasi hatukupatiwa, kutiwa utajirini*
> *Kutwa kucha huzomewa, kama majitu haini.*

Katika ubeti huu neno, “fasi” hatukupatiwa kutiwa utajirini limetumiwa kwa kufupishwa. Hii ina maana kwamba, neno “fasi” lilipaswa kuwa “nafasi” lakini ili kupata vina na mizani linalazimika kuandikwa kwa mkato. Pamoja na kuandikwa kwa mkato namna hiyo lakini bado linatoa maana iliyokusudiwa kwa wasomaji wake. Matumizi ya lugha ya mkato humvuta msomaji na kumfanya awe makini na pengine kulirudia neno hata zaidi ya mara moja ili alielewe hasa lina maana gani? Neno linapokuwa limeandikwa kwa mkato kama hilo huonekana kuwa si neno la kawaida. Msomaji anapasoma kwa mara ya kwanza na kukutana nalo atasimama kidogo na kisha kulisoma tena na tena na kisha kulihusisha na maneno mengine ili kupata dhamira mbalimbali. Neno “fasi” limetumika kuonesha kwamba, Wafrika hawakupewa nafasi na fursa ya kupata elimu katika shule za serikali na hivyo kubakia mbumbumbu wasio na mbele wala nyuma. Hata baada ya kupatikana kwa uhuru ilibidi nafasi nyingine za uongozi ziendelee kushikiliwa na Wazungu mpaka hapo wasomi wazalendo walipopatikana. Vilevile, matumizi ya neno hili la mkato yanaonesha kwamba elimu iliyotolewa katika enzi za ukoloni ilikuwa ni ya kitabaka. Wazungu na Wahindi hasa ndio waliopata elimu pamoja na watoto wa machifu. Hali

hii imechangia kurudisha nyuma maendeleo ya taifa na wananchi wake kwa ujumla. Mbinu nyingine inayotumiwa na Kandoro ni mwingiliano matini kama inavyoelezwa hapa chini.

### 5.3.8 Mwingiliano Matini

Wamitila (2008) anaeleza kwamba mazungumzo ya kifasihi yanasisitiza jinsi ambavyo kazi za kifasihi zinavyohusiana, kuumbana na hata kuchangamana. Fasihi inaweza kupatikana tu kwa kuwa pamekuwapo na fasihi ulimwenguni, yaani fasihi inatokana na fasihi yenyewe. Kwa mfano, mtunzi wa ushairi hawezi kuandika ushari bila ya kuwa na picha na taswira ya ushairi uliotangulia. Huu ni msingi mpana wa kimwingiliano matini. Msingi finyu ni pale ambao ushairi unaohusika unahusiana na kuingiliana na riwaya nyingine inayojulikana. Kandoro alipenda kuufananisha ushairi wake na ule wa Muyaka. Hali hii ilimfanya Kezilahabi (1977) kueleza kwamba, Kandoro anamwiga Muyaka katika utunzi wake wa mashairi. Hata hivyo, Kandoro hakuwahi kuiga ushairi wa Muyaka bali ni mwingiliano wa matini uliopatikana baada ya Kandoro kusoma mashairi ya Muyaka na hiyo kujikuta anaandika mashairi yake kama mshairi huyu mashuhuri katika enzi zake. Ili kuonesha kwamba Kandoro alikuwa msomaji mzuri wa ushairi wa Muyaka, katika shairi la *Siyo Insha Mashairi*, anasema:

*Muyaka Ali ni shani, kwa tungo za mashairi,*
*Huyanena kwa mighani, popote akidhihiri,*
*Akiwatia imani, masikini na tajiri,*
*Siyo Insha mashairi, ninakataa katani.*

Hapa Kandoro anamsifu Muyaka kwamba, ni mtunzi mashuhuri na mtalaamu katika utunzi wa mashairi na kwamba mashairi yake yalikuwa yanaimbika kwa hivyo

yalikuwa na vina na mizani. Kwa hivyo Kandoro aliendelea kutunga mashairi yenye urari wa vina na mizani katika maisha yake yote na yeyote aliyeandika shairi lisilofuata urari wa vina na mizani alimuona kuwa si mtunzi wa ushairi. Mawazo haya yalifanana na ya Mayoka ambaye anasema:

*Unapotaka kutunga, kwanza upate mawazo,*
*Jambo lililo kutunga, furaha au chukizo,*
*Ndipo beti utapanga, ziwe chache au mzo,*
*Ushairi ni Mawazo, Vina pamwe na mizani.*

Si hivyo tu katika ushairi wa Kandoro kuna matini zinazohusu uchumi siasa jamii na utamaduni. Kwa mfano, katika ubeti huu hapa chini anazungumzia masuala ya viwanda na biashara anasema:

*Mheshimiwa katamka, ndiye Nyerere Mwalimu,*
*Vibiriti vitawaka, na mengine ya muhimu,*
*Uhuru tumeushika, ujenzi watulazimu,*
*Ametamka mwalimu, vibiriti vitawaka.*

Hapa Kandoro, anazungumzia masuala ya kuanzisha viwanda vya kuzalisha vibiriti pamoja na bidhaa nyingine ili kuwapatia wananchi maisha bora na yenye kuridhisha. Haya ni masuala ya uchumi na si fasihi lakini yameelezwa kupitia ushairi-huu ndio muingiliano matini tunaouzungumzia. Kwa kutumia mwingiliano matini Kandoro ameufanya ushairi wake kuwa hai na wenye kueleza masuala yanavyowagusa wananchi katika maisha yao ya kila siku. Mbinu nyingine inayotumiwa na Kandoro katika kusawiri masuala ya kisiasa katika jamii ni ile ya mazungumzo kama inavyoelezwa hapa chini.

### 5.3.9 Mbinu ya Mazungumzo katika Ushairi

Kwa kawaida mazungumzo hufanywa baina ya mtu na mtu ama mtu na kikundi na kadhalika. Kandoro amekuwa akitumia mbinu hii hasa katika mashairi aliyokuwa

akiandikiana yeye na Mwalimu Nyerere. Katika shairi la Nyerere Pokea *hicho anasema*:

> *Linda sasa nchi yako, pokea uizatiti,*
> *Ufute machozi yako, uketi ushike kiti,*
> *Na mawaziri wenzako, mshike nchi kwa dhati,*
> *Nyerere kalia kiti, uichunge nchi yako*!

Kandoro kwa kukupitia njia ya mazungumzo anamtaka baba wa taifa mwalimu Julius Nyerere kuhakikisha kwamba, anaiongoza nchi vizuri kama inavyopasa ili kuwaletea wananchi maendeleo. Anamtaka pia ahakikishe kwamba mawaziri alionao ni wachapa kazi na wenye uadilifu uliotukuka. Hii ina maana kwamba, mawaziri ndio wasaidizi na washauri wakubwa wa Rais hivyo wakikosa uadilifu nchi itaenda mrama.

Vilevile, Kandoro anamtaka Mwalimu Nyerere kuilinda nchi dhidi ya ukoloni mamboleo. Mwalimu naye alionekana kwa kiasi kikubwa akitenda kama alivyotakwa na Kandoro katika shairi husika. Kwa mfano, katika enzi ya utawala wake alikataa katakata kuruhusu mabepari kupitia jina la uwekezaji kuchimba madini ya aina mbalimbali yanayopatikana nchini. Mwalimu aliahidi kwamba, uchimbaji wa madini hayo utafanyika katika kipindi nchi itakapokuwa imejenga uwezo wake wa kuwa na wataalamu wa kutosha katika sekta hiyo ya madini. Alifanya maamuzi haya kwa sababu alifahamu kwamba, iwapo madini yatachimbwa katika kipindi ambacho hatuna wataalamu basi ni dhahiri kwamba madini hayo yatawanufaisha wawekezaji wa kigeni kuliko wananchi wa Tanganyika. Mbinu nyingine ya kisanaa ni ile ya muundo kama inavyoelezwa hapa chini.

### 5.3.10 Muundo katika Ushairi wa Kandoro

Njogu na Chikerah (1999) wanaeleza kwamba; kuna miundo mingi katika ushairi wa Kiswahili. Vipengele vingi vinavyotumika kama sehemu ya muundo ni mishororo (mistari) beti mizani na vina. Urefu wa mshororo hutegemea idadi ya mizani au mtiririko wa mawazo, kama ni shairi huru urefu wa beti nao wategemea idadi ya mistari katika kila beti. Kandoro ametumia aina mbalimbali za muundo ambapo muundo wa tarbia ndio uliotawala katika mashairi yake yaliyo mengi. Muundo wa tarbia ni ule ambao shairi hutumia mistari minne katika kila ubeti wa shairi kwa mfano: Katika shairi la *Mchechema Chechemea*, Kandoro anaandika hivi:

*Ndiyo hiyo patashika, tunayoitegemea,*
*Mchechemo umefika, ule tulo usemea,*
*Chechema ukinemeka, mwanangu mchechemea,*
*Mchechema chechemea, chechemea kuneemeka*.

Ubeti huu wa shairi umeundwa kwa kutumia mistari minne ambayo hulifanya shairi hili kuitwa tarbia. Muundo huu umemwezesha mtunzi kuwasilisha maudhui kwa hadhira iliyokusudiwa kwa udhati wake. Katika ubeti huu Kandoro anawataka wananchi kuwa wavumilivu na watulivu katika kipindi kigumu cha kujenga taifa. Ujenzi wa jamii mpya sio kazi rahisi una vikwazo vingi vya hapa na pale lakini taratibu vikwazo hivyo vitatatuliwa na kisha kuweza kujiletea maendeleo endelevu.

Vilevile, Kandoro ametumia muundo wa tathilitha yaani ubeti wa shairi wenye mistari mitatu. Mfano huu tunaupata katika shairi la *Tumshukuru Manani* anaandika:

*Shuleni hatukutiwa, ili tuwe ujingani,*
*Fasi hatukupatiwa, kutiwa utajirini,*
*Kutwa kucha huzomewa, kama majitu haini*.

Ubeti huu umeundwa kwa kutumia mistari mitatu ambayo kwayo Kandoro anaeleza namna elimu ya kipindi cha ukoloni ilivyotolewa kwa ubaguzi. Ubaguzi huu uliwalenga Waafrika ambao walinyimwa fursa ya kusoma ili wafute ujinga na kujiletea maendeleo.

Miundo hii miwili ya idadi ya mistari tulioiona imepambwa pia kwa urari wa vina na mizani. Aidha ni tarbia au tathlitha, vina na mizani ndiyo pambo lake kuu. Kandoro anaeleza kwamba, shairi ambalo limeundwa kwa beti zisizo na mizani katu haliwezi kuitwa shairi la Kiswahili. Kwa kuwa yeye anatunga ushairi wa Kiswahili basi ni lazima shairi hilo liwe na urari wa vina na mizani. Kwa mfano katika shairi *Haki Huvunja Mlima* anaandika:

*Hakika nimebaini, walimu walivyosema,*
*Edita usinihini, shairi litoe hima,*
*Kiongozi wa jeshini, haiogopi lawama,*
*Haki huvunja milima, niliambiwa shuleni.*

Ubeti huu umepambwa kwa mizani 16 katika kila msitari na vina kati "ni" na vina mwisho ni "ma". Vina hivi huonesha msisitizo ambao mtunzi hutaka wasomaji wake waupate. Katika ubeti huu mshairi anaeleza kwamba, haki ya mtu huwa haipotei na mpigania haki huwa haogopi kufa.

Kimsingi, muundo kama mbinu ya kisanaa inayotumiwa na wasanii wa ushairi inaweza kujitokeza na kuelezwa kwa namna tofauti tofauti ila kwa upande wetu tumeeleza kwa ufupi tu ili kukidhi malengo ya utafiti wetu. Hata hivyo, tunakiri

kwamba hatuwezi kuueleza muundo wote anaoutumia Kandoro katika tasinifu hii kwa kuwa si lengo la utafiti wetu. Tunasema hivyo kwa sababu yapo mashairi ambayo ametumia mistari mitano na mengine sita na kuendelea. Aina nyingine ya mbinu ya kisanaa anayotumia Kandoro ni ile ya Mtindo kama inavyowasilishwa hapa chini.

### 5.3.11 Mtindo katika Ushairi wa Kandoro

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kwamba, hakuna njia moja ya kueleza neno mtindo. Lakini, kwa ujumla twaweza kusema kwamba, "mtindo ni tabia ya utungaji inayompambanua mtunzi mmoja na mwingine." Kandoro ni mtaalamu katika matumizi ya mitindo mbalimbali katika ushairi wake. Katika mengi ya mashairi yake anatumia misemo na methali. Haya tunayaona katika shairi la *Msiogope Mawimbi* anasema:

*Majini hamjatiwa, msijipige mikambi,*
*Ngalawa kutimuliwa, msiogope mawimbi,*
*Liko liloteuliwa, Kongo si ardhi mbi,*
*Msiogope mikambi, ndio mwendo wa ngalawa*.

Katika dondoo hili msanii anaonesha uwezo wake wa kutumia misemo mbalimbali kama vile "majini hamjatiwa, msijipige mikambi" na "msiogope mawimbi, ndio mwendo wa ngalawa". Misemo yote hii imelenga kuwaandaa Watanzania wasiogope kupigania haki zao kutoka kwa mkoloni. Ni vema wakaendeleza juhudi za kudai uhuru wao ili waupate na kisha waweze kuandaa mipango na mikakati maridhawa ya kupambana na hima mbalimbali za maisha. Pia katika misemo hii tunaona kwamba, imetumika lugha ya mafumbo, taswira na picha. Huu pia ni mtindo mwingine anaoutumia Kandoro. Anaposema *msiogope mawimbi, ndio mwendo wa ngalawa*

anamaanisha kwamba, mawimbi ni hima mbalimbali za maisha ambazo zimepatikana baada ya wakoloni kuiacha nchi mikononi mwa wananchi baada ya kupatikana kwa uhuru. Hima hizo ni kama vile hali ngumu ya maisha, maradhi, njaa, umasikini, na ujinga. Anaposema ndio *mwendo wa ngalawa* anamaanisha kwamba, msukosuko katika harakati za kujitawala na kujiletea maendeleo ni suala la kawaida na haipaswi kukata tamaa dhidi yake. Matumizi ya lugha ya namna hii ni nadra kuyapata kwa watunzi wengi wa ushairi wa Kiswahili.

Vilevile, tunamwona Kandoro akitumia mtindo wa kuchanganya ndimi hasa pale anapotumia msamiati wa Kiarabu katika ushairi wa Kiswahili. Kwa mfano, katika shairi *Mungu Shule Ibariki* anasema:

*Mungu Shule ibariki,*
*Itoe watoto wema, wasio wabaramaki,*
*Wawe watoto ulama, wasiwe wenye hamaki,*
*Wenye nguvu za kusoma, kuipigania haki,*
*Mungu shule ibariki, itoe watoto wema.*

Katika dondoo hili tunaona katika msitari wa tatu Kandoro anatumia neno “Ulama” akimaanisha wasomi ama usomi wa hali ya juu kabisa. Kutumiwa kwa neno hili katika ubeti huu kunaufanya ubeti kuwa hai na kuitoa maana ya shairi kama inavyopaswa.

Pia Kandoro ametunga mashairi yake katika mtindo wa kila shairi kuwa na kituo ambacho kinafanana kwa shairi zima. Mtindo huu humfanya msomaji kupata msisitizo juu ya kile kinachosemwa na msanii. Kwa mfano, katika shairi la *Unyonge umeondoka*, anasema:

*Nafurahika nacheka, cheko yangu ya fundira,*
*Nacheka narukaruka, Ghanima yangu tijara*
*Unyonge umeondoka, koloni kulipurura,*
*Kwetu Tanzania bora, unyonge umeondoka.*

Kibwagizo cha ubeti huu kinajirudiarudia katika beti zote kumi za shairi zima. Kupita marudiorudio haya msomaji hukumbushwa na kufahamishwa kuhusu maudhui na dhamira zinapopatikana katika shairi hili. Mtindo huu ni muhimu katika kutolea msisitizo wa dhamira na maudhui ya shairi husika kwa wasomaji wake. Kwa ujumla hii ni baadhi tu ya mitindo ambayo inatumiwa na Kandoro katika kuwasilisha dhamira za kisiasa katika ushairi wake kama ilivyowasilishwa hapo juu. Mbinu nyingine inavyotumiwa na Kandoro ni usimulizi. Mbinu hii inatolewa maelezo hapa chini kama ifuatavyo:

### 5.3.12 Usimulizi Katika Ushairi wa Kandoro

Usimulizi unahusishwa kwa kiasi kikubwa na tanzu za riwaya, tamthiliya na hadithi fupi. Hata hivyo, hii haina maana kuwa hakuna usimulizi katika ushairi. Tungo za kishairi ambazo zinahusishwa na usimulizi ni tenzi na tendi. Lakini inawezekana mashairi mafupi ya beti kadhaa yakawa na sifa hii ya usimulizi (Wamitila, 2008:247). Usimulizi ni sauti ya uwasilishaji wa jambo kama vile hadithi, ushairi, riwaya na kadhalika, Kandoro ametumia usimulizi wa nafsi mbalimbali katika uwasilishaji wa maudhui katika ushairi wake. Kwa mfano, katika shairi la *Kura Tatu*, Kandoro anatumia usimulizi wa nafsi ya kwanza wingi pale anaposema:

*Kuwalazimisha watu, shauri wasilotaka*
*Hiyo ni ajabu kwetu, twajifumbata twacheka,*
*Fakiri haneni kitu, mbele ya wenye madaraka,*
*Hatutaki Tanganyika, Kura ya watu Watatu.*

Maneno kama vile "*kwetu*", "*twajifumbata*", "*twacheka*" na "hatutaki", yanasimama kuwasilisha nafsi ya kwanza wingi yaani "sisi". Matumizi ya usimulizi wa nafsi ya kwanza wingi hulifanya shairi kuwa na uzito zaidi katika maudhui yake. Nafsi ya kwanza wingi hulifanya shairi kuwa na uzito. Zaidi katika maudhui yake kwa sababu inaonesha wingi wa watu wanaopinga suala la kura tatu.

Vilevile, tunaona utumizi wa nafsi ya pili umoja katika shairi la *Soma Sana kwa bidii* anasema:

> *Kusoma ni nuru yako, asomaye hafifii,*
> *Kusoma ni sifa zako, jina halikuwalii.*

Maneno kama vile "yako na zako" yanasimama kuwasilisha usimamizi wa nafsi ya pili umoja yaani "wewe". Hapa Kandoro anamtaka kila mtu kuhakikisha kwamba, anasoma ili apate elimu itakayomkomboa katikt maisha yake. Kwa kutumia nafsi hii, Kandoro hajabagua watu katika jamii. Wawe watoto, vijana, wazee, akina mama, dada na kadhalika wote wametakiwa kusoma, kwa bidii ili wawe na maisha bora. Kwa ufupi, hivi ndivyo namna usimulizi wa nafsi unavyojitokeza katika ushairi wa Kandoro. Zipo aina nyingine za nafsi, zinazojitokeza katika ushairi wa Kandoro ila kwa minajili ya utafiti huu inatosha kuishia hapa.

### 5.3.13 Muhutasari

Sehemu hii ililenga kujibu swali la upili la utafiti wetu lililokuwa likiuliza juu ya mbinu za kisanaa zinazotumiwa na Kandoro katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Ujumbe huo ni ule unaohusu masuala ya kisiasa. Kwa msingi huu basi, tumeweza kuonesha mbinu mbalimbali kama vile, matumizi ya lugha; ambapo tumeona uchanganyaji wa lugha; Kiswahili Sanifu na tamathali za usemi, kama vile

tashihisi, taswira, ishara na marudiorudio. Vile vile, tumeona matumizi ya wahusika, mandhari, lugha ya mkato, mwingiliano matini na mbinu ya mazungumzo. Pia tumeonesha mbinu nyingine kama matumizi ya muundo, mtindo na usimulizi. Mbinu hizi kwa hakika zimesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuibua dhamira na maudhui ya kisiasa katika ushairi wa Kandoro.

## 5.4 Falsafa Katika Ushairi wa Kandoro

Dhumuni mahususi la tatu la utafiti huu lililenga kubainisha falsafa ya Saadan Kandoro kama inavyojitokeza katika ushairi wake. Sehemu hii inafanya uchambuzi na uwasilishaji wa kina kuhusu falsafa ya Kandoro. Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kwamba:

> *Neno hili "falsafa" limetoholewa kutokana na neno la Kiingereza philosophy" kupitia kwa neno la Kiarabu, "falsafa." Kwa Kilatini, Philla ni harakati na Sophia ni busara. Kwa hiyo falsafa ni busara iliyofikiwa baada ya mtu au watu kutafakari kwa kina kuhusu jambo lolote la kilimwengu. Ni busara inayotokana na harakati ya kimawazo.*

Kandoro alikuwa ni mwanaharakati mpigania uhuru ambayo ndiyo ilikuwa falsafa yake. Kandoro aliamini kwamba, maendeleo ya kweli yatapatikana pale tu wakoloni watakapoondoka nchini na kuipatia Tanganyika na watu wake uhuru. Falsafa hii inajitokeza katika mengi ya mashairi yake hasa lile la *Kwetu ni kwao kwa Nini*. Katika shairi hili, mshairi anashangaa kuona wakoloni waking'ang'ania kutawala na kunyonya rasilimali za wananchi kwa masilahi yao wao wenyewe. Kwa hali hiyo anawataka kuondoka nchini na kutoa uhuru kwa wananchi ili waweze kujitawala wenyewe na kujileta maendeleo. Falsafa ya Kandoro kuhusu uwanaharakati inaonekana katika shairi hili:

*TANU inalia sana, wote wanachama wetu,*
*Wanakulilia, bwana, Uondoke hapa kwetu,*
*Bwana tafadhali sana, Ondoka nchini mwetu,*
*Ondoka nchini mwetu, mwishoni mwa mwaka huu.*

Ukitazama dondoo hili kwa makini utabaini kwamba, Kandoro ni mwanaharakati ambaye bila kujali wala kuogopa anamueleza mkoloni kwamba, aondoke nchini na kutoa uhuru kwa wananchi. Anatumia lugha kali ya kumfukuza mkoloni na si kumuomba aondoke nchini. Anatumia msamiati "Ondoka", ambao bila shaka ni wa kumfukuza kabisa mkononi. Falsafa hii inaonekana pia katika mashairi mengi pale anaposema kwamba, yeye yupo tayari kufa masikini lakini ahakikishe kwamba nchi inakuwa huru.

Aina nyingine ya falsafa inayojitokeza katika ushairi wa Kandoro ni ile ya Utu. Kandoro kama ilivyo kwa Shaaban Robert katika *Utu Bora Mkulima* na *Siku ya Watenzi Wote* anazungumzia umuhimu wa kutukuza na kuujali utu wa mwanadamu. Kandoro anaona kwamba, utu wa Mtanganyika ulidumishwa sana na serikali ya kikoloni kutokana na kumtumikisha mwananchi bila kumpatia malipo stahiki ya kile alichokifanya katika kumzalishia mali mkoloni. Vilevile, mwananchi alinyimwa fursa ya kupata huduma muhimu kama vile afya, elimu, maji, barabara na kadhalika. Baada ya kupatikana kwa uhuru Kandoro anaitaka Serikali kuhakikisha kwamba, inawajali wananchi kwa kuwapatia huduma muhimu kama vile elimu, maji, afya, barabara na bidhaa nyingine muhimu kwa mahitaji ya wananchi. Kwa mfano, katika shairi, *Ametamka Mwalimu, viberiti vitawaka*, anasema:

*Muheshimiwa katamka, ndie Nyerere Mwalimu,*
*Vibiriti vitawaka na mengine ya muhimu,*
*Uhuru tumeushika, ujenzi watulazimu,*
*Ametamka mwalimu, vibiriti vitawaka.*

Katika ubeti huu tunaipata falsafa ya utu ikielezwa na Kandoro. Kandoro anaona kwamba, ipo haja kwa kila mwananchi kupata huduma bora ili aweze kuendesha maisha yake ipasavyo. Serikali ya kikoloni haikuwapatia wananchi huduma muhimu na hivyo kuwafanya kuiishi maisha ya taabu. Suala hili lilimpa taabu Kandoro na hivyo kutamani siku moja mambo yatakuwa mazuri baada ya nchi kupata uhuru. Hapa matumaini ya Kandoro yanaonekana kufanikiwa baada ya kiongozi mkuu wa nchi kutamka kwamba maisha yatakuwa mazuri katika ubeti mwingine anasema:

*Ukoloni kukumbuka, sisi kwetu ni adimu,*
*Kukumbuka kuadimika, ndio yetu maalumu,*
*Bendera tumesimika, ndilo letu la muhimu*
*Ametamka Mwalimu, vibiriti vitawaka.*

Kandoro anasema kwamba, kuukumbuka ukoloni ni mwiko kwa sababu haukuwa unajali utu wa Mwafrika. Mwafrika alichukuliwa kama mtu asiyefaa katika jamii hali ya kuwa ndiye aliyekuwa mzalishaji mali mkuu wa kuwanufaisha wakoloni. Katika shairi la *Tumshukuru Manani* anasema:

*Shuleni hatukutiwa, ili tuwe ujingani,*
*Fasi hatukupatiwa, kutiwa utajirini,*
*Kutwa kucha huzomewa, kama majitu haini.*

Mwafrika alionekana kama mtu haini, yaani mtu muovu, mtukutu na mkorofi asiyestahili kupewa heshima ya aina yoyote ile ndio maana hata shuleni hakutiwa. Hii yote inaonesha ni namna gani wakoloni walivyokuwa hawajali utu wa Mwafrika. Suala la Mwafrika kunyimwa nafasi ya kupata elimu ni kinyume na utu wa mwanadamu. Baada ya kupatikana kwa uhuru Kandoro ana wahimiza wananchi kuhakikisha kwamba, wanasoma kwa bidii ili hatimaye wasionekane kuwa ni majitu

haini bali watu wanaostahili heshima na hadhi katika maisha yao. Hili lilifanikiwa kwa kiasi kikubwa sana pale serikali ya Tanganyika ilipotoa elimu bure kwa watu wake.

Vilevile, katika falsafa yake ya utu anapigania usawa wa mwanadamu. Kandoro ana waona binadamu wote kuwa ni sawa na hakuna aliye na haki zaidi ya mwingine. Anaona kwamba, kama wanadamu wote ni sawa basi wanastahili haki sawa katika mambo mbalimbali likiwemo lile la kushirikishwa katika maamuzi. Haya tunayaona katika shairi la *Kura Tatu* pale anaposema:

*Kura moja kwa watatu, watu gani wametaka,*
*Hajure kura kwa mtu, kura moja tunataka,*
*Ili tuchague watu kwa kura isiyo mipaka,*
*Hatuitaki Tanganyika, kura ya watu watatu*.

Uamuzi wa kwamba, kila mwananchi apige kura tatu katika uchaguzi wa wabunge ulifanywa na watu wachache tena Wakoloni wenyewe. Kandoro alikera na uamuzi huu ambao haukuwashirikisha wananchi kwa kuwa walionekana mbele ya wakoloni kama watu wasiokuwa na umuhimu katika jamii. Suala hili linaenda kinyume na misingi ya utu wa mwanadamu. Katika kuonesha kwamba Kandoro ni mtu anayejali na kuheshimu utu wa binadamu wote, anasema:

*Twadai tarehe yetu, kutawala, Tanganyika,*
*Twaomba uhuru wetu, ndio tunaoutaka,*
*Haki zenu na za kwetu, tutalinda bila shaka,*
*Hatutaki Tanganyika, kura ya watu watatu*.

Pamoja kwamba Kandoro anafahamu fika kwamba, wakoloni hawakuwa watu wema kwa Waafrika na kwamba, waliwatendea manyanyaso mengi bado anasema kwamba

hata uhuru ukipatikana haki za wakoloni nazo pia zitalindwa. Hiki ni kipimo cha hali ya juu kabisa cha utu wa mwanadamu.

Pia, falsafa ya Kandoro inajikita katika Ujamaa na Kujitegemea. Falsafa hii inajitokeza sana katika kitabu chacke cha *Liwazo la Ujamaa*. Kandoro anaamini kwamba, maendeleo ya kweli yatapatikana pale tu wananchi watakapoweza kujitegemea katika nyanja zote za maisha. Katika shairi la *Liwazo la Ujamaa* anasema:

*Natoa liwazo la Ujamaa,*
*Watalipenda wale jamaa,*
*Sio wale watu walokomaa*
*Katika dhuluma wazitendazo.*

Katika shairi hili Kandoro anaonesha kwamba, ujamaa ni jambo zuri ambalo kwalo dhuluma itakomeshwa. Hata hivyo, anakiri kwamba, wale waliokomaa katika dhuluma watalipiga vita *Azimio la Arusha*. Watalipiga vita ili waendelea kuwanyonya wanajamii wenzao. Kandoro katika kuhakikisha kwamba Azimio linafanikiwa anasema:

*Tushikamane kushikamana,*
*Tudumishe penzi la Ujamaa,*
*Hata kila siku Jumapili na Ijumaa,*
*Dua zetu wote ziwe ni nguzo.*

Hapa Kandoro anawataka waumini kuliombea dua kwa Mwenyezi Mungu Azimio la Arusha ili lidumu na likubaliwe na wananchi wote. Wale wachache wanaolipinga washindwe kutimiza azma yao kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Kandoro hakuishia kumuomba Mungu pekee bali pia kutoa elimu ya ujamaa kwa wananchi ili waweze kufahamu sifa za ujamaa pamoja na faida zake. Anasema:

*Mjamaa elimisha, Ujamaa ulioko,*
*Kuneemesha maisha ya wenzako na ya kwako,*
*Mpaka yatakapoisha, uende kwa mola wako,*
*Mjamaa kazi yako kutuongoza maisha*.

Katika beti hizi Kandoro anaonesha kwamba, mjamaa ni lazima awafundishe wananchi wenzake faida za Ujamaa na Kujitegemea ili waweze kulikubali Azimio la Arusha. Kandoro hakupenda nguvu itumike katika kuwalazimisha wananchi kulikubali Azimio la Arusha na siasa zake. Baadala yake itumike elimu katika kuwahamasisha wananchi kulikubali na kutekeleza Azimio la Arusha.

Si hivyo tu bali pia, falsafa ya wema na upendo inajitokeza katika mashairi mbalimbali ya Kandoro hasa yale yanayopatikana katika *Liwazo la Ujamaa*. Kandoro anasema kwamba:

*Kwetu ni aibu sana, watoto wa ujamaa,*
*Iwapo wajibizana, na sura zikadumaa,*
*Vipaji kukunjiana, hao si wana jamaa,*
*Watoto wa ujamaa, hucheza wakipendana*.

Katika ubeti huu Kandoro anawaasa wananchi kuhakikisha kwamba, wanahurumiana na kupendana katika maisha yao ya kila siku. Itakuwa ni jambo la aibu kuwakuta wananchi wanapoteza muda wao kubishana na kuzozana juu ya mambo ambayo hayana faida kwao. Kwa kufanya hivyo wanaweza kupoteza upendo baina yao na kuonana kama maadui.

## 5.5 Muhutasari

Ushairi wa Kandoro umesheheni falsafa mbalimbali kuhusu maisha. Kwanza kabisa, falsafa ya uwanaharakati (mapinduzi) yaani kuleta mabadiliko katika jamii ndiyo

hasa inayojitokeza katika ushairi wa Kandoro. Falsafa hii inaonekana pale ambapo Kandoro anawataka wananchi kusimama kidete katika kuhakikisha kwamba, mkoloni anaondoka nchini na kuifanya nchi kuwa huru. Falsafa nyingine ni ile ya utu wa mwanadamu ambayo pia inajitokeza katika mashairi ya Kandoro. Hii inajitokeza pale Kandoro anaponadi kwamba, watu wote ni sawa na wanastahili kupatiwa haki zao za msingi. Vilevile, Kandoro anazungumza juu ya Ujamaa na Kujitegemea pamoja na wema, upendo na mshikamano katika jamii.

# SURA YA SITA

# MUHUTASARI, HITIMISHI NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari, hitimishi pamoja na mapendekezo ya tafiti za baadaye. Katika muhtasari sura zote sita za tasnifu hii zinapitiwa kwa muhtasari ili kufupisha mambo zinayoyaeleza. Katika hitimishi, tumepitia madhumuni mahususi ya utafiti huu na kuonesha kwamba ni matokeo gani yamepatikana kwa muhtasari. Kwa upande wa mapendekezo; tumetoa mapendekezo ya tafiti za baadaye ambazo wanataaluma mbalimbali wanaweza kuzifanya katika ngazi mbalimbali za Umahiri na Uzamivu. Kwa kuanza tunaanza na muhtasari wa Tasinifu.

## 6.2 Muhtasari

Tasinifu hii imeundwa kwa sura sita na kila sura ina mada kuu na ndogo ndogo ambazo kwazo zimekamilisha utafiti huu. Sura ya Kwanza imeeleza juu ya mambo ya msingi ambayo kwayo dira na muelekezo wa utafiti ukaweza kupatikana. Miongoni mwa mambo ama vipengele vilivyowasilishwa katika sura hii ni pamoja na mada ya utafiti, usuli wa mada, usuli wa tamko la Utafiti, tamko la tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti; madhumuni mahususi, na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo na utatuzi wa vikwazo vya utafiti, mpangilio wa tasinifu na mwisho ni muhtasari. Sura hii kwa ujumla imeweza kutoa haja ya kufanyika kwa utafiti huu kwa sababu imeweza kuonesha kwamba, ushairi wa Kandoro haujafanyiwa utafiti wa kina katika masuala ya kisiasa yatokezayo katika kazi zake za ushairi.

Baadae ilifuata sura ya pili. Sura hii imefanya kazi ya kupitia kazi tangulizi kuhusiana na ushairi kwa ujumla na badaye ushairi wa Kandoro huku masuala ya kisiasa yakizingatiwa. Mambo yaliyowasilishwa katika sura hii ni ufafanuzi wa dhana mbalimbali kama vile dhana ya ushairi, ushairi wa Kiswahili, dhana ya shairi, siasa, sitiari, ishara, na taswira. Vipengele vingine ni siasa katika ushairi kwa ujumla, siasa katika ushairi wa Kandoro, historia fupi ya Kandoro na muhtasari wa sura hii. Sura imeonesha kwamba, hakuna utafiti wa ngazi ya umahiri na kuendelea uliofanywa katika ushairi wa Kandoro kwa misingi ya kifasihi isipokuwa ule wa Kitogo (2002) uliofanywa kwa misingi ya taaluma za maendeleo. Hali hii imedhihirisha pengo la utafiti ambalo kwalo ndilo lililomshughulisha mtafiti wa tasinifu hii.

Sura ya tatu imewasilisha nadharia tatu zilizotumika katika utafiti huu. Nadharia hizo ni Simiotiki, Umarx na Ufeminist. Nadharia ya Simiotiki imetoa mwongozo katika kufafanua lugha ya picha ishara, taswira na sitiari mbalimbali zilizotumiwa na Kandoro katika ushairi wake. Ni katika aina hiyo ya lugha ndipo masuala ya kisiasa yalipofichwa na Kandoro. Nadharia ya Umarx imetusaidia katika kuianisha harakati za Kitabaka zinazojitokeza katika ushairi wa Kandoro pale wananchi walipokuwa wanadai uhuru wao kutoka kwa mkoloni. Nadharia ya Ufeministi kwa upande wake imetusaidia katika uchambuzi wa masuala ya kijinsia yanayojitokeza katika ushairi wa Kandoro.

Sura ya nne imeasilisha mbinu na njia za utafiti. Njia na mbinu hizo ni pamoja na usanifu wa tasinifu, watafitiwa, usampulishaji wa watafitiwa, vyanzo vya data na taarifa; data za msingi, na data za upili. Vilevile, mbinu za ukusanyaji wa data;

uchambuzi wa kimaudhui na usaili ndizo zilizotumika. Katika uchambuzi wa data, mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo pamoja na mkabala wa kidhamira ndizo hasa zilizotumiwa na mtafiti katika kuchambua data kama zinavyoonekana katika sura ya tano ya tasinifu hii. Vipengele vingine ni uhalali na kuaminika kwa data za utafiti. Vipengele vya mwisho ni maadili ya utafiti na muhtasari wa sura hii.

Sura ya tano ya tasinifu hii ndiyo iliyowasilisha na kuchambua data za utafiti. Miongoni mwa mambo yaliyowasilishwa katika sura hii ni pamoja na Kandoro na harakati za kupigania uhuru, Kandoro mhamasishaji wa kisiasa, Kandoro na masuala ya Haki na Kandoro na umiliki wa ardhi. Mambo mengine ni Kandoro na suala la rushwa, Kandoro na dhuluma katika jamii, Kandoro na Umasikini katika jamii na Kandoro na demokrasia. Baada ya kupatikana uhuru Kandoro aliendelea na kazi yake ya kutunga mashairi ya kuhamasisha jamii katika nyanja mbalimbali miongoni mwao ni pamoja na kufanya kazi kwa bidii, uongozi wa nchi, masuala ya kijinsia, kuweka akiba, maisha bora, kudumisha amani pamoja na Ujamaa na Kujitegemea. Pia mambo mengine ni mapenzi kwa taifa, ushereheshaji wa sera za maendeleo, Afrika ni moja pamoja na suala la mgogoro wa ushairi wa Kiswahili.

Baada ya hapo, sura hii imeendelea kuwasilisha mbinu mbalimbali za kisanaa zilizotumia na Kandoro katika kuwasilisha masuala ya kisiasa katika ushairi wake. Mbinu hizo ni pamoja na matumizi ya lugha uchanganyaji wa lugha, tamathali za usemi kama vile tashihisi, taswira na Ishara, marudiorudio, matumizi ya wahusika na mandhari katika ushairi wa Kandoro. Mbinu nyingine za kisanaa ni matumizi ya lugha ya mkato, mwingiliano matini, mbinu ya mazungumzo, na muundo katika ushairi wa Kandoro. Vipengele vingine ni mtindo, usimulizi na mwisho ni muhtasari

wa mbinu za kisanaa. Suala jingine lililowasilishwa katika sura hii ni falsafa ya Kandoro kama inavyojitokeza katika ushairi wake.

Sura ya sita ya tasinifu hii imeeleza juu ya muhtasari wa kila sura, hitimishi na mapendekezo ya utafiti wa siku zijazo. Pia mapendekezo kwa wahakiki na wasomaji wa ushairi kwa ujumla na ule wa Kandoro yametolewa. Kwa ujumla sura hii imeeleza kwa ufupi juu ya yaliyomo katika tasinifu hii yanavyoingiliana, jengana na kukamilishana sasa ni hitimishi.

## 6.3 Hitimishi

Utafiti huu ulilenga kukamilisha maswali matatu ya utafiti. Maswali hayo yamejibiwa katika tasinifu hii na kuufanya utafiti kukamilika. Swali la kwanza liliulizwa ni masuala gani ya kisiasa yanayojitokeza katika ushairi wa Kandoro? Utafiti huu umebaini kwamba, Kandoro anazungumzia masuala ya kisiasa katika vipindi vikuu viwili. Kipindi cha kwanza ni kile cha ukoloni na cha pili ni wakati wa uhuru na kuendelea. Katika kipindi cha ukoloni mengi ya mashairi ya Kandoro yaliandikwa kwa lengo la kuhamasisha wananchi kuungana pamoja katika kudai uhuru. Kandoro aliandika shairi *Kwetu ni kwao kwa nini* kwa nia ya kuwaamsha wananchi katika kuona kwamba, hakuna haja ya kuendelea kutawalia na wakoloni. Shairi hili linatoa hasira kwa yoyote alisomaye na kulielewa na hivyo kuona kwamba, jitihada za kudai uhuru zinatakiwa kuongezwa tena kwa kasi ya hali ya juu.

Utafiti huu pia unaonesha kwamba, katika kipindi cha ukoloni serikali ya kikoloni haikuwapatia Waafrika nafasi ya kuwa na viti vingi katika baraza la wawakilishi. Katika shairi la *Kitumike Kiswahili*, Kandoro anaonekana kudai nafasi sawa ya

uwakilishi katika baraza la Tanganyika. Kukosekana kwa wawakilishi wa kutosha katika baraza la Tanganyika Waafrika walinyimwa haki yao ya msingi katika maamuzi. Maamuzi mengi yaliyofanywa na baraza la wawakilishi yaliwaumiza wananchi kwa njia moja ama nyingine. Miongoni mwa maamuzi hayo ni lile la *Kura Tatu*. Kama Waafrika wangekuwa na ushiriki wa kutosha katika baraza uamuzi huu usingefanikiwa kupita na kuwa sheria. Hata hivyo, bado Kandoro aliwataka wananchi kuungana pamoja kama “Siafu” ili kuhakikisha kwamba, haki zao zinapatikana. Nao walifanya hivyo na kisha wakafanikiwa.

Vilevile, utafiti wetu umegundua kwamba, Kandoro aliwahamasisha wananchi kujiunga na chama cha TANU ili kukipa nguvu kiweze kufanikisha harakati za kudai uhuru na baadaye kutawala nchi. Aliwahimiza wananchi kujiunga na chama kwa kuwakumbusha juu ya hali mbaya ya umasikini waliyonayo na kwamba uhuru ukipatikana na TANU ikashika hatamu basi maisha yao yatakuwa mazuri tofauti na ilivyokuwa katika kipindi ukoloni.

Vilevile, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, Kandoro alitambua kwamba, kudai uhuru ni kazi ngumu sana na hivyo aliwatahadharisha wananchi kutokata tamaa kutokana na changamoto za kudai uhuru. Shairi la *Msiogope mawimbi* ndilo hasa linaloeleza namna wananchi wanavyotakiwa kufanya ili kuhakikisha kwamba wanashinda vita ya kudai uhuru.

Kwa upande mwingine, Kandoro anaonesha kwamba, huduma muhimu kama vile elimu haikutolewa kwa Waafrika na hivyo kuwafanya kuonekana kama “majitu haini”, msemo wa Kandoro katika moja ya mashairi yake. Matokeo ya utafiti

yanaonesha kwamba, Waafrika hawakupatiwa nafasi ya kupata elimu katika shule za serikali na hata zile zilizokuwa chini ya Kanisa. Kutokana na hali hii Kandoro anawahamasisha wananchi kuamka na kuanza kudai haki zao mojawapo ikiwa ni elimu. Hili litawezekana pale ambapo nchi itakuwa huru na kuwa na utawala wake.

Pia matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, Waafrika walinyang'anywa ardhi yao hasa ile iliyokuwa na rutuba na kuachwa na ardhi isiyokuwa na rutuba. Kandoro anaona kwamba, mtu asiyekuwa na ardhi kwa ajili ya kilimo ni mtumwa. Vilevile, kwa hali hiyo Mwafrika ataendelea kuwa masikini daima dumu kwa kukosa ardhi. Wakoloni walihitaji ardhi iliyo na rutuba ili waweze kufanya uzalishaji wa kutosha kuweza kukidhi mahitaji yao na faida yao. Kandoro anawataka wananchi kuchachamaa katika kuikomboa nchi yao ili waweze kumiliki ardhi yao na kuendeleza shughuli mbalimbali za uzalishaji mali kilimo kikitawala.

Vilevile, utafiti wetu umegundua kwamba vitendo vya rushwa katika jamii vinarudisha nyuma harakati za kujiletea maendeleo. Kandoro anaonesha kwamba, wanaochukua rushwa ni viongozi wakuu katika serikali. Kwa kufanya hivyo wanakuza utabaka katika jamii kati ya walionacho na wasionacho. Rushwa inahatarisha upatikanaji wa haki za binadamu kama vile afya, maji, umeme, elimu na kadhalika pale wananchi wanapokosa fedha za kutoa rushwa. Wengi kati ya wanaokosa haki zao kwa kukosa fedha za rushwa ni wananchi wa kipato cha chini. Kandoro anawataka wananchi kupambana katika kujenga serikali yao wao wenyewe ambayo itahakikishia kwamba rushwa inatokomezwa.

Si hivyo tu, bali pia, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba Kandoro alipinga sana dhuluma iliyofanywa dhidi ya Waafrika. Kitendo cha wakoloni kuchukua rasilimali za Wafrika kama vile ardhi, madini, mito na mabonde, rasilimali watu, wanyama pori na kadhalika ni dhuluma kubwa dhidi ya wananchi. Rasilimali hizi zilidhulumiwa kwa kuchukuliwa bure kabisa na wakoloni na kwenda kunufaisha nchi zao mpaka kufikia hatua ya maendeleo waliyofikia hivi sasa. Kandoro anawataka wananchi kupambana mpaka hatua ya mwisho na kuhakikisha kwamba mkoloni anaondoka nchini na nchi inakuwa huru na rasilimali zake zinatumiwa kwa masilahi ya wananchi wote.

Pia, utafiti wetu umegundua kwamba suala la umasikini limejitokeza sana katika ushairi wa Kandoro. Kandoro anabainisha kwamba, Mwafrika anakabiliwa na maadui watatu ambao ni ujinga, maradhi na umasikini. Hata hivyo, anaonesha kwamba umasikini wa Mwafrika umesababishwa na mkoloni. Hali ya Waafrika kukosa chakula, malazi na mavazi kulisababishwa na wakoloni kwa namna mbalimbali miongoni mwa namna hizo ni ile ya kuchukua ardhi ya wananchi iliyo na rutuba na kuwaachia ardhi isiyofaa kwa kilimo. Hali hii ilifanya jamii kuishi maisha ya umasikini, uliokithiri. Kwa mantiki hii Kandoro aliwataka wananchi kuhakikisha kwamba, wanafanya kila linalowezekana kukomboa nchi yao. Hili lilifanikiwa kwa kiasi chake.

Baada ya kupatikana uhuru, Kandoro aliendelea kutunga mashairi mbalimbali ya kuhamasisha harakati za kujiletea maendeleo. Jambo la kwanza alilosisitiza ni kufanya kazi kwa bidii ili kufuta hali mbaya ya maisha iliyoachwa na wakoloni. Kandoro anawakumbusha wananchi kwamba, uhuru umekwisha patikana

kinachotakiwa sasa ni kuchapa kazi kwa juhudi na maarifa ili kujiletea maendeleo. Pia alikemea wananchi kutojenga fikra ya utegemezi wa aina yoyote kutoka kwa wahisani kwani misaada yao haitaisaidia nchi kuwapatia wananchi wake maendeleo na badala yake umasikini utaongezeka.

Matokeo ya utafiti yanaendelea kuonesha kwamba, uongozi imara ndio ngao ya maendeleo na hivyo Kandoro anawataka viongozi wakuu wa nchi kuhakikisha kwamba wanaitawala nchi vizuri ili kutimiza ndoto na matarajio ya wananchi kuhusu kujiletea maendeleo. Kandoro anaonesha kwamba, raisi wa nchi peke yake hawezi kamwe kuletea taifa maendeleo bila kushirikiana na wenzake yaani mawaziri. Kwa hali hiyo anamtaka rais pamoja na mawaziri wake kuwa waadilifu katika kuwatumikia wananchi na katu wasirejeshe madhila na maovu ya wakoloni kwa raia wake.

Kwa upande mwingine Kandoro anakiri kwamba, kujitawala ni kugumu na wananchi wasifikiri kwamba, kupatikana kwa uhuru ndio kila jambo litakuwa rahisi tu kupatikana. Nchi iliyopewa uhuru na wakoloni bado ni changa sana na hivyo uvumilivu wa hali ya juu unahitajika miongoni mwa wananchi. Uvumilivu huo ni pamoja na kuisaidia serikali yao kwa kuziunga mkono sera mbalimbali za maendeleo. Kwa kufanya hivyo itakuwa ni rahisi kwa wananchi na serikali yao kujiletea maendeleo endelevu.

Pia, matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba Kandoro alitawaliwa na mfumo dume kiasi cha kuona kwamba, mwanamke hana mchango katika harakati za ukombozi na kwamba mwanamke hachukii kutawaliwa. Kauli hii ya Kandoro

inamwonesha kwamba yupo nyuma katika kuelewa mchango wa mwanamke katika ukombozi wa Tanganyika. Vilevile, inawezekana Kandoro anafahamu vizuri mchango wa wanawake katika maendeleo ya nchi lakini tatizo ni kwamba, katika kuhakikisha kwamba anapata vina katika ushairi wake ndio maana akasema:

*Ni mume si mwanamke, aliniambia fahamu,*
*Mtawaliwa mcheke, cheko ya kumlaumu,*
*Na tena yapambazuke, kujitawala kugumu,*
*Kujitawala kugumu, tujikongoje tufike.*

Ukiutazama msitari wa kwanza utaona namna uzingativu wa vina ulivyomponza Kandoro na kumfanya mwanamke aonekana kama kiumbe dhaifu asiyejali kutawaliwa na kufurahia jambo hilo.

Vilevile, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, Kandoro anawahimiza wananchi kuhakikisha kwamba, wanaweka akiba zao katika benki ili wazitumie kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo kama vile kuwasomesha watoto wao kulipia sehemu ya huduma muhimu za maisha na kadhalika. Pia serkali nayo itaweza kuzitumia fedha hizo pindi zinapokuwa benki katika kuimarisha huduma mbalimbali ili kuwapatia wananchi maisha bora.

Pia, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, Kandoro alihamasisha wananchi kulikubali Azimio la Arusha lililoanzisha sera ya Ujamaa na Kujitegemea. Kandoro anaoenesha kwamba, Ujamaa na Kujitegemea ndio njia pekee itakayosaidia kuleta usawa wa mwanadamu wa Kiafrika ambaye ameonewa sana na serikali ya Kikoloni. Kupitia Ujamaa na Kujitegemea kulianzishwa vijiji vya ujamaa ambapo wananchi walizalisha mali na kuzitumia kwa usawa mali hizo baina yao. Huduma mbalimbali

ambazo walizikosa kipindi cha ukoloni kama vile elimu, maji safi na afya walizipata kwa hakika katika vijiji yao vya Ujamaa na Kujitegemea.

Swali la pili la utafiti huu liliuliza juu ya mbinu mbalimbali za kisanaa zilizotumiwa na Kandoro katika kuwasilisha masuala ya kisiasa katika ushairi wake. Utafiti huu umegundua kwamba, matumizi ya lugha ya kisitiari yametawala katika ushairi wa Kandoro. Sitiari hizo ni kama vile picha, ishara na taswira ambazo kwazo ndimo maudhui ya kisiasa yamefichwa na Kandoro. Ili kuufanya ushairi wake kuwa imara katika kuwasilisha masuala ya kisiasa Kandoro ametumia mbinu ya wahusika, marudiorudio pamoja na usimulizi wa nafasi mbalimbali. Kama ilivyo kwa mja haachi asili Kandoro ametumia vina na mizani katika kuupamba ushairi wake kwa nia ya kutoa msisitizo wa masala ya kisiasa kwa wasomaji wa wasikilizaji wa ushairi wake.

Swali la tatu la utafiti huu liliuliza juu ya falsafa ya Kandoro kama inavyojitokeza katika ushairi wake. Utafiti umegundua kwamba, Kandoro ametawaliwa na falsafa ya kimapinduzi hasa mapinduzi ya kisiasa. Aonavyo yeye ni kwamba, maisha bora kwa wananchi yatapatikana iwapo nchi itakuwa huru na kutawaliwa kwa ridhaa ya wananchi wake. Katika kuitetea falsafa yake hii Kandoro ameonekana kuwahamasisha wananchi kufanya kila linalowezekana ili kumuondoa mkoloni kisha kujitawala wenyewe. Njia ya kwanza aliyoipendekeza ni ile ya wananchi kujiunga pamoja na kuwa na mshikamano imara utakaowawezesha kumng’oa mkoloni. Hili lilifanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Vilevile, Kandoro anaonekana kuiimarisha falsafa yake ya kimapinduzi kwa falsafa nyingine ya Ujamaa na Kujitegemea. Ingawa wazo la Ujamaa na Kujitegemea lilitolewa na Mwalimu Nyerere, Kandoro alilipokea wazo hilo na kulifanya kuwa falsafa yake nyingine. Falsafa hii inajitokeza pale anapowahimiza wananchi kulikubali Azimio la Arusha kwa mikono miwili. Ameeleza kwa undani faida za Ujamaa na Kujitegemea na kwamba haina budi kwa kila mwananchi mpenda usawa, maendeleo, haki na heshima kulikubali Azimio hilo. Ndani ya falsafa hii kukazaliwa falsafa ya utu na wema wa kibinadamu katika ushairi wa Kandoro. Falsafa hizi kimsingi, zinaendana na nia hasa ya Kandoro ya kuhakikilisha kwamba wananchi wanaishi maisha ya amani, upendo, utulivu, kuheshimiana, usawa na furaha. Hili nalo liliweza kufanikiwa kwa kiasi fulani ingawa kulikuwa na mapungufu ya hapa na pale.

## 6.4 Mapendekezo

Tunapendekeza kwamba, utafiti kama huu ufanywe katika kuwachunguza washairi wengine wanaeleza masuala gani ya kisiasa. Hii itawawezesha kuibua utajiri mkubwa wa ujuzi wa elimu kuhusiana na masuala ya kisiasa katika jamii ili kuimarisha muktadha huu adhimu katika maendeleo ya nchi.

Vilevile, tunapendekeza kwamba ufanyike utafiti wa kuitazama falsafa ya Kandoro kwa undani kabisa katika utafiti wa Uzamili na Uzamivu. Utafiti huu uliifanya falsafa ya Kandoro kama moja ya madhumuni yake mahususi tu.

Pia tunapendekeza kwamba, utafiti wa baadaye ufanyike kuchunguza mbinu mbalimbali za kisanaa zinazotumiwa na Kandoro na kuzilinganisha na washairi

wengine wa ushairi wa Kiswahili. Washairi hawa wanaweza kuwa ni wale wa upande wa mapokeo na wanausasa.

Si hivyo tu, bali pia tunapendekeza utafiti kwa upande wa migogoro inaojitokeza katika ushairi wa Kandoro ufanyike kwa minajili ya kuhusianisha na migogoro inayojitokeza katika jamii ya wakati huu.

## MAREJELEO

Alhabib, E.A., (2012), "Matumizi ya Taswira katika Nyimbo za Taarab, Tasinifu ya *M.A. Kiswahili,* CKHT.

Ali, M. (1978), "Utangulizi katika Kandoro S.A., *Liwazo la Ujamaa* Dar es

Aronson, J. (1992) "A Pragmatic View of Thematic Analysis" in the *Qualitative Research Methods in Nursiny*. Pp (37-73). Oro lando FL: Grune& Stratton.

Babbie, E., (1999), *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth

Bathes, R., (1994), *The Semiotic Challenge* Berkely: University of Califonia Press.

Benner, P., (1985), "Quality of Life: A phenomeno logical perspective on explanation, prediction and Understading in Nursing Science", *Advanees in Nursing Science*, 8(1), 1-14.

Bogdan, R. (and Biklen, S.K., (1992), *Qualitative Research of Education: An introduction to Theory and Methods,* (end ed), Boston: Allyn and Bacon.

Bulaya, J., (2012), "Bongo Fleva na Siasa: Uchambuzi wa Ndiyo Mzee na Siyo Mzee za Profesa Jay", katika *Mulika*, Namba 29&30. TATAKI.

Chandler, D., (1992), *Semiotics: The Basics* London, Routledge. Press.

Chohen, L. et, al., (2000), *Research Methods in Education* (5th end) London:

Chuachua, R., (2011), *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*, Dar es Salaam: TATAKI.

Creswell, J.W., (2009), *Research Design: Qualitative, Quantitatie, and Mixed Methods Approaches*. Los Angeles: SAGE Publication.

Frolova; N., (2003), "Euphrase Kezailahabi: The Renewal of Kiswahili Poetry. In *Kiswahili*, Vol. 66 Dar es salaam. IKR.

Furlong, N. *et, al*., (2000), *Research Methods and Statistrics: An Integrated Approach*. New York: Harcourt College Publishers.

Isaac & Michael., (1981), *Handbook of Reserch and Evalution: A Collection of Principles, Methods and Strategis Useful in the Planning, design and Behaviour al Science*, San. Diago: Edips.

Ismail, J.H., (2012), "Nafasi ya Nyimbo za Bongo Fleva katika Uelimishaji wa Haki katika Jamii". Katika *Mulika*. Namba 29&30, Dar es Salaam: TATAKI.

John, L., (2004), *Critical Reading: A Guide.* In http://www. Brocku. Ca/English/jlge/criticalreadig. Html. Accesssed, 30th, October 2006.

Kandoro, S., (1978), *Ushahidi wa Mashairi ya Kiswahili na Lugha Yake*. Dar es Salaam: Longman Ltd.

Kandoro, S.A, (1972), *Mashari ya Saadan* Dar es Salaam: NPL.

Kandoro, S.A., (1961), *Mwito wa Uhuru*. Dar es Salaam: MNP.

Kandoro, S.A., (1978), *Liwazo la Ujamaa*. Dar es Salaam: TPH.

Kanppet, I.J. (1974), "The Appreciation of Kiswahili Poetry". *In Kiswahili Vol. 44/2,* September, Dar es Salaam: IKR.

Keys, B. na Wenzake (1989), "Four Faces of Fully Function Middle Manger; California Management Review; Vol. XXIV. No, 4 pp. 59-67.

Kezilahabi, E., (1974), *Kichomi,* Nairobi: Heinemann Educational books.

Kezilahabi, E., (1977), "Mashari ya Saadan*", Mulika,* Namba 14. Dr es Salaam: TUKI. Kur. 32-40.

Kezilahabi, E., (1983), "Uchambuzi katika ushari wa Kiswahili". Katika *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandsihi wa Kiswahili,* Kur. 145-165. Dar es Salaam: TUKI.

Kezilahabi, E., (1988): *Karibu Ndani* Dar es Salam: DUP.

Khalifa, A.I.S., (2012), "Usawiri wa Masuala ya Kijinsia katika Lugha ya Mashairi. Mifano Kutoka Mashairi ya Bongo Fleva Tanzania", Dar es Salaam. Tasnifu ya *M.A. Kiswahili*. CKHT.

Kitogo, S.A., (2002), "The Poets Contribution to Political Development: A case of Saadan Abdul Kandoro", Unpublished *M.A. Thesis* UDSM.

Kiwanuka, K.M., (1978), "Utangulizi in Kandoro S.A., *Liwazo la Ujamaa.* Dar es Salaam: TPH. Pp. vi-vii.

Kothari, C.R., (1992), *Reserch Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Limited.

Kothari, C.R., (2008), *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Leininger, M.M., (1985), "Ethnography and Ethnonursing: Model and Modes of Qualitative Data Analysis". In. M.M. Leininger (Ed.). *Qualitative Research Methods in Nursiny*. Pp (37-73). Oro lando FL: Grune& Stratton.

Low, N.R., (2011), "Athari ya Lugha Katika Kuibua Dhamira: Mifano kutoka Nyimbo za Kizai Kipya zinazohusu UKIMWI", Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kiukuu cha Dar es Salaam.

Madaso, "Ng'wanza (2009), Serikali yafanya Kufuru", Katika http://www.jamiifrums.com/habari- na-hoja-mchanyiko/40975 - serikali-yafanya-kufuru print. html. imesomwa tarehe 15/02/2010.

Maguire, A.G. (1969), *Towards "Uhuru" in Tanzania. The Politics of Participation.* London: Oxford University Press.

Mpangala, G.P., (1977), *Political and Social Development in Afrika* Dar es Salaam: DUP.

Mpangala, G.P., (2004), "Conflict Resolution and Peace Building in Africa as a Process: Case Studies of Burundi and the Democratic Republic of Congo", Dar es Salaam: MNF, *Nyerere Week Conference*.

Mpangala, G.P., (2007), "The Role of Civil Society in the 2005 General Elections in Tanzania", In, Tanzania *Journal of Development Studies,* Vol. 7, No. 2 Pp. 1-18. Dar es Salaam: IDS.

Msuya M.B. na A.P. Lupokela, (2012), "Dhima ya Bongo Fleva katika Maadili na Malezi kwa Jamii", Katika *Mulika,* Namba 29&30, Dar es Salaam: TATAKI.

Mulokozi, M.M. na K.K. Kahigi (1979), *Kunga za Ushari na Diwani Yetu*, Dar es

Mulokozi, M.M. na T.S.Y. Sengo (1995), *History of Kiswahili Poetry* [AD 1000-2000]. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M.M., (1975), "Revolution and Reaction in Swahili Poetry". *In Kiswahili, Vol. 45/2.* Dar es Salaam: IKR, Kur. 46-65.

Mulokozi, M.M., (1982), "Protest and Resistance in Swahili Poetry: 1600– 1885", *Kiswahili Vol. 49/1.* Dar es Salaam: IKR, pp. 25-51.

Mulokozi, M.M., (1996). *Fasihi ya Kiswahili* Dar es Salaam: IKR.

Newman, W.L., na Wenanzake, (2006), *Social Research*. Sixth Edition, Boston: Pearson.

Njogu, K. na Rocha., C. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi, JKF.

Nyerere, J.K. (1963), *Democracy and Party System*. Dar es Salaam: Tanganyika Standard.

Nyerere, J.K. (1967). *The President Explains the Arusha Declaration*. Dar es Salaam: National Printing Co.

Omari, S. (2008), "Mtindo na Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya Tanzania", Katika *Kiswahili*, Juzuu 69. TUKI. Kur. 73-92.

Omari, S. (2009), "Tanzania Hip Hop As Popular Literature", Unpublished PHD. *Thesis UDSM*.

Omary, M., (2011), "Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa *Karibu Ndani* (1988) na *Dhifa* (2008), Tanisifu ya M.A Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Oslon, S.H,, (1975), "Philosophical Implications of Some Swahili Idioms", In *Kiswahili* Vol. 45/2, Dar es Salaam: IKR. Pp. 32-37.

Publishing Company.

Raffel, B., (1984), *How to Red a Poem*. New York: Penguin Publishers. *Report*. Vol. 2, No. 1.

Robert, S. (1951), *Kusadikika*. London: Nelson.

Robert, S.(1967), *Kufikirika*. Nairobi:OUP.

Robert, S. (1968,) *Siku ya Watenzi Wote*. London: Nelson.

Robson, C., (2007), *How to do a Reserch Project*: A Guide for Undergraduate Students, Carton Victoria: Blackwell Publishing.

Samwel, M. (2012), "Masuala ya Kisasa katika Mashairi ya Mapenzi ya Muziki wa Bongo fleva", Katika *Mulika,* Na. 29&30. Dar es Salaam: TATAKI.

Sanka, S.M., (1994), "Semantic Deviation in Iraqu Oral Poenty". Unpublished *M.A Dissertation,* UDSM.

Senkoro, F.M.E.K., (1982), *Fasihi*. Dar es Salaam: DUP.

Senkoro, F.E.M.K., (2006), "Fasihiya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi simulizi na Fasihi andishi", katika, *Kioo cha Lugha*, Juzuu, 1. Idara ya Kiswahili chuo kikuu cha Dar es Salaam uk. 61-68.

Taylor, S.J. & Bogdan. R., (1984), *Introduction to Qualitative Research Methods: The Search for Meanings*. New York: John Wiley& Sons.

Topan, F., (1974), "Utangulizi katika *Kichomi*", Nairobi: Heiremann.

Wamitila, K.W., (2002), *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake,* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K.W., (2008), *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.

Warren, A. and Wellek. R., (1985), *Theory of Literature*, London: Penguin Group: London.

Yin, R.K., (1994), *Case Study Research: Design ad Methods*, (2nd eds. Thousands Oaks Calif: SAGE publishers.

# VIAMBATISHI

## Kiambatishi A: DODOSO KWA AJILI YA USAILI

## WALENGWA: NDUGU WA KARIBU NA SAADAN KANDORO

**Utangulizi**

Mimi ni Mohamed Yunus mwanafunzi wa shahada ya Uzamivu katika Kiswahili katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Ninaomba nikuulize mswali machache ili unipatie majibu ambayo yatawezesha kukamilika kwa utafiti wangu. Natanguliza shukurani zangu za dhati kwa kukubali kwako.

**UTAMBULISHO**

Jina……………………………

Uhusiano wako na Saadan Kandoro………………………………….........................

**Maswali**

1. Tueleze kwa ufupi juu ya historian a maisha ya Saadan Kandoro.
2. Saadan Kandoro alikuwa anapendalea masuala gani na yapi alikuwa anayachukia?
3. Saadan Kandoro alikuwa mwanasiasa na wakati huo huo mshairi wa mashairi ya Kiswahili, kwa maoni yako aliweza kutimiza majukumu yote haya mawili kwa ufanisi uliopaswa?
4. Saadan Kandoro aliandikiana Mashairi na Mwalimu Nyerere, nini maoni yako kuhusiana na suala hili?
5. Uliwahi kumsikia Saadan Kandoro akizungumza jambo lolote kuhusu ushairi wa kimapokeo na ule wa Kisasa? Ni mambo gani aliyokuwa akiyazungumzia?

6. Kabla ya kufariki dunia Saadan Kandoro aliwaachia wasia gani ninyi wanafamilia yake? Je, alitoa wasia kuhusu taifa? Ni wasia gani huo?
7. Saadan Kandoro alikuwa akitazamaje masuala ya rushwa na ufisadi katika jamii?
8. Kwa nini Saadan Kandoro hakuwa tajiri mkubwa kama ilivyo kwa wanasiasa wa siku hizi?
9. Unaelewa nini kuhusu falsafa ya maisha aliyokuwa nayo Saadan Kandoro?
10. Nini maoni yako ya jumla kuhusu ushairi wa Saadan Kandoro na maisha yake mpaka umauti ulipomkuta?

**ASANTE SANA KWA USHIRIKIANO ULIONIPATIA**